# Nipashe

Jumanne Desemba 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581158

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





Ni safari ya saa nne kwa basi kutoka Dar Es Salaam hadi Kijiji cha Njia Nne Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi. Baada ya hapo inaanza safari mpya ya bodaboda inayotumia takribani dakika 50 kutoka Njia Nne hadi Nahama, kijiji kilichoko kata ya Namayuni wilayani humo.

Kijiji cha Nahama chenye idadi ya wakazi 1,786 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 ni miongoni mwa vijiji 33 katika wilaya ya Kilwa ambavyo vinakabiliwa na uhaba wa majisafi na salama kwa matumizi ya watu na mifugo.

Miongoni mwa waathirika ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao nao hukabiliwa na tatizo la kuacha masomo ili kwenda kusaka maji kwa ajili ya familia zao nyumbani na pia kwa matumizi ya shule.

Mathalani, Mwandabu Said anasoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Nahama, akiwa na baadhi ya wenzake ni kama...

UKURASA 13




## Watano mbaroni tuhuma za kuiba mtoto mchanga



UKURASA 5



RIPOTI MAALUM

KUOKOTWA MAITI PORINI...

# Wenyeji waliliona gari, polisi imebaki kimya kwa siku 124

UKURASA 4

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**SHAHIDI ADAI KUOMBWA RUSHWA NA ASKARI POLISI**

MVUVI Boi Rajabu anayetuhumiwa kumuua Abas Mwijuma, amedai kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa...

UKURASA WA 3

**WANACCM WARIDHISHWA UTENDAJI DK. MWINYI**

WANACHAMA na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamesema wana matumaini makubwa ya kuongezeka...

UKURASA WA 9

**WATOTO 96 WAFANYIWA UDHALILISHAJI LUDEWA**

JUMLA ya watoto 96 wenye umri wa chini ya miaka mitano wameripotiwa kufanyiwa vitendo vya ubakaji kwa kipindi cha...




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitazama mashine ya maabara alipokagua ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Katavi jana. **PICHA: OWN**

## TRA yaja na msako mkali wasiotoa na kudai risiti

UKURASA 2

MAUAJI YA TRAFIKI

UKURASA 3

# Mshtakiwa: Sijui chochote


**MICHEZO** SIMBA YAPEWA RAJA, YANGA WATUNISIA UK.32 **KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Meneja wa TRA Mkoa wa Kodi Kariakoo, Alex Katundu, akionyesha kipeperushi cha kuelimisha wateja umuhimu wa kuhakiki risiti halisi ili kuepuka udanganyifu wa kukwepa kodi **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Wasiotoa, kudai risiti kukiona

**Na Beatrice Moses**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), mkoa wa kikodi Kariakoo, imetangaza msako mkali kwa wafanyabiashara na wateja wasiotoa na kudai stakabadhi baada ya kuuza au kununua bidhaa.

Kadhalika, imeweka mtego kwenye maeneo yanayofanya biashara nyingi, ikiwa ni mkakati maalumu wa kuwanasa wanaokwepa kodi.

Mamlaka hiyo kwa mwezi mmoja imewakamata wateja wasio waaminifu kati ya 50 hadi 60 na wafanyabiashara 13 walioonywa na kuendelea kukwepa kodi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Mkoa wa Kikodi Kariakoo, Alex Katundu, alisema msako huo utawabana wafanyabiashara wadogo (wamachinga) kuwa na mashine za kutoa risiti kila bidhaa wanazouza katika maeneo hayo.

Alibainisha kuna udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kupitia wamachinga, wanawatumia kuuza bidhaa mbalimbali, lakini hawalipi kodi inavyotakiwa.

"Tumebaini baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wanakwepa kodi kupitia wamachinga, katika kufanikisha mikakati tuliyojiwekea tayari tumeshafanya usajili wa wamachinga 5,373, wamepewa namba ya mlipakodi (TIN) na watapewa mashine, wale ambao hawajasajiliwa wanapaswa kujisajili haraka," alisema.

Hatua hiyo alisema inatokana na juhudi za awali walizofanya za kuweka mabango ya elimu ya kukumbusha umuhimu wa kuchukua risiti halali.

Katindi alisema pia watahakikisha wanabandika stika zenye kuonesha TIN za mwenye duka kwenye kila duka Kariakoo, ili kila mteja aweze kuhakiki taarifa zilizoko kwenye risiti ya EFD wanazopewa.

"TRA tunaamini kupitia mkakati huu tutaboresha usimamizi wa kodi kwenye eneo hili, tunakusudia kipindi cha Desemba tutakusanya mapato ya Sh. bilioni 19.


IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI
BILL OF COST NO.4 OF 2021
J.S.KHAMBHAITA...............PLAINTIFF
VERSUS
SHEILA CHRISTOPHER DANIEL & OTHERS.........DEFENDANT

TO: ELINE WILFRED ABRAHAM NYANGE .

NOTICE FOR MENTION,

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on **15th February,2023 at 10:00 a.m.** before Honourable Judge in charge.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this **29th day of NOVEMBER ,2022**

DEPUTY REGISTRAR

17192302



SPECIAL RESOLUTION

TIM MOTORS TANZANIA LIMITED (141119621)

EXTRACT FROM THE MINUTES OF TIM MOTORS TANZANIA LIMITED'S MEMBERS MEETING HELD ON 18TH DAY OF SEPTEMBER 2021 AT ITS REGISTERED OFFICES IN DAR ES SALAAM, TANZANIA.

It was unanimously **RESOLVED** by the Members that the following resolution be adopted: -

a) That, the company has failed to operate and as a result it has been generating unsatisfactory financial results over time,
b) That, the shareholders of the above-mentioned company do not intend to continue with the operation of the company.
c) That, the Company is to be voluntarily wound up.
d) That, the company is appointing **MR. FRANK ELIAS KIFUNDA** as a liquidator for the purpose of winding up the affairs of the company and distributing the company's assets.

It was further resolved that all changes should be notified to the registrar of companies.

Chairman
JIAN YUE

TIM MOTORS TANZANIA LIMITED
P. O. Box 12348
DAR-ES-SALAAM

Secretary
XIAOPENG ZHONG

17192402


# Shahidi adai kuombwa rushwa na askari polisi

**Na Grace Gurisha**

MVUVI Boi Rajabu anayetuhumiwa kumuua Abas Mwijuma, amedai kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa kabla ya kuchukuliwa maelezo na askari polisi, alimuuliza kwenye simu yake kulikuwa na kiasi gani, akimjibu kulikuwa na Sh. 100,000 na kuahidiwa kusaidiwa na askari huyo.

Pia amedai wakati anachukuliwa maelezo akiwa ameketi chini, aliulizwa kuhusu majina yake, kazi yake na watoto wake na pia alilazimishwa kutia saini maelezo ambayo hakuyasoma wala kusomewa kilichoandikwa.

Rajabu alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya wakati akitoa utetezi katika kesi ya mauaji ya Mwijuma inayomkabili mahakamani huko, akituhumiwa kutenda kosa hilo Februari 8, 2019 eneo la Mbweni mkoani Dar es Salaam.

Akiongozwa na wakili wake, Hilda Mushi, Rajabu alidai anakumbuka tarehe hiyo ya tukio alikuwa amelala na aliamshwa na mlio wa simu na alipoangalia simu yake aliona mtoto wake Kulwa anampigia.

Alidai kuwa alipopokea simu hiyo, mtoto wake alimuuliza alikokuwa, akamjibu alikuwa nyumbani kwake amejilaza na kutakiwa aende nyumbani kwa mwanawe.

Rajabu alidai kuwa baada ya kufika huko, mtoto wake alimwambia kuwa shangazi alikuwa amemwambia kuwa amesikia kuwa amemuua mtu, akamkatalia kuwa yeye hawezi kufanya kitu kama hicho kwa kuwa dini, serikali na hata mila zinakataza.

Baada ya hapo, mtoto akafikiria akamwambia kuwa alale hapo nyumbani kwake na kulipokucha, alimuaga mtoto wake kuwa anatoka kwenda kutafuta riziki na alipofika njiani eneo la Maputo, Mbweni alikutana na vijana wawili. Alidai kuwa vijana hao walimwambia yuko chini ya ulinzi kwa kosa la mauaji, hakubishana nao kwa sababu anajua yeye si muuaji, wakamchukua na kumpeleka Kituo cha Polisi Mbweni. "Vijana hao walinifikisha nje ya kituo cha polisi, kila askari aliyekuwapo alinipiga na kunikanyaga na kunieleza kuwa mimi ni muuaji, baada ya mateso hayo alikuja askari mmoja Erasto akanitoa hapo akaniingiza kwenye chumba cha mahojiano.

"Tulifika kwenye chumba yeye alikaa kwenye kiti, akaniambia nikae chini huku akiwa ameshika simu yangu akaniuliza nina shilingi ngapi kwenye simu, nikamwambia ni Sh. 100,000 akaniambia 'basi nitakusaidia'," alidai Rajabu.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa baada ya hapo, askari huyo alianza kuchukua maelezo kwa kutaka amtajie jina lake, kazi yake na watoto wake na baadaye alimlazimishwa kutia saini huku akimpiga vibao bila kupewa kusoma wala kusomewa maelezo hayo.

Akizungumzia kuhusu marehemu, alidai anamfahamu kama jirani yake na tangu mwaka 2000 hajawahi kumwona Mwijuma akifanya shughuli yoyote ile zaidi ya kufanya alichokiita 'kubwia unga tu'.

Kuhusiana na ushahidi wa askari polisi Erasto kuwa ana matatizo ya macho, Rajabu alidai si kweli yeye hajawahi kupata matatizo ya macho tangu azaliwe na anasoma vizuri bila shida.

Upande wa utetezi umefunga utetezi wake, huku Wakili Mushi akiomba awasilishe majumuisho ya mwisho na mahakama imekubali na atayawasilisha ndani ya siku 21 na hukumu itasomwa Januari 31, mwakani.

HABARI KITAIFA

# Wana-CCM waridhishwa na utendaji wa Rais Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WANACHAMA na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamesema wana matumaini makubwa ya kuongezeka uwajibikaji kwa watumishi wa chama hicho baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kukabidhiwa rasmi nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar.

Wakizungumza na waandishi wa habari Mkoa wa Kusini Unguja Kaskazini na Mkoa wa Mjini Magharibi siku moja baada ya Mwinyi kupokewa kwa kishindo, walisema kitendo cha wananchi na wanachama kujitokeza kwa wingi kumpokea kunaonesha wameridhishwa na utendaji wake wa kazi kwa kupambana na rushwa na ufisadi.

"Kitendo cha kukabidhiwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni imani kubwa ya mabadiliko kwa Zanzibar pamoja na kuimarisha utekelezaji wa ilani ya uchaguzi," alisema Ame Omar Ali omar.

Alisema ana amini kasi ya kupambana na rushwa na ufisadi ambayo ameonyesha tangu aliposhika madaraka itaelekezwa ndani ya chama ili kuondoa harufu za rushwa na kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa chama.

Mwanachama Suleiman Omar Gazi, alisema kukabidhiwa kofia ya pili Rais wa Zanzibar kutaongeza kasi ya maendeleo kutokana na miradi mikubwa ya ujenzi inayoendelea kujitokeza katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Hata hivyo, alisema kuna urasimu wa kuwaona viongozi wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) na kutoa mfano yeye kukwama kuwaona viongozi licha ya kufika makao makuu.

"Kazi ya kupambana na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma sio kazi ya Rais peke yake, lazima mashirikiano yapatikane kati ya wananchi na watendaji wa mamlaka wenye dhamana," alisema Gazi. Naye Mwanachama Ali Othman alisema uchaguzi ndani ya chama umemalizika ni muhimu wanachama kuondoa makundi ili kuendeleza malengo ya chama ya kuhakikisha ushindi uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Alisema wajumbe wa mkutano mkuu hawakufanya makosa kumchangua Mwenyekiti Rais Samia suluhu Hassan, Makamu Mwenyekiti Abdulrahaman Kinana, Tanzania Bara na Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Dk. Mwinyi kutokana na uwezo katika utendaji.

"Mwanga wa maendeleo tumeanza kushuhudia kwa muda mfupi tangu Rais Dk. Mwinyi kushika wadhifa huo na hatuna wasiwasi kabisa kwa kukabidhiwa kofia ya pili ya uongozi katika chama chetu," alisema Stella Cassian Mbarawa, Mjumbe wa Baraza Kuu (UVCCM), Mkoa wa Kusini Unguja.

Naye Mkurugenzi mstaafu wa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ), Omar Yussuf Chunda, alisema wajumbe wa mkutano mkuu wanapaswa kupongezwa kutokana na timu ya uongozi waliyoichagua.

Naibu Katibu wa UVCCM Zanzibar, Mussa Haji Mussa, alisema wana matumaini makubwa na Dk. Mwinyi kusafisha rushwa au ubadhirifu ndani ya chama kama anavyofanya katika serikali.

Mussa alisema wananchi wa Zanzibar wanaendelea kupata faraja kutokana na kazi nzuri inayofanywa na rais katika kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma baada ya watendaji mbalimbali kufunguliwa mashtaka ya uhujumu uchumi.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar ambaye ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe Mama Mariam Mwinyi, wakisalimiana na viongozi mbalimbali wa chama na serikali alipowasili Viwanja vya Maisara Suleiman Unguja kuhudhuria Tamasha la Usiku wa Dk. Mwinyi la kumpongeza kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa CCM Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mshtakiwa kesi ya mauaji trafiki adai hajui chochote

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Amani Filipo (38) anayetuhumiwa kumuua askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Sajenti Mensah kwa kumpiga risasi, amedai mahakamani kuwa hamtambui marehemu na hajawahi kuwa na ugomvi naye, hivyo anaomba aachiwe huru.

Pia amedai polisi walioandaa kesi hiyo ndiyo wanaojua kuhusu mauaji ya Sajenti Mensah na waliohusishwa na kesi hiyo ni zaidi ya watu watatu.

Filipo alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Romuli Mbuya wakati akitoa utetezi wake katika kesi hiyo ya mauaji anayotuhumiwa kutenda kosa hilo Julai 22, 2016 kwenye taa za Sayansi, Kijitonyama mkoani Dar es Salaam.

Alidai kuwa tarehe hiyo ya tukio, alikwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) baada ya kuombwa na rafiki yake Samwel Thomas amsindikize kwenda kuwaona wagongwa ambao ni wazazi kwenye hospitali hiyo.

Filipo alidai alikubali ombi hilo na kabla ya kufika hospitalini, walipitia watu wengine eneo la Tangi Bovu na alirudi nyumbani kwake majira ya saa nne usiku na kwamba kutokana na kuchoka, aliamua kulala ili kupumzika.

Alidai kuwa baada ya muda kidogo, alipigiwa simu na rafiki yake ambaye ni askari polisi Hamis Yangamba kuwa wakutane baa ya Afrikana, alimkatalia na kumweleza kuwa alikuwa amechoka lakini kutokana na ukaribu wao aliamua kuvaa na kwenda huko baa.

Alidai alipofika alikutana na Yangamba akamnunulia kinywaji na baada ya muda kidogo alimuaga na kumwambia kuwa anatoka kidogo anarudi na alipoondoka tu wakatokea watu asiyowajua wakamweka chini ya ulinzi, wakampeleka Kituo cha Polisi Mabitini, Kijitonyama.

Akiongozwa na Wakili wake, Hassan Kiangio, Filipo alidai Julai 23, 2016 askari walimchukua toka mahabusu wakamweleza kuwa wanakwenda kufanya upekuzi nyumbani kama kuna silaha, lakini hawakukuta chochote.

Alidai kuwa Julai 24, 2016 alichukuliwa kutoka Kituo cha Mabatini na kupelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay ambako alikaa hadi Septemba 20, 2016 ndipo alipelekwa mahakamani na kusomewa tuhuma za mauaji ya Sajenti Mensah.

Pia alidai kuwa hajawahi kuchukuliwa maelezo yoyote na pia hakuwahi kufanyiwa gwaride la utambulisho kama mashahidi wa upande wa mashtaka walivyodai anakumbuka Afande Ndege ndiye aliyekwenda mahabusu na kumhoji kuhusu majina yake na anakoishi tu.

Alidai kuwa hata Sajenti Mensah hamfahamu, labda angeona picha yake kwa sababu Mensah wako wengi na yeye ana marafiki wengi na pia waliohusishwa katika kesi hiyo ni Samwel Thomas, Stewart Marwa, Osward Mwang'unde na Marwa japo waliachiwa.

"Marehemu simtambui na sikuwahi kuwa na ugomvi naye wala mtu yeyote, kwa hiyo kuhusu hizi tuhuma sizitambui, anayezitambua ni askari walioandaa kesi hii. Ninaiomba mahakama iniachie huru," alidai.

Mshtakiwa huyo alimaliza kutoa utetezi wake, leo anaendelea kuulizwa maswali kuhusiana na utetezi wake aliyoutoa kwa sababu Wakili wa Serikali Mwandamizi Yasinta Lyimo alidai watahitaji saa mbili za kumuuliza maswali mshtakiwa.

Filipo anatuhumiwa kumuua Sajenti Mensah kwa kumpiga risasi baada ya kumvamia kwenye kibanda cha polisi cha kupumzikia kilichoko eneo la taa za Sayansi kwa lengo la kutaka kupora.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA AMANI MKOA WA MJINI MAGHARIBI TANZANIA ZANZIBAR PAMOJA NA UDIWANI KATA SABA (7) TANZANIA BARA TAREHE 17 DISEMBA, 2022**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Jimbo la amani Mkoa wa Mjini Magharibi Tanzania Zanzibar pamoja na Udiwani Kata Saba (7) Tanzania Bara kuwa kutakuwa na Uchaguzi Mdogo wa Ubunge na Udiwani siku ya Jumamosi, tarehe 17 Disemba, 2022. Kata zitakazofanya Uchaguzi ni Majohe (Dar es Salaam CC) Dar es Salaam, Mndumbwe (Tandahimba) Mtwara, Njombe Mjini (Njombe TC) Njombe, Dunda (Bagamoyo DC) Pwani, Mwamalili (Shinyanga MC) Shinyanga, Mnyanjani (Tanga CC) Tanga, na Vibaoni (Handeni DC). Tanga.

Upigaji Kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vituo vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) Asubuhi na kufungwa saa kumi kamili (10:00) jioni. Utaratibu utakaofuatwa siku ya Uchaguzi ni kama ifuatavyo:-

1. **SIKU : Wananchi watapiga Kura siku ya Jumamosi tarehe 17 Disemba, 2022**
2. **VITUO : Upigaji kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020**
3. **MUDA : Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni**

**Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi.**
1. Mpiga Kura anatakiwa kutunza kadi yake ya kupigia kura aliyoitumia kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kuhakikisha anakwenda nayo kituoni siku ya uchaguzi.
2. Aidha, kwa Kata saba (7) Tanzania Bara, Wapiga Kura waliopoteza kadi zao za kupigia kura au zilizoharibika, wanaruhusiwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:-
   -Hati ya kusafiria,
   -Leseni ya Udereva na,
   - Kitambulisho cha Uraia ambacho majina yote matatu yafanane na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
3. Kwa Upande wa Jimbo la amani Mkoa wa Mjini Magharibi Tanzania Zanzibar, watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).
4. Mpiga Kura anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni ambapo kutakuwa na mstari wa wanaume na wanawake.
5. Mpiga Kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwa Wapiga Kura wenye mahitaji maalumu kama vile Wazee, Wagonjwa, Watu Wenye Ulemavu, wajawazito na wenye watoto wachanga (watakaokuwa nao kituoni).
6. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama Wapiga Kura bado wapo kwenye mstari, Mlinzi wa Kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wote wanamalizika. Mpiga Kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga Kura.
7. Mpiga Kura anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Kituo.
8. Baada ya kumaliza kupiga kura, Mpiga Kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura.

Kumbuka kuzingatia kanuni za afya kwa kufuata maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa wa Ebola na UVIKO-19 unaosababishwa na virusi vya korona.

**Dkt. Wilson Mahera Charles**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

**Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Eneo la uwekezaji Njedengwa, Kitalu D, Kiwanja Na. 4, Uchaguzi House, S. L. P 358, Dodoma. Barua Pepe:uchaguzi@nec.go.tz, info@nec.go.tz.** Tovuti: **www.nec.go.tz.**

217174402

KUOKOTWA MAITI PORINI...

# Wenyeji waliliona gari, polisi imebaki kimya kwa siku 124

**Na Halfani Chusi aliyekuwa** KILINDI

LEO zinatimu siku 124 tangu kuripotiwa tukio la kuokotwa kwa miili ya watu wawili iliyotupwa ikiwa imefungwa kwenye viroba katika pori la Kitongoji cha Dibabara, Kijiji cha Msamvu, Kata ya Tunguli wilayani Kilindi mkoani Tanga.

Kwa lugha rahisi ya mazungumzo, ni miezi minne na siku nne tangu wenyeji wa maeneo hayo waripoti kuiona miili hiyo Agosti 11, mwaka huu.

Nipashe iliyolazimika kupiga kambi kwa wiki kadhaa baada ya kuripotiwa kwa tukio hilo ikiwa na lengo la kujua undani wake, ilishuhudia eneo hilo kutokuwa na uhakika wa mawasiliano ya simu na hakuna kituo cha polisi maeneo ya karibu na lilikotokeo tukio hilo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Henry Mwaibambe

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni

**WENYEJI WANENA**

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Yohana Ole Nzani, anadai aliona gari kwenye maeneo ilikopatikana miili hiyo lakini hakujua kilichokuwa kinaendelea na alipotaka kutoa taarifa kwa uongozi wa kijiji, alikumbana na kikwazo cha kukosa mawasiliano ya simu.

"Niliiona gari jeupe aina ya Toyota Landcruiser linazunguka zunguka maeneo yale ambayo ilikutwa miili iliyofungwa kwenye kiroba, lakini kwa sababu huku kwetu ni mara chache kuona gari kama lile, nilishtuka.

"Nikataka kumpigia simu Mwenyekiti (wa Kitongoji) kumuuliza kama anafahamu chochote juu ya gari lile lakini kwa bahati mbaya mtandao wa simu ulikuwa umeshakata, sikufanikiwa kuongea naye.

"Baada ya hapo nikaendelea na shughuli zangu, kesho yake (siku iliyofuata) nikaona watu wamejaa, kumbe muda huo lile gari ndilo lilikuwa linatupa hiyo miili! Ningefanikiwa kuongea na mwenyekiti au kama kiituo cha polisi kingekuwa jirani pengine tungeweza kuwakamata," alifafanua.

Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Joseph Nyika, anasema eneo hilo lenye msitu mkubwa, linamilikiwa na aliyemtaja kwa jina la Masai, akilitaja lina sifa ya uingiaji wa watu kiholela na hata kuwa na matukio ya kihalifu kutokana na kuwa karibu na mgodi wa madini

> "Niliiona gari jeupe aina ya Toyota Landcruiser linazunguka zunguka maeneo yale ambayo ilikutwa miili iliyofungwa kwenye kiroba, lakini kwa sababu huku kwetu ni mara chache kuona gari kama lile, nilishtuka.

ulioko kijijini kwao.

"Kijiji chetu cha Dibabara hakina kituo cha polisi kwa miaka mingi, hili linatupa mtihani kwenye kuripoti matukio ya kihalifu.

"Pia kuna huu msitu mkubwa ambao ndani yake mna kiza kinene, unashawishi wahalifu kuja kutupa miili na kufanya matukio mengine ya kihalifu.

"Hapa tulipo network (mtandao) ya simu ni tatizo, ikifika jioni kuanzia majira ya saa 12 inakata mpaka asubuhi. Kwa hiyo, usiku mzima tunakaa bila mawasiliano, lakini tupo karibu na Mlima Lundamilo ambako kunachimbwa madini na huko kuna idadi kubwa ya watu, wengine wanaingia kiholela.

"Kwenye idadi kubwa ya watu kama hiyo huwezi kumjua kwa urahisi mtu mwenye nia njema au mbaya, kuna matukio mengi ya kikatili huwa yanatokea huko, kama vile wao kwa wao kupigana kupokonyana mali," anasema.

Kiongozi huyo anashauri serikali iligawe pori hilo kwa wananchi ili walitumie kwa shughuli zingine kikiwamo kilimo, pia kuwasaka na kuwakamata waliotupa miili hiyo ili kuondoa hofu iliyotanda kijijini baada ya kuokotwa kwa miili hiyo.

Hamza Husein, Mkazi wa Kijiji hicho anashauri serikali kuwatambua wachimbaji wa madini kwenye mgodi ulioko kijijini kwao ili kukabiliana na uhalifu.

"Ukienda huko mgodini utashaanga jinsi watu walivyojazana, makabila tofauti tofauti, tatizo ni kwamba wengine wanafanya shughuli hizo kiholela, hii hali baada ya miaka mitatu mbele kuna hatari ya kuibuka matukio mengi ya uhalifu," anatahadharisha.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Alima Musa alisema tukio la miili ya watu kutupwa kwenye pori hilo limewafanya wakazi wa kijiji hicho kuwa na hofu inayotishia hata usalama wa chakula kwa kuwa baadhi yao wanashindwa hata kwenda shambani.

"Hili tukio limetuumiza, hatujui kwa nini limetokea huku kwetu, tumetawaliwa na hofu japo viongozi wa serikali walituhakikishia usalama, bado tuna shaka sana," anasema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Abdalah Mtapa, anaungana na Mwenyekiti wa Kitongoji Nyika kuiomba serikali kufanya utambuzi wa wachimbaji wa madini walioko kijijini huko ili kuwasajili.

"Kabla ya kugundulika kwamba mlima una madini, hatukuwahi kupata tukio lolote la kutupwa miili wala mauaji ya aina hii.

"Baada ya watu kuanza kumiminika kwenye mlima, kumeanza kuibuka matukio ya aina hii, sisi wenyewe tumeshtushwa na tukio hili, wanakijiji wengine wameanza kuhamia katika vijiji vingine wakihofia usalama wao.

"Ukiachana na miili hii miwili iliyopatikana hapa, pia kuna mwili mwingine uliokotwa kijiji cha mbele na wenyewe ulikuwa umefungwa kwenye mfuko kama iliyokutwa hapa," anabainisha.

Diwani wa Tunguli, Leonard Mahunda, anataja dosari nyingine kiutendaji iliyoko huko, akitamka: "Hatuna watendaji wa vijiji. Kata hii ina vijiji vinne lakini kuna watendaji wawili tu, hivyo wakati mwingine watu wanakosa huduma za msingi."

**KAULI YA POLISI**

Kimsingi, haki ya kuishi ni ya kikatiba, ikielekezwa katika Ibara ya 14 ya Katiba ya Tanzania, Toleo la Mwaka 1977 kwamba "kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria."

Alipotafutwa na Nipashe juzi kuzungumzia tukio hilo la miili iliyookotwa porini wilayani Kilindi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Henry Mwaibambe, alisema hawajawabaini wahusika wake, akisisitiza uchunguzi unaendelea.

Pia alibainisha kuwa mpaka sasa bado hawajajitokeza ndugu wa watu ambao miili yao iliokotwa porini huko, akieleza kuwa miili hiyo si ya wakazi wa eneo hilo.

"Sisi kimbilio letu ni kwa wananchi, ninawaomba waendelee kutoa taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya matukio ya kihalifu kwa sababu hata sisi tunategemea sana taarifa kutoka kwa raia wema ili tudhibiti vitendo hivyo.

"Kwa hiyo nitoe onyo kwa wote wanaofanya vitendo hivyo kwa yeyote atakayebainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwa sababu kufanya hivyo ni ukikwaji wa haki za binadamu na kuvunja sheria za nchi," alisema.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi pia alikiri baadhi ya kata kwenye eneo lake la kazi hazina vituo vya polisi, ikiwamo ya Tunguli ilikotupwa miili hiyo, akibainisha mpango ulioko ni kujenga kituo kikubwa ngazi ya tarafa.

"Kituo hicho kitakuwa na askari wengi kuanzia 20 na kuendelea na tutawapatia usafiri wa kuwawezesha kudhibiti matukio ya kihalifu mapema kuliko kuwa na kituo kila kata halafu kinakuwa na askari wachache, ufanyaji kazi wao utaathirika," alifafanua.

**NINI KIFANYIKE?**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kupitia Ofisa Programu Kitengo cha Ufuatiliaji wa Masuala ya Haki za Binadamu, Victoria Lugendo, kinatoa rai kwa serikali na Jeshi la Polisi kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa huduma ya kituo cha polisi kwenye Kata ya Tunguli.

"LHRC inaamini kuwa polisi ni chombo muhimu katika usimamizi wa amani, utulivu na ulinzi wa raia. Kukosekana kwa kituo cha polisi kwenye eneo ambalo mauaji hayo yalitokea inaweza kuwa sababu mojawapo ya kutokea kwa tukio hilo.

"Tunatoa wito kwa wananchi, hususani wakijiji hicho, kutambua wajibu wao wa kuheshimu haki za wengine ikiwamo haki ya kuishi.

"Haki za binadamu zinalenga zaidi kulinda utu wa mtu, hivyo kitendo cha kumuua binadamu mwenzako na kumtia kwenye gunia na kwenda kumtupa ni kinyume cha utu, haki za binadamu na sheria.

"Kampuni za simu pia ziangalie namna wakazi walioko huko watakavyonufaika na huduma ya mawasiliano kwa saa 24 ili iwe rahisi kwao kuripoti vitendo vya uhalifu," Victoria anawasilisha tamko rasmi la LHRC kuhusu tukio hilo.

HABARI KITAIFA

# Watano mbaroni tuhuma kuiba kichanga

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linawashikilia watu watano kwa tuhuma za wizi wa mtoto mchanga mwenye umri wa mwezi mmoja, aliyeibwa Desemba mosi, mwaka huu.

Mtoto huyo aliibwa nyumbani kwa mama mzazi Joanitha Agustino na watu waliokwenda kumpongeza baada ya kujifungua.

Akithibitisha kupatikana kwa mtoto huyo na kukamatwa kwa watu hao wanaotuhumiwa kuhusika katika wizi huo, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo, William Mwampaghale, alisema watuhumiwa walifika Mtaa wa Migera, Kata ya Nshambya, Manispaa ya Bukoba kutoa pongezi na kufanikiwa kuondoka na kichanga hicho.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo msako ulianza Desemba 2 hadi 8, mwaka huu na kubaini watuhumiwa hao walimchukua mtoto huyo na kwenda naye kwa mganga wa kienyeji katika Kata ya Kamachumu wilayani Muleba afanyiwe dawa ya kumtuliza kulia ili asiwasumbue.

Alisema baada ya hatua hiyo watuhumiwa hao walitawanyika kwenda maeneo mbalimbali ndani ya Mkoa wa Kagera ili wasikamatwe.

"Baada ya kutoka kwa mganga mtuhumiwa aliyechukua mtoto alipanda basi na kuelekea mkoani Dar es Salaam na wengine walitawanyika na kujificha maeneo mbalimbali ndani ya mkoa huo wakihofia kukamatwa," alisema Mwampaghale.

Alisema mtuhumiwa wa wizi wa mtoto huyo baada ya kugundua anafuatiliwa aliondoka kwenda Dar es Salaam kwa lengo la kumlea.

Alisema alipogundua anafuatiliwa na polisi aliondoka na kwenda Dodoma mjini kujificha, lakini Desemba 8, mwaka huu, alikamatwa.

Mwampaghale alisema baada ya kupatikana kwa mtoto huyo alipelekwa hospitalini ili kufanyiwa uchunguzi na daktari alithibitisha kuwa hali yake ipo vizuri na kukabidhiwa kwa wazazi wake.

# TBS yakamilisha kampeni elimu kwa umma Singida

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limemaliza kampeni yake ya kutoa elimu kwa umma katika wilaya za Iramba, Mkalama, Ikungi na Halmashauri ya Wilaya ya Singida mkoani Singida kuhusiana na umuhimu wa kusoma taarifa zilizoko katika bidhaa na kununua bidhaa zilizothibitishwa na shirika hilo.

Kampeni hiyo pia imeenda sambamba na kuwahamasisha wajasiriamali wadogo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao na wafanyabiashara kutakiwa kusajili maduka ya chakula na vipodozi, ikiwafikia wananchi 6,800.

Kampeni hiyo iliyoanza Novemba 28, mwaka huu, ilihitimishwa jana, ikifanyika katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu wengi ikiwamo sokoni, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, aliipongeza TBS kwa kutoa elimu kwa wananchi na alishauri kufanya ukaguzi wa kushtukiza mara kwa mara madukani hususani bidhaa za ujenzi kama nondo na mabati.

Mkaguzi wa TBS, Magesa Mwizarubi, aliwakumbusha wananchi kutambua kuwa vita ya bidhaa hafifu siyo ya shirika hilo pekee yake, bali ni ya taifa zima.

Magesa alisema wananchi wanapaswa kutambua umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku, pia kuwafahamisha fursa ya huduma ya kuthibitisha ubora wa bidhaa bure zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo.

Hata hivyo, aliwataka wawe mabalozi kwa kuhamasisha umuhimu wa matumizi ya bidhaa zenye ubora katika jamii wanazoishi.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa pindi wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote kwenye soko.

"Kwa wafanyabiashara ni muhimu kufuatilia taratibu sahihi za usajili wa bidhaa au majengo ya chakula na vipodozi kwa kutembelea ofisi ya TBS iliyoko karibu au kupiga katika kituo cha huduma kupitia mawasiliano yaliyotolewa," alisema.

Kupitia kampeni hiyo shirika limeweza kuwafikia wananchi 6,839. Kati yao, wajasiriamali wanawake ni 89.

Alifafanua kwamba kampeni hiyo ni endelevu na inatarajiwa kupelekwa kwenye wilaya za Mkoa wa Mbeya.


DERM group

OFFICE CLOSURE NOTICE

DERM group wishes to inform it's esteemed clients and business partners that our corporate offices at Derm Plaza 14th & 15th Floor New Bagamoyo Road, Makumbusho; will be closed during the festive season with effect from Saturday, 17th December 2022.

**Business will resume on 9th January 2023 in our New Offices at Skycity Mall 8th floor, University Road Dar es salaam.**

This closure will not affect our site operations in Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Geita, Mtwara, Pemba, Rukwa, Ruvuma, Songwe, Tanga, and Zanzibar.

We thank you all for the business support in the year 2022.
Our warmest wishes for a wonderful festive season filled with Love joy and happiness.

217192002




DERM group | Derm Elevators | info@derm.co.tz | dermgrouptz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pongezi wadau elimu kujadili ukatili kijinsia

**HALI** ya ukatili wa kijinsia hasa kwa watoto wa shule, inaendelea kushamiri nchini na kuwaibua wadau wa elimu ambao wameandaa kongamano kubwa la walimu wa shule za msingi na sekondari za serikali na binafsi kuzungumzia ukatili kwa watoto.

Wadau hao wameona umuhimu na wajibu wa kutafuta ufumbuzi na kushughulikia sababu za unyanyasaji huo shuleni na nyumbani ili kuhakikisha watoto wanalelewa kwenye mazingira salama.

Kadhalika walimu wana nafasi kubwa ya kukomesha vitendo vya kikatili dhidi ya watoto shuleni ikiwa watashirikishwa kwa kupewa taarifa sahihi na mbinu za kutumia ili kuwajengea watoto uwezo wa kutambua ukatili na kutoa taarifa utakapojitokeza.

Pamoja na kuwekwa kwa madawati ya jinsia katika maeneo muhimu ili wananchi waweze kutoa taarifa vitendo vya ukatili vinapojitokeza, lakini kuna baadhi ya watu wanakosa uelewa au elimu ya kuripoti matukio hayo.

Katika baadhi ya mitandao ya kijamii, kuna video fupi inayomwonesha askari polisi akiwafundisha watoto jinsi ya kujiepusha na watu wanaowafanyia ukatili wa kijinsia.

Askari huyo anawaonesha watoto namna ya kukataa iwapo watu watawashika maeneo nyeti na kuwaripoti mara moja.

Kwa kweli hatua ya askari huyo kujitoa kuwafundisha wanafunzi ni ya kuungwa mkono na watu wengi zaidi ili watoto wasiendelee kukumbwa na vitendo hivyo ambavyo huwaharibia ndoto zao za kufika mbali kielimu.

Kuna matukio ambayo hufanyika katika jamii, lakini anayefanya kitendo hicho au watu wanaomzunguka kushindwa kuelewa kama huo ni ukatili.

Ndiyo maana kunahitajika elimu ili watu waweze kuelewa matukio hayo yanapofanyika waweze kuyakemea.

Matukio ya ukatili wa kijinsia mengi yanafanywa na ndugu wa karibu.

Kumekuwa na mtukio kadhaa pia ya watoto wa shule kufanyiwa ukatili wa kingono wanapokuwa wanakwenda shule na kurudi nyumbani kwa kutumia usafiri wa mabasi ya shule.

Watu wanaowafanyia ukatili huo wanaaminiwa na wazazi na walimu.

Inakisikitisha na kuumiza pale mzazi anapokuja kugundua mtoto akiwa ameshaharibika na wengine kupata ulemavu wa maisha.

Katika baadhi ya nyumba vitendo hivyo hutokea na pengine majirani wanashuhudia, lakini wanashindwa kuwajulisha wazazi kwa kutokuwa na ushirikiano au ukaribu.

Baadhi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ni vipigo, ukeketaji kwa watoto, unyanyasaji wa aina yoyote ikiwamo wasaidizi wa ndani kupewa kazi kubwa kuliko uwezo wao na kunyimwa chakula.

Mtu yeyote anapoona vinafanyika katika eneo lake analoishi au kwa jirani yake anapaswa kutoa taarifa, ili kunusuru mhusika asiendelee kupata mateso zaidi.

Katika kipindi cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, elimu na shuhuda mbalimbali zimekuwa zikitolewa ili kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anasema mitandao ya kijamii ina mchango mkubwa katika kupunguza ukatili wa kijinsia ikiwamo kufichua unyanyasaji wanaofanyiwa watu majumbani.

Vilevile, mitandao ya kijamii inasaidia taasisi, wanaharakati na serikali kupata takwimu ya uwapo wa matendo hayo ikiwamo aina za unyanyasaji wa kijinsia inayofanyika na mikoa ambayo matendo hayo yanafanyika sana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

# Watoro hawa wasakwe kurejeshwa darasani

**WANAFUNZI** 963 wa sekondari mkoani Njombe, wanadaiwa kutofanya mtihani wa kidato cha pili kutokana na sababu mbalimbali, utoro ukitajwa.

Katika idadi hiyo wavulana ni 584 wakati wasichana ni 379, ambao wote kwa ujumla wao ni sawa na asilimia sita ya walioandikishwa kufanya mtihani huo mwaka huu.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Ofisa Elimu wa mkoa huo, Nelas Mulungu, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichokutanisha wadau mbalimbali wa elimu.

Inasikitisha kusikia idadi hiyo ya wanafunzi kutofanya mtihani, kwa sababu ya utoro, licha ya serikali kutoa maelekezo kwamba, wanafunzi wote waliosimama kutokana na sababu mbalimbali warudi shuleni.

Kuendelea kuwapo kwa utoro huo ni sawa na kukwamisha juhudi za kutaka kila mtoto apate elimu, hivyo ingekuwa ni vyema jamii ikichukua hatua kukabiliana na mtindo huo.

Katika karne hii ya 21 elimu haipaswi kuwekwa pembeni hasa kwa kuzingatia kwamba kila jambo linahitaji kujua kusoma, kuandika kuhesabu na ujasiriamali, hivyo ni vyema wadau wa elimu wakiwamo wazazi, walimu, viongozi na walezi kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.

Njia hiyo inaweza kusaidia kupunguza kama si kumaliza utoro shuleni ambao umeendelea kuwapo licha ya serikali kumfanya kila jitihada za kuhakikisha kila mtoto anapata elimu kuanzia ya awali na kuendelea.

Ninaamini kwamba, Tanzania bila utoro shuleni inawezekana, iwapo kila mmoja atafanya sehemu yake kuhakikisha wanafunzi wanahudhuria vipindi vyote vya masomo, badala ya kudhani ni jukumu la kundi fulani.

Katika kuonyesha umuhimu wa elimu kumekuwapo kaulimbiu mbalimbali nchini, zinazotumika kueleza umuhimu huo, miongoni mwake ikiwa ni 'elimu ni ukombozi, ni kazi', msingi wa maendeleo na elimu ni ufunguo wa maisha.

Kaulimbiu hizo zinalenga kutaka kuonyesha ni kwa kiasi gani elimu ni muhimu katika nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu, lakini inasikitisha kusikia kuwa bado kuna watu hawaoni umuhimu wa kusoma, wala kuwapeleka watoto wao madarasani licha ya serikali kugharamia masomo.

Ikumbukwe, miaka ya mwanzo ya uhuru wa Tanganyika ambao sasa umetimiza miaka 61, ujinga uliorodheshwa na waasisi wa taifa letu kama miongoni wa maadui wa maendeleo.

Hatua hiyo ilitokana na kwamba, ikiwa jamii ingeondokana na ujinga ingekuwa imepiga hatua mojawapo ya maendeleo, na kwa kutambua hilo, serikali ilitumia mbinu mbalimbali, kuhakikisha kila mtoto anapata elimu.

Ilikuja na mpango wa elimu kwa wote, ukilenga kuwapatia watoto wote wenye umri wa kuanza shule kuwa madarasani.

Mambo mengine mengi yalifanyika na hadi sasa inaendelea kufanyika, lengo likiwa ni kutaka kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu tena katika mazingira ya karibu.

Mazingira hayo ya karibu yanachagizwa na kuwapo kwa shule za sekondari za kata ambazo zimeenea kote nchini, ingawa sasa inaonekana bado wapo baadhi ya wanafunzi ambao hawaoni umuhimu wa elimu.

Kuendelea kuwapo kwa utoro shuleni, kunaweza kuathiri lengo namba nne la Maendeleo Endelevu (SDGs) ambalo linaelekeza kuwapo elimu bora yenye usawa inayotoa fursa kwa wote kujiendeleza.

Kama wanajamii, mashirika ya umma na binafsi, tuna nafasi ya kuhamasisha elimu bora yenye usawa katika mikakati ya maendeleo ya kiuchumi na kuhakikisha mafunzo yanaleta tija katika soko la ajira.

Lakini utoro shuleni unaweza kuwa ni moja ya tishio la kutotimiza lengo hilo iwapo jukumu la kuhamasisha elimu litabaki kwa serikali na wadau wachache, ni vyema jamii nzima ikavalia njuga utoro huo na kuukomesha.

Ni muhimu kutafuta chanzo cha utoro huo na kama kitakuwa ni kukosekana chakula shuleni, basi wadau wa elimu, wazazi na walezi, wahakikishe watoto wanapata chakula cha mchana shuleni ili kupunguza utoro huo.

Viongozi wa Kamati ya Maendeleo ya Kata nao wafanye juu chini ili chakula kwa wanafunzi shuleni, kiwe ajenda ya kudumu katika mikutano yao, kwani ukosefu wa chakula umekuwa ukidaiwa kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia utoro kwa baadhi ya wanafunzi.

## Magari 1,400 yaunganishiwa mfumo wa gesi asilia Dar

**Na Pilly Kigome**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limesema jumla ya magari 1,400 yameunganishwa kwenye mfumo wa nishati ya gesi asilia.

Vilevile, nyumba 1,500, viwanda 48, hoteli moja na taasisi nne zimeshaunganishwa na mfumo huo kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano, Marie Msellemu, wakati wa maonyesho ya saba ya viwanda yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa tangu kufungwa kwa mfumo wa gesi asilia Julai 2004 hadi Desemba 2021, zaidi ya Sh. trilioni 60 zimeokolewa.

Alisema lengo ni kuleta unafuu wa gharama ya maisha kwa Watanzania kwa kuwa nishati hiyo inapatikana kwa uhakika na bei nafuu.

Msellemu alisema gesi asilia ina mchango katika kuinua uchumi kwa kuwa ina gharama nafuu, hivyo wananchi kutopeteza fedha nyingi katika matumizi ya lazima ya kila siku kulinganisha na matumizi ya umeme na mafuta.

Alisema gesi asilia ni mkombozi na inaendana na kasi ya serikali katika kuwaangalia wananchi wanyonge, ili wafurahie maisha kidigitali yanayokwenda na wakati.

Alibainisha tayari yapo maeneo ambayo yameshaunganishwa na gesi asilia ambayo ni pamoja na Mkuranga, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Sinza na Mikocheni huku wakiendelea kuunganisha maeneo mengine.

Pia mifumo ya gesi ya kushindilia (CNG) imeshajenga kwenye vituo vya mafuta viwili vinavyotoa huduma ya gesi asilia.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jim Yonaz, aliwapongeza TPDC kwa kuzalisha gesi asilia na kuleta unafuu wa maisha kwa Watanzania, akiamini utaleta mabadiliko makubwa kiuchumi.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa hiyo kwa kuunganisha mifumo ya gesi asilia nyumbani, viwandani na kwenye magari ili kupata unafuu wa maisha.




Mchuuzi akiwauzia wateja wake madafu barabarani eneo la Manzese Bakhresa Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Yetu Microfinance yawekwa chini ya uangalizi maalumu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeiweka chini ya usimamizi wake taasisi ya fedha ya Yetu Microfinance Bank Plc kuanzia jana kutokana na upungufu mkubwa wa ukwasi na mtaji.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na BoT, ukwasi na mtaji uliopo ni kinyume cha matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006 na kanuni zake.

"Upungufu huu wa ukwasi na mtaji unahatarisha usalama wa sekta ya fedha, pia Yetu Microfinance Bank Plc kuendelea kutoa huduma za kibenki, kutahatarisha usalama wa amana za wateja wake.

"Kutokana na uamuzi huo, BoT imeisimamisha Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi wa Yetu Microfinance Bank Plc kuanzia leo (jana)," BoT ilibainisha kupitia taarifa yake hiyo.


Benki Kuu pia imemteua Meneja Msimamizi atakayekuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Yetu Microfinance Bank Plc kwa kipindi itakavyokuwa chini ya usimamizi wa BoT.

"Umma unaarifiwa kuwa katika kipindi kisichozidi siku 90 kuanzia siku ya taarifa hii, shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za Yetu Microfinance Bank Plc zitasimama ili kuipa nafasi BoT kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa suala hili," BoT ilibainisha.

BoT pia iliuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika benki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya fedha.

Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, imeipa BoT mamlaka ya kusimamia shughuli zote za kibenki na taasisi za fedha nchini kwa lengo la kuhakikisha uimara na ustahimilivu wa sekta ya benki na ya fedha kwa ujumla.

**KABWELA** Fadhili Mohamed



# Halmashauri yatoa mil. 240/- kuwezesha makundi maalum

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

HALMASHAURI ya Manispaa Mtwara-Mikindani mkoani Mtwara imetoa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 244.8 kwa vikundi 35 vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuviwezesha kujikwamua kiuchumi.

Akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 244.8 mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, alisema fedha hizo zinapaswa kutumika kama ilivyokusudiwa kwa vikundi hivyo kuendeleza biashara zao wanazofanya.

Alisema halmashauri inatekeleza utoaji wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya halmashauri kwa vikundi vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kukuza uchumi wa makundi hayo.

Kyobya alisema fedha hizo ni mapato ya ndani ya halmashauri hiyo ambapo katika mapato hayo sheria inaitaka halmashauri kutoa mikopo hiyo kila mwaka.

Alisema wanavikundi wanapaswa kutangaza biashara zao kwenye mitandao ya kijamii ili zifahamike zaidi na watu waweze kufikia kwani njia za kisasa.

"Mikopo hii kama mkiitumia vyema, basi kila mmoja wenu atakuwa mfanyabiashara mkubwa, hivyo tumieni fursa ya mitandao ya kijamii kutangaza biashara zenu ili ziweze kufahamika zaidi," aliagiza Kyobya.

Alisema mikopo hiyo haina riba, hivyo wanaofanikiwa kupata ni lazima watambue kurejesha fedha hizo kwa wakati ni muhimu ili na wengine wakopeshwe ili vikundi vingi zaidi wanufaike na mikopo hiyo.

Mwajuma Kaporo, mjasiriamali ambaye ni mnufaika wa mkopo huo, aliishukuru serikali kwa kuwapatia mkopo huo, akiahidi watarejesha fedha hizo kwa wakati.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani, Emmanuel Mwaigobeko, alisema halmashauri hiyo itaendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo kuyawezesha makundi hayo kuinuka kiuchumi.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Riziki Pembe Juma (kulia), akisalimiana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Uganda, Robinah Nabbanja (katikati), kwenye sherehe ya ufunguzi wa maonesho ya 22 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Wajasiriamali Wadogo na Wakati maarufu Juakali, jijini Kampala, Uganda. **PICHA: MAMBO YA NJE**

## Madiwani wapewa mafunzo matumizi matokeo ya sensa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amefungua mafunzo kwa madiwani na watendaji wa kata na mitaa ya Jiji la Dodoma kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa ajili ya mipango jumuishi na maendeleo endelevu ya jiji hilo.

Akifungua mafunzo hayo kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini hapa juzi, Senyamule alisema katika kutatua kero ya upatikanaji wa takwimu na kupunguza gharama za kufanya sensa tatu tofauti, serikali iliamua kufanya sensa zote tatu kwa pamoja chini ya uongozi mahiri wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ilifanyika kwa pamoja na mazoezi mengine makuu mawili; Sensa ya Majengo na Sensa ya Anwani za Makazi.

"Kwa kipindi kirefu nchi yetu ilikuwa haina takwimu za majengo za kutosha na za uhakika ambazo zimeunganishwa na takwimu za watu, hali zao za makazi na anwani za makazi kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo ya sekta ya nyumba," alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema matokeo ya sensa yanakwenda kubadilisha sura na mwenendo wa utungaji sera, upangaji wa mipango, tathmini ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kuimarisha ustawi wa wananchi na kuwahimiza madiwani na watendaji wa kata na mitaa kutumia mafunzo hayo kama nyenzo muhimu ya kutafsiri kwa vitendo matokeo ya sensa katika maeneo yao.

"Kwetu sisi hapa Dodoma tuna kazi kubwa sana ya kuendelea na kazi ya kuupanga huu mji ipasavyo. Matokeo yameonyesha kuwa idadi ya watu imeendelea kuongezeka kutoka watu milioni 2.1 mwaka 2012 hadi watu milioni 3.1 mwaka 2022 sawa na kasi ya ongezeko la asilimia 3.9 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita," alisisitiza Senyamule.

Aliwaagiza wadiwani na watendaji wa kata na mitaa ya Jiji la Dodoma kukaa na wakurugenzi wa halmashauri zao na kufanyia kazi kwa kina matokeo ya sensa tatu na kusisitiza kupata mrejesho wa haraka kujua yatakayobainika kuhusu huduma za jamii zilizoko, majengo na anwani za makazi.

"Nitumie nafasi hii kuwaagiza wakuu wote wa wilaya mliopo kuwa serikali imetumia rasilimali fedha za kukusanya taarifa hizi na sisi tumebahatika kupata mafunzo haya kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

"Hivyo, ninapenda kuwaelekeza mnipatie mrejesho wa wapi tunatakiwa kuboresha zaidi na hususan katika sekta za jamii kama vile shule za msingi na sekondari," aliagiza.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema wameanza mafunzo hayo kwa watendaji wa Mkoa wa Dodoma kwa kuwa yataainisha viashiria vya kiuchumi, kimaendeleo na kijamii kwa ajili ya mipango jumuishi.

Kamisaa wa Sensa na Spika mstaafu, Anne Makinda, alisema Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imelenga kuhakikisha takwimu si za kupita bali ziishi kwa miaka 10.

Mkoa wa Dodoma umekuwa wa kwanza kupatiwa mafunzo na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yanayoongozwa na kaulimbiu 'Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa Mipango Jumuishi na Maendeleo Endelevu'.

Serikali imeandaa Mwongozo Maalum wa Kitaifa wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa lengo la kuongeza uelewa, uwazi na kupanua wigo wa matumizi ya matokeo hayo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuweka mipango jumuishi kwa maendeleo endelevu ya kijamii, kiuchumi na mazingira.

## Apendekeza utaratibu mabasi ya shule kushusha wanafunzi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAMILIKI wa shule wanaosafirisha watoto kwa kutumia mabasi wamesisitizwa kusimamia utaratibu wa kuwashusha wanafunzi wanapofika majumbani mwao kuwaepusha na ukatili wa kijinsia.

Mkurugenzi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Multi Dome Relief Centre, Fauzi Albaggar, alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari kuwa wanafunzi hubakwa au kulawitiwa kwenye magari wanaporudishwa nyumbani na historia inajionesha hufanyiwa hivyo anapobaki mtoto anayeshuka kituo cha mwisho.

"Tatizo kubwa mtoto akibaki peke yake kwenye gari wakati wa kurudishwa nyumbani, inapaswa watoto wanaoshukia kituo kimoja kuanzia watatu na kuendelea wabaki kuwa wa mwisho kushuka na anayeshuka peke yake kituoni awahishwe kushuka ili kuwalinda watoto wetu," alisema.

Albaggar alisema kuwashusha watoto wakiwa zaidi ya wawili au watatu kutasaidia kupunguza au kuondoa kabisa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa sababu wanaweza kupiga kelele za kuomba msaada au mmoja anaweza akawa na ujasiri wa kusema linapotokea lolote tofauti akiwa mmoja.

Hata hivyo, aliwasisitiza wazazi kuwaogesha watoto wao hata mara chache wanapopata nafasi na kuwakagua ili kubaini kama wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia waweze kuwasaidia.

Alisema kituo hicho cha Multi Dome kinachofadhiliwa na familia ya Albaggar kina jumla ya watoto 32 huku zaidi ya 20 wakiwa wanasoma katika shule mbalimbali za msingi na sekondari aliowajengea utaratibu wa kuwazuia kukumbwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Alifafanua utaratibu huo ni pamoja na kuwalaza kila mtu na kitanda chake, milango yao kutowekwa funguo wala vitasa vya kufunga kwa ndani ili kuepusha vishawishi, kuwapeleka na magari yao binafsi shule huku wakiwa na walezi wao.

Albaggar alisema watoto wanapaswa kulelewa katika maadili mazuri kutoka kwa mzazi au mlezi aliyeamua kuwalea ili kuwafanya wawe na upendo na kuzungumza waliyofanyiwa.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka kwenye kituo hicho, Salvatory Augustino, alisema kituo hicho kina utaratibu wa kutoa elimu kwa watoto na jamii inayoishi humo kila mara ili kuwaepusha na masuala ya ukatili wa kijinsia.

Augustino alisema utoaji wa elimu ya kijamii kwa mtiririko mbalimbali unasaidia jamii inayowazunguka kujitambua na kujenga tabia ya kuishi kama ndugu.

Desemba 10 kila mwaka ni siku ya kuadhimisha sherehe za uwekwaji wa mkataba wa haki za binadamu pamoja na kilele cha kampeni za siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na udhalilishaji wa binadamu.

HABARI KITAIFA

## Watoto 96 wafanyiwa udhalilishaji Ludewa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JUMLA ya watoto 96 wenye umri wa chini ya miaka mitano wameripotiwa kufanyiwa vitendo vya ubakaji kwa kipindi cha mwaka 2022 wilayani Ludewa, Mkoa wa Njombe.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, alitoa takwimu hizo katika maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru na kuwataka wazazi na walezi kushirikiana kufichua vitendo vya ukatili.

"Nawaomba wazazi tushirikiane kufichua vitendo vya ukatili kwa watoto, pia viongozi mbalimbali wa dini tengeni siku maalumu ya maombezi kupinga ukatili, ubakaji, mauaji ili kutokomeza matendo mabaya katika wilaya yetu," alisema Trese.

Alisema pamoja na kuadhimisha Miaka 61 ya Uhuru, jamii inatakiwa kupinga adui rushwa kwa sababu amekuwa akirudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Matham Chalamila, alisema katika kuadhimisha Miaka 61 ya Uhuru, Wilaya ya Ludewa imepiga hatua kubwa kimaendeleo kwa sababu ya uwapo wa barabara bora, uchimbaji wa makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma pamoja na fursa mbalimbali za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Diwani wa Kata ya Ludewa, Monica Mchilo, alisema kwa kipindi cha Miaka 61 ya Uhuru serikali imeboresha maendeleo mbalimbali hasa katika sekta ya afya kutokana na kinamama kujifungulia nyumbani.

Isabela Mgimba mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Chifu Kidulile, wilayani Ludewa alisema kwa miaka 61 ya Uhuru serikali imesaidia ujenzi wa madarasa na madawati bora.

Silivesta Haule mkazi wa kijiji cha Luilo, alisema kumekua na mapinduzi makubwa baada ya Uhuru kwa uwapo wa miundombinu bora ya barabara kwa sababu hapo zamani walikuwa wanatembea umbali mrefu kufuata mahitaji.

# Kongamano kujadili ukatili kwa wanafunzi

**Na Mary Geofrey**

WADAU wa elimu nchini wameandaa kongamano kubwa la walimu wa shule za msingi na sekondari za serikali na binafsi kuzungumzia ukatili kwa watoto.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Kairuki, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo litakalofanyika Desemba 15, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwasisi na Mkurugenzi wa Shule za Rightway, Mercy Mchechu, kwa niaba ya wamiliki wengine wa shule, alisema lengo ni kushirikishana mbinu mbalimbali za kuwalinda watoto dhidi ya ukatili hasa wakiwa maeneo ya shuleni.

"Sisi sote kwa pamoja tuna wajibu wa kutafuta ufumbuzi na kushughulikia sababu za unyanyasaji huu shuleni na nyumbani ili kuhakikisha watoto wanalelewa kwenye mazingira salama," alisema Mercy na kuongeza kuwa;

"Walimu wana nafasi kubwa ya kukomesha vitendo vya kikatili dhidi ya watoto shuleni ikiwa watashirikishwa kwa kupewa taarifa sahihi na mbinu za kutumia ili kuwajengea uwezo wa kutambua ukatili na kuutolea taarifa utakapojitokeza na hili ndio lengo kuu la kongamano hili."

Mdau wa shule za Rightway na Meneja wa Mine Foundation, Joab Ndanzi, alisema kuwa mada na mijadala katika kongamano hilo itaendeshwa na wataalamu kutoka polisi dawati la jinsia, ustawi wa jamii, Shirika la HakiElimu na wadau wengine.

Kongamano hili la siku moja litawakutanisha walimu zaidi ya 500 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Utafiti uliofanywa na Shirika la HakiElimu mwaka 2020, ulibaini uwapo mkubwa wa matukio ya unyanyasaji wa watoto katika mifumo tofauti.

Takribani asilimia 87.9 ya watoto wote waliosailiwa, wamewahi kukumbana na ukatili wa kimwili, hususani kupitia adhabu za viboko, asilimia 17.0 ya watoto walio shule za umma na asilimia 14.3 walio shule binafsi wamewahi kunyanyaswa kingono angalau mara moja, wakati asilimia 34.3 ya watoto wa shule kwa ujumla wamenyanyaswa kisaikolojia hasa na wazazi au walezi.



Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi kutoka ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Polisi Kinondoni Kitengo cha Ushirikishwaji Jamii (dawati la jinsia na watoto), Christopher Newton, akitoa elimu ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Twiga, Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofikia kilele chake mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EPZA yahamasisha wawekezaji wa ndani kutumia fursa

**Na Mwandishi Wetu**

WAWEKEZAJI wa ndani wametakiwa kutumia fursa zinazotolewa na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya uwekezaji kwa mauzo ya nje (EPZA) kupitia maeneo maalum ya kiuchumi ili kukuza biashara zao na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Ofisa Mkuu Uhamasishaji na Uwezeshaji wa EPZA, Nakadongo Fares, alisema hayo wakati wa maonesho ya saba ya bidhaa za viwanda yaliyofanyika viwanja vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

"Wawekezaji wa ndani wana fursa kubwa sana ya kupata mafanikio makubwa endapo watawekeza kupitia maeneo maalum ya kiuchumi ya EPZ na SEZ," alisema.

Aliwahimiza kuchangamkia fursa hiyo ya kuwekeza kupitia maeneo hayo maalum ikizingatiwa kuwa serikali inafanya juhudi kubwa kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Alisema kuwekeza katika maeneo maalumu ya kiuchumi kuna manufaa makubwa kama miundombinu ambayo ipo tayari na kusaidia kuzalisha bidhaa zenye ubora na kwa gharama nafuu.

Alisema serikali kupitia EPZA imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa wazawa na wa nje kupitia maeneo maalum ya kiuchumi na hasa ikilenga sekta za kilimo na viwanda.

Alisema Tanzania imejaliwa kuwa na malighafi nyingi na za aina mbalimbali, hiyo ikiwa ni fursa muhimu kwa wawekezaji katika kukuza biashara zao na kuzalisha ajira nyingi zaidi.

Aidha, alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na wanyama wengi na kutoa fursa kubwa kwa wawekezaji kwenye bidhaa za ngozi kuzalisha kwa ajili ya soko la ndani na nje.

Kwenye sekta ya pamba, alisema kuna fursa kubwa kwa wawekezaji kuitumia kuzalisha, kujenga viwanda vya nguo kwa ajili ya kuuza kwenye soko la ndani na la nje.

Alisema mamlaka hutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji kupitia SEZ ikiwa ni vya kifedha na visivyo vya kifedha kama misamaha ya kikodi, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ushuru mbalimbali katika serikali za mitaa.

Wawekezaji katika maeneo maalum ya SEZ wanaruhusiwa kuuza nje ya nchi hadi asilimia 80 ya bidhaa wanazozalisha na asilimia 20 ndio zinauzwa katika soko la ndani.

Pia, EPZA huwasaidia wawekezaji kupata ardhi na kuwaunganisha wakulima na masoko ya mbalimbali ya kimataifa duniani na kuongeza upana wa masoko yao.

# Madiwani waomba mbolea ruzuku kupelekwa kila kata

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, wameomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kupeleka mbolea ya ruzuku makao makuu ya kila kata ili wakulima waweze kuondokana na adha ya kuifuata Songea Mjini kwa gharama kubwa.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Diwani wa Kata ya Mkongo Nakawale, Danieli Nyambo, wakati alipokuwa akichangia ajenda ya mbolea kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichohudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Francis Ningu.

Nyambo alisema wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kwa muda mrefu wanalalamika adha wanayoipata ya kutoka kwenye vijiji vyao kwenda Songea kununua mbolea.

Alifafanua kuwa tangu msimu wa kilimo ulipoanza mbolea inapatikana kwa shida kutokana na wakulima kuifuata Songea na kulazimika kulala kati ya siku moja hadi tano kuisubiri na baadhi ya wakulima wakiibiwa fedha kabla ya kuipata.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Juma Pandu, alisema hali ya upatikanaji mbolea si nzuri kwa kuwa ya ruzuku inapatikana Songea Mjini ambako wakulima wengi wanashindwa kwenda kuinunua.

Pandu alisema mahitaji ya mbolea kwa Wilaya ya Namtumbo ni tani 19,000, lakini mpaka sasa iliyopokewa wilayani Namtumbo ni tani 700 pekee. Akifungua kikao cha Baraza la Madiwani Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Francis Ningu, alisema kilio cha wakulima kuhusu tatizo la upatikanaji wa mbolea za ruzuku ofisi yake ilishapokea na tayari jitihada zimeanza kuchukuliwa za kuhakikisha wakulima wanapata.

Dk. Ningu alisema kuwa ofisi yake ilisha pata taarifa kuwapo baadhi ya wafanyabiashara wanaokwenda kuuza mbolea vijijini kwa bei kubwa tofauti na elekezi na kuwaonya waache tabia hiyo huku ufuatiliaji ukifanywa kuwabaini wanaokwenda kuwalangua wakulima kwa kuwauzia kati ya Sh. 100,000 mpaka 120,000.

Akijibu ombi lililotolewa na madiwani la gharama ya kusafirisha mbolea kutoka Songea Mjini hadi makao makuu ya kila kata ibebwe na wakulima wenyewe ili iwe rahisi kupata mbolea ya ruzuku, alisema ombi amelipokea na litafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili wakulima waipate kwa wakati.




Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, akipokea vitabu vya miongozo ya maadili kutoka kwa Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Baraka Makona, wakati wa ufungaji wa kikao cha Jukwaa la Malezi Mbadala mjini Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo kusaidiwa utafiti madini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

KAIMU Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini Kahama, Eva Kahwili, amesema taasisi za serikali zinazojishughulisha na masuala ya madini zinaweza kuwa msaada kwa wachimbaji wadogo kufanya utafiti.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni GST na Shirika la Taifa la Madini (STAMICO).

Alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari waliofika ofisini kwake kujua ofisi yao inavyowasaidia wachimbaji wadogo kufanya utafiti wa kubaini miamba yenye madini ya dhahabu ili kuondokana na uchimbaji holela unaoathiri mazingira.

"Taasisi hizi zitawasaidia kufanya utafiti kwenye maeneo yao na itawasaidia kuondoa hasara wanazokutana nazo za kushindwa kujua miamba ina mwelekeo gani na kushindwa kupata data ambazo zinaweza kuwasaidia kupata mikopo kwenye taasisi za kibenki," alisema Eva.

Pia aliwahamasisha wachimbaji wadogo kujiunga kwenye vyama vya wachimbaji ili kurahisisha kupata mikopo kwa kuwa wakiwa na data sahihi wanaweza kukopesheka na kufanya shughuli za uchimbaji bila kuwa na shaka.

Ofisa Madini Wilaya ya Kahama, Sebastian Masau, alisema kuwa Tume ya Madini itatatua changamoto wanazokutana nazo wachimbaji wadogo kwa sababu serikali imejipanga kuwa na tawi la GST mkoani Geita, pia huduma nyingine ya kimaabara itafunguliwa muda wowote.

Alisema kutokana na uwapo wa huduma hizo majibu ya wachimbaji wadogo yanakwenda kupatikana haraka na ni sehemu ambazo ni karibu na shughuli zao na kutoa wito wachimbaji hao waendelee kutumia ofisi za madini na katika vyama vya wachimbaji wanaojiunga wawe wanafika ofisi za madini kama walezi wao ili kupata elimu zaidi.

# NGO zatakiwa kushirikisha wenye ulemavu

**Na Frank Monyo**

TAASISI zisizo za kiserikali zimetakiwa kuzingatia ushiriki wa watu wenye ulemavu ili wajitokeze kwenye uchaguzi na kutumia haki ya kuchagua viongozi bora wanaoamini watawaletea maendeleo.

Msajili wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali Zanzibar, Ahmed Abdullah, alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya miaka mitano ya Mtandao wa Ushiriki Tanzania wenye mashirika wanachama 22.

Mtandao huo lengo lake ni kuwasemea vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika mambo mbalimbali ya kijamii.

"Bado kuna umuhimu wa kushirikisha watu wanaoishi na ulemavu kwa sababu unapoona kipindi cha uchaguzi ushiriki wa watu wenye ulemavu unahitaji kuzingatiwa," alisema.

"Watu wenye ulemavu katika kipindi cha uchaguzi wanatakiwa kutumia haki ya demokrasia kuwachagua viongozi bora na wanaowaamini watashirikiana nao kuwapa vipaumbele kama watu wenye ulemavu," aliongeza.

Alisema watahakikisha wanajenga dhana nzuri ya utawala bora, lakini kusaidia ukuaji wa demokrasia nchini.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Ushiriki Tanzania, Israel Ilunde, alisema katika kuhakikisha wanakuwa na uchaguzi bora, wamehakikisha kumekuwa na mabadiliko ya kisera, kimfumo na kitaasisi.

Alitoa wito kwa jamii pamoja na wadau wengine wa maendeleo na serikali, kuunga mkono asasi za kiraia zinazoanza kufanya kazi muhimu za kusaidia jamii ili kujenga nguvu za pamoja.

"Jamii pamoja na wadau wengine wa maendeleo na serikali tunaomba mziunge mkono asasi za kiraia zinazoanza kufanya kazi muhimu za kusaidia jamii ili waweze kupunguza mzigo ambao wanaufanya kwa kutumia nguvu ndogo kuwa pamoja, kujenga nguvu za pamoja kupitia mitandao," alisema Ilunde.

## Kukithiri matukio ukatili kingono walishtua Dawati la Jinsia

**Na Allan Isack,** ARUMERU

ONGEZEKO la matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto wa kiume yanayoripotiwa kufanywa zaidi na ndugu wa karibu wa watoto hao katika Wilaya ya Arumeru, yamelishtua Dawati la Jinsia la Halmashauri ya Arusha.

Kanzidata ya ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Arusha kwa mwaka huu, inaonyesha kuwa ukatili wa kingono ni tishio jipya kwa watoto wa kiume, huku matukio ya ukatili wa wanawake na watoto bado yapo sana katika mkoa huo.

Kutokana na tishio hilo, Ofisa Dawati la Jinsia wa Halmashauri ya Arusha, Rovil Nguyaine, alisema kuna umuhimu kwa wazazi na walezi kuanza harakati madhubuti ya kupambana na ukatili wa kingono dhidi ya watoto wa kiume, kama inavyofanyika kwa watoto wa kike.

"Wazazi au walezi jengeni desturi ya kushirikiana na walimu katika kupambana na ukatili wa kijinsia, hakikisheni mnakuwa karibu na watoto wenu, kwa kuwa hali ya ukatili ni mbaya sana hasa kwa watoto wa kiume," alisema.

Aidha Nguyaine alisema ongezeko la kasi la matukio ya ulawiti kwa watoto wa kiume, linasababishwa na baadhi ya wazazi na walezi kutokuwa nao karibu, kutokana na dhana potofu kuwa wanao uwezo wa kujitetea kiume.

Alisema ni jukumu la wazazi na jamii, kuhakikisha wanawalinda watoto dhidi ya ukatili wa kijinsia na siyo watoto wa kike peke yao, kwa kuwa wote ni sawa na wanahitaji kulindwa kuanzia nyumbani, njiani mpaka shuleni.

Juzi Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha (RAS), Missaile Mussa, alinukuliwa akisema matukio ya ukatili wa wanawake na watoto, bado yapo kwa wingi katika mkoa huo, kwa kuwa mwaka 2021/2022, jumla ya matukio 4,705 yalilipotiwa na kati yake matukio 4,013.

Awali Mratibu wa Mradi wa Kupinga Ukatili wa Kingono dhidi ya watoto wa kiume wa Shirika la CWCD, Mariam Rashid, alisema lengo la kikao kazi hicho ni kukumbushana majukumu kwa wajumbe wanaotekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na kuwashirikisha kushiriki mradi wa ukatili wa kingono kwa wavulana unaoendelea kwenye kata zao.

Mmoja wa wajumbe wa MTAKUWWA katika Kata ya Moivo, Wilaya ya Arumeru, Elizabeth Mollel, alilitupia lawama Jeshi la Polisi kwa kuwa sehemu ya kikwazo cha ufuatiliaji wa kesi za ukatili na kusababisha usumbufu wakati wa upatikanaji na ushughulikiaji wa majibu ya fomu namba tatu ya Polisi (PF3).

# Watakiwa kuwafichua wanaoendeleza vitendo vya ukatili wa kingono

**Na Allan Isack,** LONGIDO

MTANDAO wa Polisi Wanawake nchini (TPF NET), umewapa somo wanawake wa jamii ya kifugaji ya kimasai wanaoishi Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, kuwafichua wanaume wa kabila hilo wanaoendeleza matukio ya ukatili wa kingono, vipigo na ukatili wa kiuchumi.

Akizungumza jana na wakazi wa wilaya hiyo katika eneo la Namanga, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP), Edith Swebe, alisema Longido ni miongoni mwa wilaya ambazo zinatishiwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia, lakini wananchi wake wamekuwa wakiwaficha wahalifu.

SSP Swebe, alimwakilisha Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi (ACP), Justine Masejo, katika kilele cha siku 16 za maadhimisho ya kupinga ukatili wa kijinsia. "Umefika wakati muafaka sasa kwa wananchi kuwaibua na kuwafichua watu wachache wanaofanya vitendo vya ukatili katika jamii. Jeshi la Polisi, litaendelea kufanya doria pamoja na kutoa elimu kuanzia ngazi ya familia, mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi taifa ili kuhakikisha tunatokomeza na kumaliza kabisa matukio ya ukatili na watakaobainika kufanya vitendo hivyo watafikishwa kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Kabla tamko hilo la Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Boniphace Lugola, aliwasihi wananchi, viongozi wa vitongoji, vijiji na watendaji wa ngazi zote, kila mmoja kwa nafasi yake kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo, kwa kufuatilia na kuwafichua wahalifu wote wanaojihusisha na matukio hayo.

Alifafanua kuwa serikali kupitia wasaidizi wa kisheria katika maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakiwafikia wananchi hadi vijijini kwa ajili ya kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia.

"Tatizo kubwa hapa watu ni kuvunja ukimya kwa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii zinazotuzunguka," alisema.

Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya ya Longido, Mrakibu wa Polisi SP, Leah Ncheyeki, alisema wilaya hiyo ilipata mafanikio kwa jumla ya kesi 36 zilifikishwa mahakamani na watuhumiwa walipatikana na hatia na kuhukumiwa.



Mafundi wakipima upana wa barabara inayotoka Songe makao makuu ya Wilaya ya Kilindi kuelekea Gairo Mkoa wa Morogoro eneo la Kwasantemo mjini Songe, jana. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Shule ya Sayansi Arusha yaibuka kidedea mashindano Afrika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI wa kidato cha tano wa Shule ya Sekondari ya Sayansi Arusha, wameibuka washindi wa kwanza katika mashindano ya kutafuta kampuni bora ya vijana Afrika iliyoiva katika uibuaji wazo la kibiashara.

Mashindano hayo yaliyofanyikia katika Jiji la Lagos nchini Nigeria, yalizishirikisha nchi tisa za Afrika ambazo ni Afrika Kusini, Zimbabwe, Zambia, Tanzania, Nigeria, Ghana, Eswatini, Kenya na Uganda.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Arusha, Abel Ntupwa, akizungumzia jana ushindi huo, alisema uwezo huo ulionyeshwa na shule hiyo ni funzo kwa shule nyingine kuiga mfano huo.

"Hii sasa inazifanya shule nyingine kuiga kuwaandaa wanafunzi kuwa na miradi yao wakiwa shuleni na kwenda kidigitali zaidi. Kama serikali tunaangalia namna ya kushirikiana na shule hii ya Sekondari ya Sayansi Arusha ili ubunifu huo uweze kuzifikia shule zote mkoani Arusha," alisema.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Nuhu Hatibu, alisema wamefurahi kwa namna ambavyo wanafunzi hao wameibuka kidedea na kuiwakilisha Tanzania vyema, kwa kuwa ndio shauku kubwa ya shule hiyo, kuhakikisha kila mwanafunzi anaondoka na mradi wa kwenda kutatua tatizo katika jamii pindi anapohitimu.

Alisema malengo makubwa ya shule hiyo ni kutekeleza mtaala wa elimu kwa vitendo ulioanzishwa na serikali na tayari unafanya kazi shuleni hapo, kwani elimu ya mwanafunzi inapimwa kwa vitendo kulingana na kile alichojifunza na siyo kujaza mitihani kwa muda aliokaa darasani.


Alisema: "Elimu hii ya mafunzo kwa vitendo inatakiwa ianzie ngazi ya elimu ya awali hadi vyuo vikuu, ili kuweza kupata wataalamu wengi zaidi waliobobea katika masuala mbalimbali kuanzia ngazi ya chini kama ambavyo leo wanafunzi hawa wakihitimu tayari wana kampuni yao."

Mmoja wa wanafunzi hao Koko Georgies, ambaye ameshinda nafasi ya kwanza ya kiongozi bora chipukizi kutokana na kuanzisha kampuni ya mauzo sokoni kwa njia ya mtandao (Kibega) ambayo inamrahisishia mteja yoyote kufikishiwa huduma hiyo popote alipo baada ya kufungua app hiyo kwa njia ya simu.

Koko alisema wameweza kubuni mradi huo ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo ambayo hutolewa shuleni hapo na kumwezesha kila mwanafunzi kuja na ubunifu wake ambao utasaidia kutatua tatizo ndani ya jamii husika.

"Mimi na wenzangu tulifikia hatua ya kubuni app hii, ambayo inasaidia kutatua tatizo kwenye jamii kwa mfano mtu yupo nyumbani anaumwa na anahitaji matumizi ya nyumbani, akifungua app hii ya Kibega anapata huduma zote anazohitaji baada ya kulipia moja kwa moja na kufikishiwa huduma hii, ndani ya muda mchache na ubunifu huu ulikuwa wa kipekee ndiyo maana tukaibuka washindi na kuiwakilisha nchi katika mashindano hayo," alisema.

Kampuni hiyo ya Kibega, inaendeshwa na wanafunzi wenzake wawili, ambao ni Ofisa Masoko wa Kampuni hiyo, Mwanahawa Ally na Junior Bonaventure (Mhasibu), huku wote wakiwa ni wanafunzi wa kidato cha tano shuleni hapo.





# DC atoa onyo kwa wafugaji watakaoingiza mifugo KINAPA

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema wafugaji wanaofikiria kwamba wanaweza kuichezea serikali kwa kuingiza mifugo katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) ili kutafuta malisho, wajiandae kupoteza mifugo kwa kuwa itauzwa kwa mnada.

Alitoa tahadhari hiyo jana wakati akipokea timu ya watu 200 wakiwamo mabalozi, maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na wanahabari waliopandisha Bendera ya Taifa kwenye kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro kama sehemu ya maadhimisho ya Uhuru wa Tanganyika.

"Tumesema kwamba kuanzia sasa tutataifisha mali zote, ikiwamo mifugo inayoingizwa katika hifadhi hii kinyume cha sheria, kwa kisingizio cha kutafuta malisho. Lakini hivi karibuni uliibuka moto katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro. Wapo wanaoingia na kuua wanyama wadogo na kuvuna asali, naonya mara ya mwisho, baadaye msinilaumu," alisema.

Kwa mujibu wa Babu, kati ya watu 200 waliopanda Mlima Kilimanjaro, waliofanikiwa kufika kilele cha Uhuru ni 101.

Awali, kiongozi wa timu hiyo, Brigedia Jenerali, Salum Numbe, akizungumza kwa niaba ya maofisa na mabalozi hao, aliomba serikali kwa kushirikiana na kampuni za utalii kuona namna ya kuwasaidia wapagazi, kupata bima za afya ili kuwa na uhakika wa afya zao, wanapokuwa wakitekeleza shughuli za kusaidia kupandisha wageni mlimani.

# Diwani atangaza kiama kwa vijana wanaotelekeza watoto

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

TABIA ya vijana kuwatelekeza watoto wao kwa bibi na babu limemvuruga Diwani wa Masama Magharibi, Mashoya Natai ambaye ameapa kuwabana wapigakura wake wanaojificha nyuma ya ukatili huo.

Kata hiyo inatishiwa na ongezeko kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ambao wazazi wao wako hai na wameacha majukumu ya kulea na kukimbilia mijini kutafuta maisha.

Akizungumza jana kuhusu wimbi hilo, Diwani Natai, alisema kwa sasa watoto wengi wanaopokelewa katika kituo cha kulea yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Lukani Children Center, ni wale walioachwa kwa babu na bibi, huku wakiwa hawana uwezo wa kuwahudumia chakula, mavazi na kuwapa elimu.

"Watoto wengi tunaowapokea kwenye kituo hiki, unakuta aidha anaishi na bibi zao au babu na wametelekezwa na baba na mama zao. Wengine ni yatima waliofiwa na wazazi, ila hawa waliotelekezwa wanaongezeka siku hadi siku. Huu ni ukatili usioelezeka na hatuwezi kuendelea kukaa kimya, lazima tuzungumze nao kuhusu malezi na makuzi ya watoto hawa," alisema

Kutelekeza mtoto ni kosa la jinai, kwa mujibu wa Sura ya 16 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Kifungu cha 166 ambacho kinaelekeza kuwa, mtu yeyote ambaye ni mzazi au mlezi au mtu mwingine mwenye uangalizi halali wa mtoto yeyote mwenye umri usiozidi miaka 14, hali ana uwezo wa kumhudumia mtoto, kwa kuamua au kinyume cha sheria au bila sababu za msingi akakataa kumhudumia na akamtelekeza mtoto bila msaada, atakuwa ametenda kosa.

Diwani Natai, ameiomba Halmashauri ya Wilaya ya Hai, wafanyabiashara, taasisi za umma na binafsi, kukiunga mkono kituo hicho kwa kukipatia misaada ya kibinadamu ikiwamo chakula, nguo, magodoro na mahitaji mengine muhimu ili kukiwezesha kuhudumia watoto hao wanaoongezeka kila uchao kwenye kata hiyo.

Msimamizi Msaidizi wa Kituo hicho, Mwalimu Ester Lyamuya, alieleza Nipashe kuwa, kituo hicho kilichoanzishwa mwaka 2017, kina watoto 45 ambao wanasomeshwa katika Shule ya Msingi Lukani, Sufi, Lokiri (Wilaya ya Hai) na Shule ya Msingi Lawate iliyoko Wilaya ya Siha.

Ripoti ya Jeshi la Polisi nchini, inaonyesha kuna ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili dhidi ya watoto, wakati mwaka 2020, kulikuwa na visa 7,388 viliripotiwa kote nchini tofauti na mwaka 2015, ambapo matukio 5,803 yaliripotiwa.




Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka, akipeperusha Bendera ya Taifa baada ya kufanikiwa kufika kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro katika kusherehekea maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru juzi.
**PICHA: GIFT THADEY**

## Shirika lajitolea kufadhili utoaji chakula shule za msingi

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

NEEMA imeiangukia Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, baada ya Shirika la World Vision Tanzania kujitosa kuboresha taaluma katika shule zake za msingi kwa kufadhili utoaji wa chakula kwa wanafunzi.

Jana Mwakilishi wa Meneja wa Shirika hilo, Kanda ya Mashariki, Daniel Chuma, alisema uamuzi wao wa kufadhili utoaji wa chakula shuleni, unatokana na watoto wengi wanaosoma shule zisizotoa chakula shuleni, kujikuta dhaifu darasani kiasi cha kupunguza ufanisi wao katika kujifunza.

"Tulipofika wilayani Mkinga, tulikuta shule nyingi zina tatizo hilo na ikatubidi kuingia ubia na wenzetu wa Shirika la Save the Children na sasa tunatoa chakula shuleni, jambo ambalo limeongeza ufaulu kwa wanafunzi," alisema.

Mpaka sasa mashirika hayo mawili yanawagusa wanafunzi zaidi ya 28, 110 wa shule za msingi 53 katika wilaya mbili za Mkinga na Handeni, ambazo zilionekana kukabiliwa na uhaba wa chakula katika tathmini ya lishe nchini.

Miradi inayotekeleza na World Vision katika Wilaya ya Mkinga ni ya afya, elimu, maji, lishe, mazingira na masuala mtambuka, yakiwamo ya jinsia na afya ya mama na mtoto.

Chuma alisema kwa sasa shirika hilo ambalo linatekeleza miradi yake katika Wilaya za Kilindi, Handeni, Korogwe na Mkinga, mkoani Tanga, wametekeleza miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa mwaka huu wa fedha.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkinga, Amani Kisinya, akizungumzia uwekezaji wa miradi hiyo, alilishukuru shirika hilo kwa kutekeleza miradi mbalimbali katika wilaya hiyo.

Meneja Miradi wa Wilaya ya Mkinga, AP Evodia Chija, alisema miradi mbalimbali iliyoanza tangu 2010, wanaitekeleza katika kata saba ni Manza, Doda, Mtimbwani, Boma, Parungu Kasera, Duga na Mkinga, ambako wamejenga zahanati, vyumba vya madarasa, miradi ya mazingira pamoja na maji.

**Miradi inayotekeleza na World Vision katika Wilaya ya Mkinga ni ya afya, elimu, maji, lishe, mazingira na masuala mtambuka, yakiwamo ya jinsia na afya ya mama na mtoto.**

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 13, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Ni wakati wa kuifanya elimu iwe ya kizalendo badala ya 'mali binafsi'**



Ukurasa 15

Wazazi, walezi wapeni raha watoto wenu kwa kuwafanyia mambo haya



Ukurasa 17

**'Watoto kataeni kuguswa sehemu nyeti, pigeni kelele ili msaidiwe'**

ELIMU

**NA HAIKA KIMARO, LINDI**

AJABU SAA 5 KISIMANI

# Kusotea maji licha ya chanzo kuwa jirani, yakimwagika saa 24 kila leo

• Wanafunzi hoi wakichota ya shuleni na nyumbani



Wanafunzi wa Shule ya Nahama wakisaka maji kwenye dimbwi muda waliotakiwa kuwa darasani. **PICHA: HAIKA KIMARO**

Ni safari ya saa nne kwa basi kutoka Dar Es Salaam hadi Kijiji cha Njia Nne Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi. Baada ya hapo inaanza safari mpya ya bodaboda inayotumia takribani dakika 50 kutoka Njia Nne hadi Nahama, kijiji kilichoko kata ya Namayuni wilayani humo.

Kijiji cha Nahama chenye idadi ya wakazi 1,786 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 ni miongoni mwa vijiji 33 katika wilaya ya Kilwa ambavyo vinakabiliwa na uhaba wa majisafi na salama kwa matumizi ya watu na mifugo.

Miongoni mwa waathirika ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao nao hukabiliwa na tatizo la kuacha masomo ili kwenda kusaka maji kwa ajili ya familia zao nyumbani na pia kwa matumizi ya shule.

Mathalani, Mwandabu Said anasoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Nahama, akiwa na baadhi ya wenzake ni kama wanaishi kwenye bwawa la maji akisema kutokana na ukosefu wa maji baadhi ya wanafunzi hulazimika kukatisha masomo na kwenda kutafuta maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

"Shuleni kwetu kuna matatizo mojawapo ni ukosefu wa vyoo vya wanafunzi na walimu, lakini hatuna maji kwa ajili ya matumizi ya kila siku iwe jikoni kupikia, vyooni na kufanyia usafi maeneo mbalimbali kwa hiyo tumefika bwawani kuchota maji kama wanavijiji wengine." Anaimbia Nipashe.

Anaongeza kuwa mengine ni kwa ajili ya shule lakini wanaporudi nyumbani wanatakiwa kwenda kusaidia wazazi na walezi kutafuta maji ya matumizi ya nyumbani.

Kutokana na changamoto hiyo wanavijiji na wanafunzi hutegemea kutumia maji yanayopatikana kwenye mabwawa ya asili yanayojikusanya wakati wa mvua.

Mwanafunzi huyo anasema maji hayo pia hutumiwa na wanyama wafugwao na wa porini kama mbwa, fisi na mifugo kutoka sehemu mbalimbali baada ya

INAENDELEA UK.18

ELIMU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Ni wakati wa kuifanya elimu iwe ya kizalendo badala ya 'mali binafsi'

MIAKA 61 ya Uhuru wa Tanganyika inalikuta taifa katika utafiti, kutoa maoni na mijadala ya namna ya kuboresha mitaala ili iwe na tija kwa taifa kutokana na ukweli kuwa elimu inayotolea ina maswali zaidi kuliko majibu.

Kwa kuangalia nukuu ya Mwalimu Julius Nyerere Baba wa Taifa, elimu si mali ya mtu mmoja kama anavyoeleza:

"Wale wanaopata nafasi hii wana wajibu wa kulipa sadaka ambayo wengine wametoa. Wao ni kama mtu aliyepewa chakula chote kwenye kijiji kilicho na njaa ili apate nguvu za kwenda kuleta chakula kingine kutoka mbali. Ikiwa atachukua chakula hiki na asilete msaada kwa ndugu zake, ni msaliti. Vile vile, iwapo miongoni mwa vijana wa kiume na wa kike wanaopewa elimu na Watanzania watakuwa na mitazamo ya kujiona bora na kushindwa kutumia ujuzi wao kusaidia maendeleo ya nchi hii wanasaliti."

Nukuu hii inayoishi ya Baba wa Taifa inatakiwa kuwa kiongozi kwa kila aliyesomeshwa, akijihoji elimu aliyopewa anaitumiaje kunufaisha taifa na wengine?

Wakati huu, wadau wameanza kutoa maoni ya kuboresha mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ili ikidhi mahitaji ya Tanzania ya uchumi wa kati kwa vile mitaala bora inajenga msingi imara wa elimu, ambao ndiyo Nyerere anaouzungumzia.

Ni msingi huo utakaowawezesha wahitimu kuwa na ujuzi na maarifa stahiki na kuwajengea ari ya kupenda kujifunza zaidi ili kumudu kikamilifu mazingira wanayoishi na shughuli za maendeleo kiujasiriamali na kusaidia wengine.

Katika uwanja huo wa elimu ndani ya miaka 61 pamoja na kutoa maoni ya kuboresha mitaala ni vyema pia kukubali kuwa kama taifa lazima liamue elimu inayohitaji kwa kuwekeza kwenye kuzalisha utaalamu unaosaidia jamii na si mtu mmoja mmoja msomi ambaye si jamii mfano kijiji hata jirani zake hawanufaiki na usomi wake.

Kijiji au mtaa kina profesa au daktari mwenye shahada ya uzamivu pengine akibobea kwenye taaluma za viumbe bahari, uhandisi wa vyakula, umeme jua na kilimo au ufugaji.

Profesa au daktari huyo anakisaidiaje kijiji au mtaa? Amesomeshwa na pesa za serikali ambazo ni za Watanzania iwe mikopo ya Bodi ya Elimu ya Juu, Hazina au hata wahisani anatakiwa alete matokeo kwenye chuo anachofundisha na kwenye eneo lake na majirani au jamii.

Huo ndiyo uzalendo kwenye elimu mtaalamu huyo awe na elimu ya ujasiriamali asaidie kijiji awe na miradi inayozalisha, inayoajiri na kuinua maisha ya wengine wanaomzunguka.



Elimu ya kilimo inayotolewa iwezesha wahitimu kuzalisha kitaalamu, kuajiri wengine na kubadilisha maisha ya jamii kubwa. **PICHA: MARAFIKI WA ELIMU**

> Inawezekana wanaleta lakini ni kidogo na taifa linapoendelea kuwasomesha wataleta nini baada ya miaka mitatu ya shahada?

Kama Nyerere anavyosema: "Wale wanaopata nafasi hii wana wajibu wa kulipa sadaka ambayo wengine wamefanya. Wao ni kama mtu aliyepewa chakula chote kwenye kijiji kilicho na njaa ili apate nguvu za kwenda kuleta chakula kingine kutoka mbali..."

Mathalani, bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya mwaka 2022/23 inasema imeratibu maombi ya wanafunzi 112,228 kati ya 120,000 yaliyolengwa kujiunga na shahada ya kwanza katika vyuo vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu 74.

Taasisi za elimu ya juu ni nyingi zikikaribia 100, lakini zinatoa elimu inayoakisi uzalendo? Wasomi wote hao 100,000 wanapomaliza shule wanaleta mabadiliko kwa jamii zao? Mtaala unaoandaliwa uliangalie hilo.

Inawezekana wanaleta lakini ni kidogo na taifa linapoendelea kuwasomesha wataleta nini baada ya miaka mitatu ya shahada?

Kwa miaka 61 ya Uhuru inawezekana elimu imekuwa ni ya kutoa vyeti zaidi badala ya kujenga jamii yenye uwezo, maarifa na ujuzi vitu ambavyo vinahitajika kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania.

Elimu inayohitajika sasa ni kufanikisha mambo ya sasa na ya vizazi vijavyo kwa kutoa maarifa yanayohitajika kwa raia na mbinu za ujasiriamali ambazo zitamwezesha kila mmoja kupata maendeleo lakini kuchangia maendeleo ya wengine.

Uzalendo wa elimu, unawaibua wanafunzi kutoka kumiliki elimu kwa masalahi binafsi wanapokuwa wazalendo wanahakikisha kwamba elimu waliyopata inawanufaisha na kuwa baraka kwa wengine na taifa.

Tanzania kwa miaka mingi inawasomi wakiwamo maprofesa na madaktari waliochimbuka na kuandika tasnifu mbalimbali wasiishie kuonekana kwenye makabrasha lakini watumie utaalamu kusaidia majirani, vijana wasio na kazi kujiajiri au kuwawezesha kiajira kutokana na ujuzi na elimu waliyo nayo.

## MITAALA MABADILIKO

Katika kuboresha mitaala, Tanzania inahitaji kupata teknolojia yake inayofundishwa na kuboresha maisha ya Watanzania, mipya itakayokuja ibadilishe fikra na kufikiria.

Kwa mfano kama inawezekana mwanafunzi akimaliza darasa la saba awe na uwezo, ujuzi na mbinu za kuzalisha mboga za kulisha kijiji kizima, au hata na vingine majirani kutokana na kazi za kilimo.

Elimu za Ufundi zinazotolewa kwenye vyuo vya VETA ziweze kuzalisha wataalamu baada ya kumaliza kidato cha nne au cha sita, wanaoweza kugundua na kutengeneza vitendea kazi kama baiskeli zinazoweza kutumiwa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wakiziunda kwa malighafi na vifaa vinavyotoka nchini siyo kutegemea vipuri kutoka nje.

Baiskeli hizo zinazotengenezwa kwa gharama na teknolojia ya Kitanzania zikipatikana kwa bei nafuu zitatumiwa na wanafunzi wa msingi na sekondari wanaotembea umbali mrefu na huko ndiko kuwa na 'elimu baraka' kwa wengine.

Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya mwaka 2022/23 inasema imeratibu maombi ya wanafunzi 112,228 kati ya 120,000 yaliyolengwa kujiunga na shahada ya kwanza katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu 74.

Pengine mitaala inayoandaliwa kuchukua nafasi ya ile ya miaka 61 ya UHuru iangalie kuna haja ya kuwa na vyuo vikuu na taasisi zaidi ya 71 za elimu ya juu?

Mitaala inaweza pia kupendekeza elimu ya ufundi zaidi na hata kuachana na wingi wa vyuo vikuu ili kuwekeza zaidi kwenye ufundi unaosaidia vijana kuwa mahiri na wabunifu, wajasiriamali wanaobadili maisha ya Watanzania.

Mitaala inapoangalia miaka 61 ya Uhuru ijiulize mbona kuna mamilioni ya digrii mitaani lakini umaskini unazidi? Si kwa wenye digrii au shahada na madaktari, maprofesa tu na hata majirani zao na ndugu wa karibu nao hali si shwari sababu ni nini hasa elimu haijaleta baraka?

## UTAFITI KWANZA

Pamoja na kukusanya maoni kubadilisha mitaala jambo hilo haliwezi kufanyika bila kufanya utafiti wa kina ili ujibu ni masomo gani ya kutokuendelea nayo kwenye mitaala mipya na kwa sababu gani?

Ni yapi yanaondoka kwenye orodha na kwanini yaondolewe? Masomo ya ujasiriamali yanapoletwa ni kwa kiasi gani yatabadili sura ya elimu ya nchi na kuongeza maarifa mapya, ujuzi na uelewa miongoni mwa wanafunzi shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu.

Aidha, ubainishe wapi serikali iwekeze zaidi na utoe aina ya utaalamu upi utumike kufundisha taaluma, ujasiriamali, ubunifu na teknolojia.

ELIMU

NA ANKRAS LUOGA

NDANI YA LIKIZO...

# Wazazi, walezi wapeni raha watoto wenu kwa kuwafanyia mambo haya

WIKI hii ni mwanzo wa likizo kwa shule za msingi na sekondari japo hata vyuo vitaendelea kufungwa ili wanafunzi waungane na familia zao na wanajamii kwa mapumziko ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Ikiwa ni pamoja na kusherehekea sikukuu za Noeli na Mwaka Mpya 2023, katika mchakato huo kuna mambo ambayo wazazi na walezi wanatakiwa kuyafanya kama maandalizi ya kuwapokea na kukaa na watoto wao kipindi cha likizo.

Kwa wanafunzi wa chini ya miaka 18 ambayo kwa umri wao bado ni wadogo maisha yao hutegemea miongozo na maelekezo ya wazazi na walezi wao, hivyo ni lazima kuiandaa. Hali za watoto kipindi cha likizo, inaanza na maandalizi ya kuwapokea wanafunzi hao kwa ajili ya mapumziko, hapo kuna mambo mengi yanatakiwa kuzingatiwa na wazazi na walezi kwa watoto walitoka shuleni.

Moja ni kuwa mwaka wa masomo umekwisha, kwa hiyo ni muhimu kufanya tathmini ya kina ya maendeleo na changamoto za kielimu kwa mwaka mzima.

Pili, pamoja na watoto kupata muda wa kupumzika na kujiweka kando kidogo na mambo ya darasani, ili kupata muda wa kupumzisha vichwa na kujifunza vitu vingine vya kijamii. Na zaidi wengine hutumia muda huu kwenda kuwatembelea ndugu na jamaa hasa vijijini ili kuendeleza undugu na kuepuka kusahau asili zao kwa maana ya mila na desturi zao.

Hata hivyo wazazi na walezi lazima wakumbuke kuwa huu ni muda muafaka kwa watoto kujifunza zaidi masomo ya ziada 'tuitioni' ili kujikumbusha masomo yao na pia kujiandaa na masomo yanayoanza Januari 2023 pale shule zitakapofunguliwa.



Watoto wacheze wakati wa likizo lakini walindwe ili wasome. **PICHA: MKURANGA VILLAGE**

> Hili husababisha kukosa muda wa kufanya maandalizi ya likizo za watoto wao kama vile kukosa muda wa kwenda shuleni na kuonana na kuzungumza na walimu wa watoto wao.

### WAJIBU WA LIKIZO

Nini wajibu wa wazazi na walezi katika kuwaandalia watoto wao likizo yenye mafanikio? Hilo nalo ni swali la kujiuliza, kwanza ni kuanza kuandaa mahitaji kwa ajili ya watoto kwa muda atakaokuwapo nyumbani kama vile chakula, mavazi na malazi mtoto anapokuwa nyumbani.

Jingine muhimu ni wazazi na walezi kwenda shuleni na kuongea na walimu wa watoto wao ili kujua maendeleo yao kwa mwaka unaomalizika. Kusikiliza changamoto, fursa na mapendekezo ya walimu.

Na hii hufanyika kwa nia ya kujua sehemu ambazo mtoto amefanya vizuri kwenye masomo na maeneo yenye changamoto. Hivyo kujiandaa kwa kumtafutia msaada wa masomo ya ziada atakapokuwa nyumbani kwa maana kuanzia wiki hii au ijayo.

Hii ni pamoja na kumtafutia masomo ya ziada kulingana na upungufu wa mtoto utakaobainika baada ya kuongea na walimu wa mtoto na pia mtoto mwenyewe.

### HALI IKOJE?

Tujiulize kwa sasa hali halisi ikoje katika jamii yetu? Kuna mengi ndani ya jamii kumekuwa na maandalizi duni ya wazazi na walezi kwa ajili ya kuwapokea watoto hasa kuelekea muda wa mapumziko.

Hii inatokana na maandalizi yasiyo sahihi yanayoletwa na kubadilika kwa mifumo ya maisha ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kuwa na majukumu mengi ya kimaisha hasa kutafuta pesa na mahitaji mengine ya kuendesha familia zao. Mfano, wazazi hasa wale wanaofanya kazi iwe ya umma au binafsi, wafanyabiashara na watu wengine wametingwa kupindukia na kutafuta hela na kuondoka nyumbani alfajiri na kurudi baada ya saa 4.30 usiku.

Hili hupelekea kukosa muda wa kufanya maandalizi ya likizo za watoto wao kama vile kukosa muda wa kwenda shuleni na kuonana na kuzungumza na walimu wa watoto wao.

Hivyo kukosa kujua maendeleo na changamoto za watoto wao kimasomo ambazo zingeweza kutatuliwa kipindi cha likizo zao. Na hii ni dalili wazi ya kushindwa kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa elimu ya watoto wao.

Tukumbuke kuwa bila kuongea na kushauriana na walimu si rahisi wazazi na walezi kufanya ufuatiliaji wa ukaribu wa elimu ya watoto wao. Mwisho wa haya yote ni kulipa ada bila kujua maendeleo ya watoto wao kielimu na kushindwa kuwasaidia ikiwa ni pamoja na kushirikiana nao kutatua changamoto na matatizo ya kielimu.

Mfano, kushindwa kujua na kutafuta masomo ya ziada ambayo watoto wao wamekuwa na changamoto zaidi kwa mwaka unaokwisha ila hufanya hivyo kwa kufuata mkumbo wa majirani hasa kwa kusikia kuwa somo fulani ngumu basi naye hufanya hivyo.

Bila kujua je, mtoto wake ana changamoto kwenye somo gani? Na hivyo kuhitaji msaada katika eneo au somo husika.

### CHA KUFANYA

Ni muhimu kwa wazazi na walezi watenge muda wa kwenda kuonana na kuongea na walimu wa watoto wao shuleni. Hili litasaidia katika kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa maendeleo ya mtoto.

Kujua maeneo anayofanya vizuri na yale yenye changamoto hivyo kuhitaji msaada au juhudi zaidi.

Pili, ni wazazi na walezi kuanza kufanya maandalizi ya mipango na rasilimali zitakazotumika kumsaidia mtoto kupata msaada wa ziada katika maeneo ambayo ana changamoto zaidi. Kwa ujumla wazazi wanatakiwa kujua nani na wapi msaada huo unaweza kupatikana mfano ni wapi masomo ya ziada yanapatikana kwa kuzingatia changamoto za mtoto wake.

Pia kuanza kuweka akiba ili kulipia masomo hayo ili mtoto aweze kusaidiwa na kuondokana na changamoto zinazowakwamisha, ikumbukwe, bila kumsaidia mtoto katika kutatua changamoto zake, unawapa walimu mzigo mkubwa na wakati mgumu sana katika kutekeleza majukumu yao.

Bila kufanya hivyo ni kuwaandalia watoto mazingira ya kuzurura, kucheza kupitiliza, kushinda na kukesha kwenye vibanda vya kuonyesha picha na tamthilia zisizo na maadili na kusahau kulala, kutosoma mpaka likizo inaisha hivyo kusahau kabisa mambo ya elimu hivyo kuanza tena upya kipindi shule zitakapofunguliwa.

Wanafamilia wakumbuke kuwa katika kujiandaa kikamilifu kwa kutimiza jukumu hili muhimu lazima walezi na wazazi wazingatie misingi yaifuatayo, maandalizi ya utoaji wa rasilimali zitakazohitajika kuwezesha utekelezaji wa hatua za kubadilisha rasilimali na kuwa bidhaa au huduma na kuchua hatua za kurekebisha kasoro zilizokitokeza mapema ili kutoa mazao bora yaani mwisho kupata matokeo bora ambayo ni kufanikiwa kuwa na watoto wenye elimu na maadili bora katika jamii.

Ikiwa ni pamoja na mzazi au mlezi kumwandalia mtoto mazingira ya kuwa na muda wa kutosha wa kupumzika, nafasi kujisomea, muda wa kucheza kwa kiasi, chakula, upendo na heshima.

Hii itasaidia kuwa na mipango mizuri na kufanya watoto kuona thamani ya muda wa likizo yao bila kusahau masuala ya elimu.

Wito wangu kwa jamii ni kuwa wazazi au walezi aanze sasa maandalizi ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa elimu ya watoto wao. Hasa katika kipindi tunapoelekea kuanza likizo za mwisho wa mwaka.

Hii inaanza na kuonana na kuongea na walimu wa mtoto wenu ili kujua maendeleo na changamoto za kielimu. Wazazi na walezi lazima waanze kuandaa mipango na rasilimali za kuwasaidia watoto wao katika kuondokana na changamoto zao za kimasomo, hii ni pamoja na kutafuta mahali na gharama halisi ya kupata masomo hayo.

***Mwandishi ni mhadhiri msaidizi Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.***

***MAONI 0757-645746***

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA




Watoto wakiozwa huingizwa kwenye maisha mapya na majukumu wasiyoyajua wala kuyamudu na kuwaongezea matatizo. **PICHA: AFP**

# Ndoa utotoni zilivyo mzigo kwa mabinti, jamaa zao

• Ni migogoro, kusuluhishwa kila uchao

NDOA za utotoni kinatajwa kuwa kikwazo kwa mafanikio ya kielimu na kimaisha kwa baadhi ya wasichana ambao wanalazimika kufuata matakwa ya wazazi na walezi, wanaotamani kupata fedha na utajiri kwa kuwaoza badala ya kuwasomesha.

Stephen Joseph, mkazi wa Kibaha anaeleza kuwa ndoa za utotoni mbali ya kuwakatili mabinti na kuwakwamisha ni sababu ya kurudisha nyuma maendeleo na kupoteza wakati, ni kwa sababu wenye ndoa na wazazi au walezi hujikuta zaidi kwenye usuluhishi badala ya kufanya mambo ya maendeleo.

"Mfano binti ameolewa bado ni mdogo akafika mtaani kwake kuna watoto wana umri kama wake wakicheza rede nje na yeye anajiunga, mume akimkuta hajafanya baadhi ya majukumu wanagombana. Kwa kuwa kiumri kuna vitu alivikosa basi atamwambia kama umenichoka nirudishe kwetu bila kujua anachofanya si sahihi."

"Haitaishia hapo siku nyingine atarudia watakuwa na kazi ya kupelekana kwenye vikao vya usuluhishi wa familia kwa hali hii hawawezi kutimiza majukumu wala kujielekeza kwenye maendeleo na umri unavyozidi kuongezeka wanakumbuka kilichowachelewesha," anasema Joseph.

Aidha, anasema ni vema taasisi zinazojihusisha na masuala ya watoto zikajikita vijijini kutoa elimu ya madhara ya ndoa za utotoni hasa kwa wazazi, walezi na shuleni walipo watoto hao ambako na kuwaelimisha kwa ufasaha.

> Kutokana na hali hii tumekuwa tukiwafuata makundi mbalimbali kule waliko kuwaelimisha haki zao kisheria na moja ya makundi hayo ni madereva boda, mama lishe na wajasiriamali wengine.

Anasema vituo vya msaada wa kisheria pia vinatakiwa kuchukua jukumu hilo badala ya kujikita kuelimisha zaidi masuala ya haki kwenye mirathi na majukumu ya huduma kwa wazazi wasiozingatia huduma kwa watoto wao.

Zainab Kassim, mkazi wa Kibaha anasema ili kukomesha ndoa za utotoni kwenye jamii serikali iandae kampeni maalumu badala ya kuacha kazi hiyo kufanywa na mashirika na taasisi za kiraia zinazotetea haki za mtoto.

"Binti kuozwa ni ukatili na hili linatakiwa kukemewa kuanzia ngazi ya kijiji ambapo matukio haya yanafanyika tusiyaachie mashirika binafsi peke yake huu ni wakati wa mtoto wa kike kujua kwa ufasaha haki zake na kuzipambania," anasema Kassim.

Humphrey Munuo wa Kituo cha Msaada wa Kisheria kilichoko Kibaha mkoani Pwani, anaeleza namna wanavyotoa msaada kwenye eneo la ukatili na elimu kwenye mapambano ya ndoa za utotoni.

Munuo anasema kituo chao kinatoa elimu kuhusiana na masuala ya ukatili, sheria ya mtoto, ya ndoa, mambo ya mirathi lakini pia wanashirkisha makundi mbalimbali.

Anasema kuhusiana na marekebisho sheria ya ndoa ya mwaka 1971 tayari wameshatoa mapendekezo ambayo wanadhani yakifanyiwa kazi yatamlinda mtoto wa kike.

Munuo anaeleza kuwa wanaelimisha jamii na mambo wanayoyafanya ni pamoja na ufahamu kuhusiana na mila potofu zilizopitwa na wakati ambazo bado zinaendelezwa na zimekuwa kikwazo kwa mtoto wa kike.

Anaeleza kuwa kituo chao kinaamini kuwapa elimu wanayoitoa itasaidia kuleta mabadiliko kwa mtoto wa kike hususani kuanzia kwa wazazi na walezi wao.

Anasema mwaka huu wamefikia watoto zaidi ya 3,762 kutoka shule mbalimbali za msingi zilizoko katika Wilaya ya Kibaha na kuwapa elimu hiyo kwa ufasaha.

"Makundi mbalimbali tunayaelimisha madhara ya ndoa za utotoni, kwa kuwa ndoa hizi zinafungwa kwa siri tunawapa uelewa na kuwasisitiza kuwa na ushirikiano na kituo chetu pale wanapobaini uwepo wa ndoa inayofungwa ambayo inamkatili binti," anasema Munuo.

Kadhalika, anasema katika kituo hicho wamekuwa wakipokea kesi nyingi zinazohusiana na matunzo ya watoto. Wapo wazazi wanakwepa majukumu yao na wengi kuwaachia malezi na mtunzo mama pekee jambo ambalo linaendelea kumkandamiza mwanamke."

"Na katika kesi hizi hasa kundi linaloongoza ni madereva wa bodaboda ambao wengi wao wamekuwa wakiwapa wanawake mimba na kukwepa majukumu," anaongeza Munuo.

Aidha, anaeleza kuwa kundi la wanawake wanaofika kuomba msaada wa kisheria kwa kutosaidiwa matunzo na waliozaa nao ni la wanawake wenye umri kuanzia miaka 20 hadi 30 ambao wengi wao nao huwaacha watoto kulelewa na wazazi au walezi wao, kwa hiyo motto anakuwa mikononi mwa bibi au babu.

"Kutokana na hali hii tumekuwa tukiwafuata makundi mbalimbali kule waliko kuwaelimisha haki zao kisheria na moja ya makundi hayo ni madereva boda, mama lishe na wajasiriamali wengine".

"Wapo ambao wameanza kubadilika na kupata uelewa kuwa suala la matunzo kwa mtoto sio hiari ni jukumu lao, tunaendelea na utaratibu wetu wa kutoa elimu kwenye makundi hayo na kuwapa msaada wa kisheria," anasema.

Katika maadhimisho ya siku 16 kupinga ukatili kituo hicho kinashirikiana na mashirika mengine kutoa elimu kwenye jamii hususani katika shule za msingi na sekondari.

Hivi karibuni akiwa Kibaha Mwanasheria wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) Tanzania, Zakia Msangi, anaeleza kuwa uanzishwaji wa madawati ya kijinsia kwenye shule na makundi mbalimbali ya jamii utasaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Anasema moja ya makundi yanayoathirika na vitendo hivyo ni watoto na kwamba madawati hayo yataundwa kwa kushirikiana na walimu wa malezi kwenye shule na yatakuwa yakitoa elimu kuhusiana na kupambana na ukatili wa kijinsia na kutoa taarifa za vitendo hivyo kwenye vyombo husika ikiwamo dawati la jinsia na vyombo vingine vya sheria

Zakia anasema katika shule hizo kutakuwa na wanafunzi wawili vinara ambao watakuwa na ujasiri wa kujieleza na wenye usiri pia kutakuwa na sanduku la siri la kutolea maoni.

Mkurugenzi wa Kituo Cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC), Catherine Mlenga, anasema wamekuwa wakipokea wateja ambao wengi wao ni wa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Catherine, wanashirikiana na vyombo vya sheria kuanzia polisi na mahakama kupambana na vitendo hivyo mkoa mzima wa Pwani na wanatoa elimu kwenye maeneo mbalimbali na makundi ya kijamii.

ELIMU
**NA PILLY KIGOME**

SIKU 16 UKATILI KIJINSIA

# ‘Watoto kataeni kuguswa sehemu nyeti, pigeni kelele ili msaidiwe’

KATIKA Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia uwekezaji mkubwa unalenga kuwapa elimu wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi na sekondari ili watoto waweze kuelewa kiufasaha matendo hayo yanayohusha nini na hatua za kuchukua kujinusuru.

Moja ya wadau wanaoelimisha watoto kuhusu ukatili wa kingono na unyanyasaji dhidi yao ni Shirika la Wanawake katika Juhudi za Kimaendeleo (WAJIKI), wanaoeleza kuwa kila mmoja ana jukumu la kuilinda jamii anayomzunguka hasa watoto ili kustawisha familia, jamii na taifa bora.

WAJIKI wanaamini kuwa ulinzi wa chipukizi au watoto kwa kuwaelimisha mara kwa mara ili wafikie malengo yao ya baadaye bila kuathiriwa kisaikolojia na kukatishwa ndoto zao ni jambo la kipaumbele, anasema Mkurugenzi wa shirika hilo, Janeth Mawinza.

Anaongeza kuwa wanaamini kuwa kuandaa watoto bora leo ni kutayarisha kizazi na taifa bora la kesho na kuwa na Tanzania yenye mafanikio.

Janeth, anawataka wanafunzi wawe wawazi katika kutoa taarifa wanapokutana na ukatili wa kimwili na kijinsia iwe ni nyumbani, shuleni na hata sehemu zingine kwani kufanya hivyo kutaweza kutokomeza ama kuondoa vitendo hivyo katika jamii kwa kuwaadhibu kisheria wahusika.

Janeth anayasema hayo katika Shule ya Msingi Mivumoni jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia unaoandaliwa na shirika hilo wenye kauli mbiu isemayo “safari salama bila ukatili wa kijinsia inawezekana” vunja ukimya kila uhai una thamani kubwa.

Anasema ni vizuri watoto wakapewa elimu stahiki na mara kwa mara kwa vile kurudia mara nyingi kuwafundisha kunawawezesha kujitambua ni jinsi gani ni muhimu kuripoti matukio hayo bila aibu katika sehemu mbalimbali kama polisi, shuleni, kwa wazazi na walezi na viongozi wa serikali ili kuchukua hatua.

Anawataka wanafunzi wanapoona dalili au viashiria vya ukatili wa kijinsia au kingono kama kuwagusa sehemu za siri, kuwashika mabinti matiti, kuwaonyesha picha za ngono, waripoti kwa walimu, wazazi au mlezi ili watuhumiwa wachukuliwe hatua stahiki kukomesha vitendo hivyo.

Mawinza anasema wanatakiwa kuongeza nguvu kuiunga mkono serikali katika kuijenga jamii na kuweka mkazo katika kusimamia sheria dhidi ya unyanyasaji wa watoto.

Anasema shirika hilo linatoa elimu kwa maneno na vitendo wakiongozwa na nyimbo maalum kuhusiana na ukatili wa kingono na kuwaelekeza wanafunzi maeneo hatarishi ambayo hawastahili mtu kuwagusa kwa namna yoyote.

Janeth anawakumbusha kuwa wasiruhusu kushikwa maeneo ya kifua kwa wanafunzi wa kike, kuguswa makalio na katika sehemu za jinsi au za siri kwa wanafunzi wa jinsia zote ni hatari kwao na wanatakiwa wapige kelele kwa sauti na kuomba msaada, wasikae kimya.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Dawati la Jinsia wa Manispaa ya Kinondoni, Zena Nalipa, aliyemwakilisha Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, anawaambia wanafunzi kuwa wasiyafumbie macho matendo ya ukatili wa kijinsia na kingono kwani kuyanyamazia ni hatari kwao na wataweza kuathirika na hasara nyingi.

Zena anataja kukatishwa masomo kwa mimba za udogoni, kuathirika kisaikolojia, kuambukizwa magonjwa, kuharabikiwa na maisha kutokana na ulawiti na hata wakati mwingine kufikiria kukatisha maisha kuwa ni moja ya matokeo mabaya ya ukatili wa kijinsia.

Anasema katika kuunga mkono serikali manispaa hiyo iko katika mikakati ya kutokomeza vitendo hivyo kwa kuwachukulia hatua wale wote wanaofanya ukatili dhidi ya watoto.

Clara Urasa Ofisa Maendeleo ya Jamii Dawati la Watoto kutoka Manispaa ya Kinondoni anasema serikali inaweka mipango mingi madhubuti yenye maudhui ya kuwalinda watoto katika janga la ukatili dhidi yao.

“Hatutafumbia macho vitendo viovu dhidi ya watoto wetu kwani vitendo hivyo vinawaharibu kisaikoilojia watoto na kusababisha kuwarudisha nyuma hasa katika masomo yao na kuwaharibia malengo yao ya baadaye.”

“Tunaendа kwa kasi ya serikali kutokomezaa vitendo vya uhalifu dhidi ya watoto, kuwahamasisha kuripoti na pia jamii kuwa macho na kukabiliana na unyanyasaji kila wakati,” anasema Clara.

Anawataka watoto wajilinde wenyewe kabla hawajalindwa kwani kufanya hivyo kutaweza kuisaidia serikali katika kutokomeza vitendo hivyo, wasikae kimya wakinyanyaswa lakini pia wajiepushe na makundi ya kihalifu na kuwasemea kwa walimu na walezi watoto ambao mienendo yao inakwenda kombo.

“Jilindeni wenyewe kabla hamjalindwa na watu wengine, elimu hii mliyopewa mnatakiwa muifanyie kazi, izingatieni. Wewe ndiyo unatakiwa uwe wa kwanza kutuambia sisi, ukinyamaza sisi hatutajua wala watuhumiwa hawatafuatiliwa,” anasisitiza Clara.

Akizungumza kwa niaba ya walimu; Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mivumoni, Mario Gandye, analishukuru shirika hilo la WAJIKI kwa kuwapatia elimu wanafunzi wa shule hiyo kwani ujio wao shuleni hapo umeleta hamasa kubwa na uelewa dhidi ya watoto wametambua na kuwaongezea uelewa kuhusiana na matukio hayo ya ukatili.

Anasema walikuwa wakipata taarifa tofauti kutoka majumbani kuhusiana na matukio ya ukatili na elimu hiyo imewafumbua macho na kuwapa uelewa mkubwa zaidi watoto kuhusiana na matendo hayo kwa ujumla wao na kutambua kutakiwa kutolea taarifa pindi wanapokutana na changamoto hizo.

Anaiomba WAJIKI kuendelea kutoa elimu katika shule nyingine ili kuwapa uelewa watoto kama walioipata wanafunzi wa shule hiyo na kuomba pia elimu hiyo iwe endelevu shuleni hapo kwa nyakati zijazo.

Wakiongea kwa nyuso za furaha baadhi ya wanafunzi kutoka shuleni hapo wanasema wamefurahi kwa ujio wa shirika hilo na wameweza kujitambua na kuongeza uelewa wa jinsi gani wanatakiwa kufanya wanapokutana na ukatili huo.

Wanasema kuanzia sasa wakikutana njiani na yeyote ambaye hawamfahamu akiwasemesha au kutaka kuwapatia zawadi, lift ya gari au pikipiki hawatakiwi kupokea zawadi hizo na pia watamweleza kuwa matendo hayo yanafanana na unyanyasaji wa watoto kijinsia.



Mkurugenzi wa Shirika la WAJIKI, Janeth Mawinza, akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mivumoni, kuhusu kujiepusha na ukatili wa kijinsia. **PICHA: PILLY KIGOME**

> “katika kuunga mkono serikali manispaa hiyo iko katika mikakati ya kutokomeza vitendo hivyo kwa kuwachukulia hatua wale wote wanaofanya ukatili dhidi ya watoto.

# Kusotea maji licha ya chanzo kuwa jirani, yakimwagika saa 24 kila leo



Wanavijiji wakihangaikia maji kwenye kisima kilichochimbwa lakini huduma haijasambazwa kufikia wanavijiji. **PICHA: HAIKA KIMARO**

**INATOKA UK.13**

wafugaji kutoka mikoa mingine kuhamia Nahama kutokana na ukame kwenye maeneo yao ya awali.

Hata hivyo, maji hayo hukauka kipindi cha kiangazi na hivyo kuwalazimu zaidi wanawake wakiwamo wanafunzi na mabinti kutembea umbali wa takribani saa mbili kutafuta maji na hivyo kushindwa kufanya shughuli nyingine muhimu.

Asha Namweka mzaliwa na mkazi wa Nahama anasema kukosekana maji safi hulazimika kutembea umbali wa kilomita tatu kutoka yalipo makazi yao kwenda kuchota maji katika moja ya visima vilivyochimbwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) katika Kitongoji cha Kiwanga.

Lakini anasema maji yake, hayajasambazwa kufikia wateja na kuachwa kumwagika wakati wote.

"Tunapata shida kina mama na wasichana kwa sababu unaweza kutoka nyumbani saa 9:00 usiku, ukifika kisimani kuna msururu na unaweza kupata maji saa 1:00 asubuhi asubuhi takribani saa tano za kusota.

"Maji ni mengi lakini uchotaji ni wa usumbufu kutokana na kisima kukizibwa lakini bado maji yanavuja kidogo hivyo tunachota kidogo kidogo, tunaiomba serikali iyasambaze kwa wanavijiji tupate unafuu," anasema Asha.

> Mwaka wa fedha ujao tutajenga miundombinu kwa ajili ya kusambaza maji kwa wananchi, ili tuendeleze mradi wa Nahama.

Mussa Abdallah ni mkazi mwingine wa kijiji hicho anasema awali walilazimika kutumia maji ya mabwawa pamoja na wanyama lakini sasa maji mengi yameanza kukauka kutokana na ukame pamoja na ongezeko la wanyama wanaotegemea maji hayo hivyo kutumia maji yaliyochimbwa na RUWASA bila maelekezo.

"Tunashukuru serikali imetuletea mradi wa kisima kwenye kata yetu lakini changamoto inabakia kuwa baada ya maji kuchimbwa yameachwa bila kusambazwa yanamwagika na kuharibu mazao kwenye mashamba jirani na kisima," anasema Mussa.

**MAJI YATIRIRIKA OVYO**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nahama, Mohammed Ndiwate, anasema tatizo lipo na linakuwa kubwa kipindi cha ukame kwani bwawa wanalotumia limepungua, matumizi yakiongezeka.

"Sasa hivi kuna ukame wafugaji wamehamia katika maeneo yetu, maji wanayonywesha mifugo ndiyo binadamu tunayategemea kwa sababu hakuna miundombinu ya kuwazuia wanyama wasiyafikie. Changamoto ya maji ni kubwa sana licha ya kata yetu kuwa na chanzo cha maji chenye uwezo wa kuhudumia vijiji vyote," anasema Ndiwate.

Wakati Nahama wana shida hiyo kisima kina maji yanayomwagika saa 24 kwa mwaka mzima yakitiririkia mashamba ya makazi ya jirani.

Mwenyekiti wa Kijiji anasema wakati kisima hicho kinachimbwa 2018 walielezwa mradi huo ni mkubwa utakaosambaza maji vijiji vya Nahama, Namakoro, Ngorongo, Namayuni na Liomanga vilivyoko kata ya Namayuni lakini mpaka sasa haujaendelezwa zaidi ya maji kumwagika ovyo.

"Toka walivyotoboa na kuona maji yanapatikana yalikuwa yanamwagika mengi sana wakayaziba ili yasichafuliwa lakini kutokana na maji kuwa mengi bado yanavuja ndio sababu yanatiririka kwenda kwenye mashamba," anasema Ndiwate.

**UTETEZI WA RUWASA**

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kilwa, Ramadhani Mabula, akizungumzia madai ya wananchi anasema wilaya hiyo ina vijiji 94 vya kufikishwa maji na kwamba tayari vijiji 60 vina majisafi na salama na kwamba vimebakia 34 ikiwamo Nahama.

Anasema kuna mipango mingi na wa kwanza katika Kijiji cha Nahama walishachimba kisima kirefu chenye maji safi na salama cha mita 150 chenye uwezo wa kuzalisha takribani lita 16,000 kwa saa.

"Mwaka wa fedha ujao tutajenga miundombinu kwa ajili ya kusambaza maji kwa wananchi, ili tuendeleze mradi wa Nahama," anasema Mabula.

Akizungumzia maji kumwagika ovyo katika kitongoji cha Kiwanga anasema wanafanyakazi tatu kila mwaka nazo ni kutafuta vyanzo vya maji, ujenzi wa miradi ya maji na kufanya upembuzi na 'kudizaini' miradi ya maji.

"Kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya utafutaji wa vyanzo vya maji, kufanya savei, hatuna fedha lakini tunakuwa tunajua sehemu fulani tukichimba tutapata maji hivyo mwakani tukipata pesa tunachimba sehemu tulipofanya savei,"anasema na kongeza;

"Sasa kisima cha Kiwanga ni katika vile ambavyo tulikuwa tunatafuta vyanzo vya maji, tulichimba visima 19 kwenye vijiji 19 lakini tulivyoviendeleza mpaka sasa ni sita na mwaka huu tunachimba visima nane."

Mabula anasema mwaka huu wa fedha wanatumia wastani wa Shilingi bilioni tatu kufanya miradi wanayoiendeleza na hivyo wananchi wakiwa na shida ya maji lazima kelele zitakuwapo akiahidi kuwa lengo lao ni kutatua kero hiyo.

## WANENAVYO MALENGA

### WABANGAIZAJI

Wapo wabangaizaji, kwetu kwao wengi sana,
Kujituma ni mtaji, wasiadhirike sana,
Na wala siyo kipaji, ni shida zinawabana,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Jinsi unabangaiza, hata Mungu akuona,
Njia yako aangaza, nawe uweze muona,
Hawezi kutelekeza, kesho yako taiona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Mifano iko lukuki, twasoma na tunaona,
Walisema hawatoki, sasa wanang'aa sana,
Vile hawakudiriki, nao kukubaliana,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Neno la Mungu lasema na hayo tunayaona,
Kwenye kazi zote njema, mwishowe kuna kuvuna,
Hivyo acha kulalama, ujishughulishe sana,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Mwenye nacho utaona, kama vile ajivuna,
Kumbe unavyomuona, alishapigika sana,
Sasa mwezi kauona, kivuli amekiona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Huyu Ruto twamuona, jinsi alibezwa sana,
Wengi walivyomuona, ya kwamba hafai sana,
Lakini aling'ang'ana, alipo tunamuona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Bangaiza bangaiza, kesho yako taiona,
Uzidi kujilemaza, utapata tabu sana,
Hilo linajieleza, na mambo tunayaona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

Nami ninabangaiza, mwanga nipate kuona,
Mbele nikijisogeza, niweze kutulizana,
Kivuli cha kupendeza, nami niweze kiona,
Jinsi unahangaika, wajivutia Baraka.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

HATIHATI UKAME

# Ianzishwe elimu na kampeni ya kitaifa upandaji miti asilia

WALIOKUWAPO miaka ya 1940 hadi mapema 1980 wana kumbukumbu za kuwapo uoto wa asili wa kijani uliokuwa ukiipamba Tanzania kwa kila upande. Uoto huo ulifanikisha mvua kunyesha kwa wakati, kila msimu, mito ikitiririka na kujaa maji karibu nchi nzima.

Mwanamuziki Mbaraka Mwinshehe, miaka ya 1970 alishuhudia, akaimba wimbo na kuisifia Morogoro kuwa inapendeza maji yatitiririka milimani na kuwaalika watu wajionee uzuri wa asili wa mkoa huo. Ulikuwa mfano wa namna Tanzania ilivyokuwa.

Ukungu ulishona kwenye milima na mabonde mengi, ulitanda na kusababisha giza na hata wakati mwingine ilikuwa vigumu kuonana na kuwatambua wengine waliokuwa mbele au nyuma yako iwe shuleni au mitaani kutokana na 'giza jeupe' lililofunga hata mchana tena kukiwa na baridi kila wakati.

Leo mambo yamebadilika. Jua na joto kali vimechukua nafasi na mwaka huu ukame umeshuhudiwa maeneo mengi ukisababisha uhaba wa chakula, kuua mifugo na hata kuwalazimisha wafugaji kulisha wanyama wao pumba. Upepo unavuma kwa mwaka mzima ukikausha maji, mito, mabonde, maziwa na ardhi inayobaki bila majani.

Ni mabadiliko ya tabianchi au athari za uharibifu wa mazingira duniani. Tatizo linaloanzia na nchi zenye viwanda vinavyozalisha bidhaa za kila aina na kujaza moshi angani. Lakini, huchochewa na matumizi ya nishati zenye hewa ukaa kwa wingi kama dizeli, petroli, gesi asilia na makaa ya mawe kwa upande mmoja.

Kadhalika, ukataji miti, kuchoma misitu, matumizi ya kuni, kilimo na ufugaji wa kizamani wa wanyama wengi wanaozalisha samadi nyingi inayochangia kuongeza hewa ukaa. Hayo ndiyo mabadiliko ya tabianchi ambayo athari zake zinaonekana kwa wengi, mfano kupata mavuno duni hasa kwa vile kilimo hutegemea mvua kwa asilimia 95 na inapokosekana ni njaa na vifo kwa mifugo.

Ukame ukizidi kama ilivyokuwa inaonekana mwaka huu, unakausha maziwa na mito na kuathiri maisha, ufugaji na uvuvi hivyo kudidimiza pato la taifa kwa vile kilimo kinachangia zaidi pato hilo.

Ni chanzo cha ajira huajiri watu wengi zaidi hivyo kinapoyumba nchi hupoteza mapato, aidha, kuongezeka njaa au uhaba wa chakula na mahitaji mengine yote muhimu kama malighafi viwandani.

Mabadiliko tabianchi huleta mafuriko na kuharibu miundombinu ya usafiri, ya nishati, maji na majengo mambo ambayo si mageni nchini.

Mabadiliko hayo ni tatizo ambalo linahitaji nguvu ya pamoja duniani, lakini kila taifa lina mchango wake, la muhimu ni uwekezaji na usimamizi kwenye sekta ya kuokoa mazingira na kuirudishia tena Tanzania uasilia au ukijani.

Kurudisha mazingira katika hali ya asili ni suala linalohitaji kupewa msukumo wa kipekee na nguvu mpya ili kufanikisha kupanda miti ya asili wala si ya kigeni.

Ikiwezekana kuanzia sasa kuwe na kampeni ya kitaifa ya kuandaa miche na mbegu za asilia kulingana na mazingira inapopatikana miti inayopandwa iwe mikoani, wilayani na vijiji.

Wakala wa Taifa wa Huduma za Misitu TFS na Wizara ya Maliasili na Utalii, zishiriki moja kwa moja kuandaa vitalu vya miti ya asili na mbegu ili zisambazwe kwa kila mkoa zikifikie ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya nao wazifikishe kwa viongozi wa vijini na mitaa, kazi inayofanywa na ofisa za misitu na mazingira.

Mbegu na miche ziwafikie pia viongozi na watendaji kwenye ofisi za taasisi za serikali kama mamlaka na wakala zote, shule za msingi na sekondari, vyuo vya chini, kati na vikuu, majeshi kama Polisi, JWTZ, JKT na Magereza.



Mkuyu ni mti asilia ambao unaotunza maji. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI**

Miche ifikishwe pia kwenye makanisa, misikiti, asasi za kiraia na watu binafsi, viwandani, kwenye masoko, hospitalini na kwenye bustani za hoteli na migahawa na kupandwa.

Upandaji miti unahitaji ufuatiliaji na ni suala ambalo halina kutengea bajeti kubwa iwe vyuoni, vijiji, majeshini au halmashauri au kwenye shule au kwenye hospitali.

Ni kwa sababu ni sehemu ya majukumu ya kila siku ya utunzaji wa bustani au mazingira usiohitaji gari wala posho kwa ajili ya kwenda kukagua na kupalilia kwa vile kuna wahusika wanaofanya jukumu hilo kama waajiriwa.

Mbegu hizo zikifikishwa kwenye wilaya na mikoa mamlaka za maji na usafi wa mazingira zishirikiane na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) ziwapatie wahusika maji ili kutunza vitalu na bustani.

Kupanda miti kuhusishe pia mamlaka za kuendeleza mabonde kama vile la RUBADA Mto Rufiji, Pangani, Mto Ruvu na Bonde la Ziwa Victoria ili kupanda na kutunza miti kwenye vyanzo vya maji.

Mamlaka hizi zipande miti ya asili kwenye vyanzo vya maji na mabonde inayoyasimamia wakati Wakala wa Barabara wa Taifa (TANROADS) na ule wa Barabara za Mijini na Vijijini TARURA zikipanda miti pembeni ya barabara kote nchini.

> Miringaringa na misesewe inavuta na kuhifadhi maji lakini pia majani yake ni mapana makubwa na yanayotoa rutuba ardhini hivyo hutunza udongo.

Kwa upande huo unahitajika utalaamu pengine kujua aina za miti zisizopasua lami au kusambaza mizizi barabarani na kwenye madaraja na umbali kati ya mti na aina inayohitajika.

### MITI ASILIA

Eneo mojawapo la kupewa kipaumbele ni kupanda miti ya asilia na siyo ya kigeni kama 'ashoki, mikaratusi na mijohoro. Mkazo uwe kuwaelimisha wananchi umuhimu na faida za miti asilia, kwa mfano mkoani Kilimanjaro kuna miti kama mikuyu au mikuu, mivumo, misesewe, miringaringa, milama na mikufi.

Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) linaitaja miti ya jamii ya mikuyu na mivumo kuwa inahifadhi maji ardhini na pia ina uwezo wa kuvuta mvua.

Aidha, inaeleza kuwa miti hiyo inastawi kwa muda mfupi takribani baada ya miaka minne hivyo si miti ya kuupuzwa.

Miringaringa na misesewe inavuta na kuhifadhi maji lakini pia majani yake ni mapana makubwa na yanayotoa rutuba ardhini hivyo hutunza udongo.

Baadhi ya wakazi wa Kilimanjaro wanaueleza msesewe kuwa hutumiwa pia kuchachusha pombe ya mbege unapokomaa majani yake hudondosha maji ikimaanisha kuwa mizizi yake inahifadhi maji.

Lakini, juhudi za kupanda miti hazitafanikiwa iwapo serikali haitadhibiti uvunaji asali kienyeji unaotumia moto. Ni vyema kufuga nyuki 'wasiong'ata' na kusambaza teknolojia ya kuvuna asali bila moto ili kulinda mazingira.

### KILIMO MABONDENI

Kulima kwenye mabonde ya mito kusiachwe tena kubakia kuwa suala la kupuuzwa. Sheria iongeze umbali na ikibidi uwe hata mita 100 kutoka mtoni na iwe marufuku kulima na kuanzisha bustani chini na pembeni ya madaraja pia.

Kadhalika suala la kuchimba mchanga kwenye mito, chini ya madaraja na kwenye makalvati nalo lidhibitiwe kwa sheria na badala yake kupanda miti ya asili na kuondoa uharibifu wa mazingira na miundombinu ya maeneo hayo kiwe kipaumbele.

Kudhibiti na kuzuia ukataji miti kiholela, kuchoma mkaa na kilimo kila mahali pamoja na juhudi hizo, huenda kwa miaka mitano, Tanzania ikawa ya kijani na maji kutiririka kwa wingi kama ilivyokuwa wakati wa Uhuru mwaka 1961.

## HABARI PICHANI




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizindua rasmi huduma ya intaneti katika Mlima Kilimanjaro kuanzia lango la Marangu (Marangu Gate) hadi kilele cha mlima huo cha Uhuru Peak. **PICHA: JAMES LANKA**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omar Mgumba, akiruka na morani wa Kimasai kwenye sherehe ya maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru mjini Songe wilayani Kilindi. **PICHA: DEGE MASOLI**




Ofisa Elimu Mkoa wa Arusha, Abel Ntupwa, akiwapongeza wanafunzi (pichani) waliofanya vizuri mashindano ya kutafuta kampuni bora ya vijana Afrika na ukuaji wa wazo la kibiashara yaliofanyika Lagos nchini Nigeria na kuibuka washindi wa kwanza. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## CHEMSHABONGO NA -00 29 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. hutumika kusikiliza sauti
6. maoni
8. Muscati ni mji wake mkuu
9. fanya kuwa kamili
11.shuhudia kwa macho
12.chukua bila ya idhini
13.alika watu kwako
14.Uo 17.heshima
18.uwazi mwembamba ukutani
20.shauku ya kutenda jambo
21.tembea kwa kuburuza tumbo
23.nasaba


Chini:
1. gulio
2. Itikadi
3. shika
4. kiungo kitoacho nyongo
5. mafuta
6. hotuba inayosomwa kwa mgeni rasmi 7. Tehrani ni mji mkuu
10.misa 15.Msafiri
16.nguo
17.Siha 19.Ng'ata kwa meno
22.labda



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

TAKATA
UNGANA
KAMA
ADANA
DARASA
ULIMI
AMBIWA
MASAA
ADABU
MAKUNDI
AINA
ATHARI

IBUA
ABU
ANA
KAKA
LOME
MBAO
SOMA
KATA
DAI
DAKA




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | K | A | T | O | | U | T | U |
| K | | C | | M | | | A | |
| A | D | H | A | B | U | | N | |
| T | | A | | E | | A | G | O |
| E | | M | W | A | N | Z | O | |
| | K | A | A | | | A | | M |
| | I | | K | W | A | N | Z | A |
| T | A | M | A | A | | I | | T |
| | M | | T | A | B | A | K | A |
| K | A | Z | I | | | | | A |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | G | A | O | | | A | | B |
| Y | | D | | K | E | N | Y | A |
| O | B | A | M | A | | G | | R |
| T | | M | A | D | H | A | R | A |
| A | J | U | Z | A | | Z | | K |
| | U | | A | | M | A | D | A |
| M | A | K | O | S | A | | H | |
| K | | A | | | A | D | A | A |
| O | M | B | A | | N | | N | |
| A | | A | | B | A | L | A | A |



## Uongozi kununua mitambo ya kuchonga barabara

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amesema uongozi wa mkoa huo unatarajia kununua mitambo ya kuchonga barabara katika mwaka wa fedha ujao, ili kuboresha miundombinu ya barabara.

Aliyasema hayo alipofanya ziara katika Kata ya Masoko wilayani Rungwe kusema kwamba barabara nyingi za mkoa huo zitaboreshwa baada ya kununuliwa kwa mitambo hiyo.

Homera alisema mitambo hiyo itakuwa inahamishwa kutoka katika halmashauri moja kwenda nyingine kwa lengo la kuboresha barabara ambazo hali yake siyo nzuri ili kuhakikisha hali ya usafiri na usafirishaji inaimarika.

Alisisitiza kwamba katika baadhi ya maeneo mkoani humo hasa ya vijijini miundombinu ya barabara siyo mizuri na hivyo inakwamisha shughuli za wananchi.

"Mkoa wetu una shughuli mbalimbali za uzalishaji lakini tatizo lililoko ni ubovu wa miundombinu, kwa hiyo tukishanunua miundombinu hii tutahakikisha tunaboresha barabara hizi kwa kiwango kikubwa," alisema Homera.

Katika hatua nyingine, Homera alisema serikali imeamua kuwasaidia wakulima nchini kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea ili kupunguza gharama hiyo.

Alisema ruzuku hiyo itasaidia kuboresha kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa ajili ya kuinua uchumi wa wananchi na taifa.

# Viongozi wa mila watakiwa kuhamasisha utunzaji mazingira

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

VIONGOZI wa mila katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameagizwa kuhamasisha wananchi kutunza mazingira kwa kuepuka kukata miti ovyo na kuchoma moto misitu ili kuepuka mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili dunia kwa sasa.

Mkuu wa Machifu wilayani humo, Joel Mwakatumbula, alitoa agizo hilo kwenye Tamasha la Utamaduni la Kufunga Mwaka 2022 lililofanyika katika Kitongoji cha London kilichoko Kata ya Kisiba na kushirikisha wadau mbalimbali wa mila.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kuwazuia wananchi kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji ili kulinda rasilimali hiyo ambayo kwa miaka ya karibuni imeanza kupungua kutokana na uvamizi wa binadamu.

Hivyo aliwataka kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika wakifanya shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira hasa kwenye vyanzo vya maji na misituni, huku akiwataka wananchi kuzingatia sheria ya mazingira inayowazuia kulima ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za mito.

"Tunawaomba pia viongozi wa serikali za vijiji kushirikiana na sisi kutunza mazingira, wamekuwa wakishiriki kuuza maeneo ambayo yamehifadhiwa, sasa tunakuwa kama tunapingana kitu ambacho sio sahihi," alisema Chifu Mwakatumbula.

Alisema waliamua kufanya tamasha hilo kwa lengo la kuikumbusha jamii kutunza mila na desturi za kitanzania na kuwazuia vijana kuiga tamaduni za kigeni.

Alisema tamasha hilo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Mkuu wa Machifu Tanzania Rais Samia Suluhu Hassan ambaye jina la kichifu anaitwa 'Hangaya'.

Chifu wa Kata ya Itete, Kuntukumbu Mwaikuka, alisema kulinda misitu ni miongoni mwa majukumu yao makuu na kwamba wao wanatumia njia nyingi za kulinda maeneo hayo ikiwamo njia za asili ambazo zingine hawaziweki wazi.

Alisema wanazuia watu kulima maeneo ya milimani kwa maelezo kuwa kilimo hicho kinasababisha mmomonyoko wa ardhi ambao mbali na madhara ya kimazingira lakini ina madhara kwa binadamu.

Alisema kilimo cha aina hiyo kimekuwa kikisababisha udongo kuhama kutoka kwenye maeneo ambayo unahitajika na kwenda kwenye maeneo ambayo hauhitajiki.

Chifu wa Kata ya Lupepo, Roman Mwasyeka, alisema kwa sasa uharibifu wa mazingira umekuwa mkubwa nchini hali ambayo inaweza ikasababisha hali mbaya miaka 30 ijayo.

Alisema baada ya tamasha hilo wao wataendelea kuitisha mikutano ya hadhara kwenye maeneo yao kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kutekeleza maagizo ya viongozi wa juu wa serikali.

Mkuu wa Machifu Mkoa wa Mbeya, Rocket Mwashinga, aliwataka machifu wa maeneo mengine ndani ya mkoa huo kufanya matamasha ya utamaduni ili kuwakumbusha wananchi hasa vijana kutunza tamaduni.



Mkuu wa Machifu wa Mkoa wa Mbeya, Rocket Mwashinga, akizungumza na wananchi wa Kata ya Kisiba wilayani Rungwe wakati wa tamasha la utamaduni la kufunga mwaka 2022 lililofanyika juzi kwa lengo la kuhamasisha utunzaji wa mazingira. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Aomba msaada wa fedha kumwezesha kupata matibabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Mtaa wa Benki Mwanjelwa mkoani hapo, Mariam Mwakaleke amewaomba wasamaria kumsaidia fedha kwa ajili ya matibabu kutokana na kuugua kwa zaidi ya miaka sita ugonjwa ambao haujulikani.

Mwanamke huyo ambaye kwa sasa amelala kitandani kwa zaidi ya miaka sita bila kuinuka kutokana na kuugua ugonjwa ambao unasababisha viungo vyake kukosa nguvu na kufa ganzi kwa muda mrefu huku akikosa fedha za matibabu.

Akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake juzi, Mariam alisema awali alikuwa anatibiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Mbeya ambako ilishindikana kupata tiba.

Alisema baada ya kushindikana walimhamishia katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambako ilishindikana kutibiwa kutokana na kukosa fedha jambo ambalo lilimlazimu kurejea nyumbani ambako anaendelea kugulia.

Alisema kwa sasa hali ni mbaya kutokana na kutojiweza na anauguzwa na mwanawe ambaye ndiye anahangaika kutafuta chakula na kumhudumia.

"Mimi ni mjane na nina mtoto mmoja tu, hapa nilipo siwezi kuinuka hata kukaa kitandani, muda wote nalala tena nalalia upande mmoja na najisikia maumivu makali sana, sina msaada wowote, naomba Watanzania wenzangu wanisaidie," alisema Mariam.

Alisema hali aliyonayo kwa sasa ni mbaya na kinachomkwamisha kupata matibabu ni ukosefu wa fedha, hivyo akawaomba wasamalia wema kumsaidia.

Alisema kutokana na hali aliyonayo hawezi kufanya kazi yoyote ya kumwingizia kipato hali inayofanya maisha kuwa magumu zaidi kwake ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa chakula.

Alisema anaishi kwenye nyumba ya kupanga ambayo hajalipa kodi kwa muda mrefu na hivyo kufanya deni kuwa kubwa na ana wasiwasi kwamba anaweza akafukuzwa muda wowote.

Mtoto wa mama huyo, Samson Mwanjala, alisema yeye ndiye anayemhudumia mama yake na hawana msaada mwingine wowote wa matibabu tangu alipoanza kuugua.

Alisema anafanya kazi ya kusukuma matoroli Mwanjelwa ili kupata fedha kwa ajili ya kumhudumia mama yake.

Hivyo aliwaomba Watanzania kumsaidia kupata fedha kwa ajili ya kumhudumia mama yake na kueleza kuwa kitendo cha kulala muda mrefu kitamsababishia matatizo mengine ya kiafya ambayo yanaweza yakawa vigumu kutibiwa.

Alisema mama yake kwa sasa amekata tamaa ya maisha hivyo anahitaji msaada wa hali na mali ili kunusuru maisha yake.





# TMB yateketeza kilo 171 za nyama ya ng'ombe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BODI ya Nyama Tanzania (TMB) imeteketeza kilo 171 za nyama ya ng'ombe yenye thamani ya Sh. milioni 1.2 na kumtoza faini ya Sh. 300,000 mfanyabiashara Elisha Daudi kwa kuuza bidhaa hiyo bila kukaguliwa na wataalam.

Faini hiyo inajumuisha kosa la kusafirishwa kwa bidhaa hiyo kwa usafiri usiotakiwa (pikipiki) hivyo kuhatarisha usalama kwa walaji.

Uteketezaji wa nyama hiyo ulifanyika mwishoni mwa wiki mkoani hapo baada ya timu ya wataalamu wa mifugo kutoka TMB kwa kushirikiana na Mtaalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufanya operesheni ya kushtukiza katika bucha.

Ukaguzi huo ulikuwa na lengo la kubaini wafanyabiashara wa nyama wanaofanya shughuli zao kinyume na Sheria ya Tasnia ya Nyama Namba 10 ya Mwaka 2006.

Ofisa Mifugo wa Bodi hiyo, Alex Mkenda, alisema sababu ya kuteketezwa kwa nyama hiyo ni kutokana na mifugo kutokaguliwa na kuchinjwa kwenye machinjio yaliyosajiliwa na TMB, hivyo kukosa uhalali na usalama kwa walaji.

Alisema sababu nyingine ya kuteketeza nyama hiyo ni ubebaji wa bidhaa hiyo kwa kutumia pikipiki kinyume na sheria ya ubebaji ambayo inaelekeza yatumike magari maalum yaliyosajiliwa na TMB.

"Usafirishaji wa nyama kutoka kwenye machinjio hadi kwenye bucha unapaswa kufanywa kwa kutumia magari ya kubebea nyama tu yaliyokaguliwa na kusajiliwa na Bodi ya Nyama Tanzania lengo likiwa ni kuhakikisha usalama wa nyama unazingatiwa,"alisema Mkenda.

Ofisa Mifugo wa Kata ya Viwandani mkoani Dodoma, Elia Mtamwa, alisema licha ya elimu ya nyama bora, safi na salama kutolewa wafanyabiashara wengi bado wamekuwa wakirudia makosa.

Mtamwa alisema kutofuata sheria kwa wafanyabiashara kuna sababishwa na matukio ya wizi wa mifugo ambayo inachinjwa kiholela na kisha kuuzwa katika bucha bila kukaguliwa na wataalamu wa nyama.

Kadhalika alisema mapambano dhidi ya wafanyabiashara wanaochinja kiholela mifugo na kusafirisha kimagendo ni zaidi ya vita dhidi ya dawa za kulevya kutokana na biashara kufanyika usiku na kusafirishwa zimefungashwa kwenye mifuko isiyo salama.

Muuzaji wa nyama iliyoteketezwa, Elisha Daudi, alikiri kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali na kuahidi kutorudia tena makosa hayo.




Mkurugenzi wa kituo cha habari kuhusu ulemavu akizungumza kwenye kongamano la wadau wa elimu jumuishi wakiwamo wazazi na watumishi wa serikali (hawapo pichani) lililofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Simbachawene akipongeza kikundi kuchangia madawati

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amekipongeza kikundi cha vijana cha kisima umoja kwa kuchangia madawati katika Shule ya Msingi Kisima.

Alitoa pongezi hizo juzi alipofanya ziara ya kutembelea na kuzungumza na wananchi wa Kibakwe Halmashauri ya Mpwapwa.

"Vijana wameweza kuchangia madawati 14 yenye thamani ya Sh. milioni moja, ni jambo kubwa na vijana wengine igeni mfano wa vijana hawa."

Aliongeza: "Wamekumbuka nyumbani wameona wadogo zao wakae mahali pazuri kwa kuamua kutengeneza madawati na umoja wao ni wa watu ambao hawana kitu lakini ni umoja ambao unadhamira. Jambo la msingi katika maisha ni kuwa na dhamira na jambo lako, kwa sababu Mungu anabariki mipango, Mungu anabariki dhamira".

Kiongozi wa kikundi hicho, Kepher Mdachi, alisema malengo yao ni kuendelea kusaidia jamii katika kero mbalimbali ambazo ziko ndani ya uwezo wao.

"Kutoa hamasa kwa wanafunzi ili kuongeza ufaulu, kutoa elimu kwa jamii kwa kuwafikia wazazi na walezi ili kuwahamasisha umuhimu wa elimu kwa vijana wao," alisema.

Mdachi alisema kikundi hicho kimelenga kujenga taasisi imara itakayolenga kusaidia watu na kufanya jambo la kijamii kila mwisho wa mwaka ikiwa pamoja na kusaidia sekta ya afya kwa kuchangia vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya afya wilayani hapo.

# Viongozi CCM wapigwa msasa kuhusu utendaji kazi

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

CHUO cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI) kimetoa mafunzo kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Dodoma Mjini kuhusu kuboresha utendaji wa kazi.

Utoaji mafunzo hayo umefanyika baada ya Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Ramadhan Kailima, kukiagiza chuo hicho kurudisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa madiwani na viongozi wengine pindi wanapochaguliwa ili kuondoa migogoro baina ya viongozi wa serikali za mitaa na chama.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Donald Mejeti, aliwataka viongozi wa CCM kuwa watiifu na wasimamizi wazuri wa mali za umma ikiwa ni pamoja na kuhoji pale ambapo wanaona haki za wananchi zinaminywa.

"Ilani ya CCM ndiyo inayotekelezwa sasa na nyinyi ndiyo wasimamizi wakuu wa ilani na Chuo cha Hombolo kinatekeleza ilani hivyo wakaona watuongezee elimu ya utekelezaji wa ilani," alisema Mejeti. Aidha, alisema viongozi hao wanapaswa kuwasaidia wananchi ili kutoa nafasi kwao kuwa na imani na chama hicho na kuongeza kuwa hiyo ndiyo itakuwa tiketi ya ushindi wa kishindo wakati wa uchaguzi.

Mejeti aliwataka viongozi hao kutumia vizuri mada zitakazofundishwa katika mafunzo hayo ikiwamo ya ujasiriamali ili kutengeneza uchumi wao.

"Nimeona kwenye ratiba kuna mada ya ujasiriamali nendeni mkatengeneze uchumi kwasababu huwezi kutatua shida ya mtu kama hauna kitu mfukoni na ili tuwe sehemu ya kutenda haki lazima tutengeneze uchumi wetu kwanza," alisema.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Lameck Mashala, alisema lengo la mafunzo hayo ni kutekeleza agizo la serikali katika kutoa elimu kwa viongozi kuhusu namna ya kuuishi uongozi na kwamba hatua hiyo ni mchango wa mamlaka za serikali za mitaa katika kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

Alisema LGTI kina wajibu wa kutoa mafunzo hayo ili kushirikiana na serikali kwenye malengo makuu ya kitaifa ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kutekeleza kikamilifu ilani ya CCM kwa vitendo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, Charles Mamba, alisema kuwa mafunzo hayo ni ya viongozi wa CCM Dodoma Mjini yenye kata 41.

"Niwaombe mkitoka hapa mkawe wazungumzaji wazuri na mtakayoyapata hapa mkawaelekeze wenzenu wa chini," alisema Mamba.





Baadhi ya washiriki wa kongamano la Siku ya Haki za Binadamu wakifuatilia mada, lililoandaliwa na Kituo cha Huduma na Sheria Zanzibar, Kijangwani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Meli ya MV Maendeleo yauzwa kwa Dola 230,000

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeshauza Meli ya MV Maendeleo kwa Dola za Marekani 230,000 baada ya meli hiyo kutofanya kazi zake kwa muda mrefu kutokana na kuharibika.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Uchukuzi, Nadil Abdullatif, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mkoani, Abdallah Hussein Kombo aliyetaka kujua meli hiyo imeuzwa kwa kiasi gani.

Naibu waziri huyo alisema kabla ya meli hiyo ya MV. Maendeleo kupelekwa kwenye eneo la matengenezo (chelezoni) ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 500,000.

Alisema baada ya matengenezo ambayo hayakukamilika kutokana na kuwa Serikali ilifanya maamuzi mengine ya kuuza, meli hiyo ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 370,000.

Alisema Serikali ya Zanzibar ilitumia Dola za Marekani milioni 1.5 kuitengeneza meli hiyo kabla haijafanya maamuzi ya kuiuza.

**Naibu waziri huyo alisema kabla ya meli hiyo ya MV. Maendeleo kupelekwa kwenye eneo la matengenezo (chelezoni) ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 500,000.**

# SMZ yatoa ufafanuzi umiliki wa Msitu wa Kichunjuu

**Na Rahama Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema Msitu wa Kichunjuu haujaingizwa katika Hifadhi ya Taifa kwa sababu haumilikiwi na serikali bali ni mkusanyiko wa mashamba ya watu binafsi ya mikarafuu na eneo la makaburi.

Alitoa ufafanuzi huo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Mtambile, Mohammed Mgaza Jecha, aliyetaka kujua endapo msitu huo umo katika Hifadhi ya Taifa.

Waziri Shamata alisema Wizara ya Kilimo haihusiki na wala haina taarifa ya uwapo wa shughuli za ukusanyaji wa mapato unaofanywa katika eneo hilo kutokana na watalii wanaofika kutembelea vivutio katika msitu huo.

Katika hatua nyingine alisema serikali imetumia gharama kubwa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji katika kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji.

Alisema hiyo imetokana na umuhimu wa kilimo hicho kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao.

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha vipindi virefu vya jua na mvua zisizotabirika, serikali imekipa kipaumbele kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na tatizo hilo.

“Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili serikali pia imetekeleza mradi wa miundombnu ya umwagilijai wenye ukubwa wa hekta 1,053 katika mabonde sita ya Cheju, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Kinyasini na Mlemele,” alisema.

Shamata alisema mradi tayari umeshaanza kutumika katika Bonde la Cheju (hekta 314), Bonde la Kinyasini lenye hekta 184 na Mlemele (hekta 44) ambapo wakulima 4,796 tayari wameshakabidhiwa bonde zao kwa kuendelea na kilimo.

Hata hivyo alisema mkandarasi anamalizia marekebisho madogo katika Bonde la Kilombero, Chaani na Kibokwa ili yakabidhiwe kwa wakulima waendelee na kilimo chao kama wenzao.

# ‘Jamii ipewe fedha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa taasisi isiyo ya serikali ya CCI-CENTER, Timothy Ndezi, amesema katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni lazima jamii iwezeshwe fedha ili kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti hasa katika maeneo ya fukwe.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar wakati akifungua mkutano wa kujadili athari za mabadiliko ya tabianchi na kueleza kuwa mamlaka zinapaswa kutambua shughuli zinazofanywa na jamii katika kuinusuru nchi na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mara nyingi mashirika makubwa ya kimataifa pekee ndiyo yanayofaidika na fedha zinazoelekezwa katika miradi ya kukabili maafa ikiwamo mabadiliko ya tabianchi.

Alisema katika ngazi ya chini, wananchi wanaunda jumuiya zinazofanya kazi kubwa ya kuhifadhi mazingira lakini mchango wao hauonekani.


Mtaalamu wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira Hispania, Prof. Venesa Broto, alisema kunapotokea mabadiliko ya tabianchi ni muhimu kujua wananchi katika jamii wanafanya nini na kutafuta namna ya kuwawezesha.

Alisema kwa kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi ni makubwa, ulimwengu unatafuta fedha kwa ajili ya kupambana na athari hizo.

Broto alisema kwa kutambua ushiriki wa jumuiya ndogo katika jamii katika kutatua athari hizo ni vyema serikali na mashirika ya kimataifa wakathamini mchango wa wananchi na kuwaorodhesha kwenye mipango yao na kuwawezesha kifedha.

Mkurugenzi wa Shirika la Kuwezesha Jamii (URAS) kutoka Malawi, Dk. Mtafu Manda, alisema Malawi hakuna taka isiyokuwa na thamani bali hutharifiwa na kugeuzwa vitu vyenye manufaa ikiwamo mbolea kwa ajili ya kilimo.

Manda ambaye ni mwalimu wa Chuo Kikuu cha Mzuzu Malawi alisema miongoni mwa taka hizo ni chupa za plastiki ambazo wamejifunza kutengeneza kitaalamu kwa kujengea nyumba.





# Ulevi uliokithiri chanzo cha wanawake kubakwa Kata ya Didia

**Na Neema Sawaka,**
SHINYANGA

MWENYEKITI wa Kitongoji wa Danduhu, Kata ya Didia, mkoani Shinyanga, Kwezi Ramadhani, amesema wanawake wa kitongoji hicho wanaendekeza vitendo vya ulevi hali inayowasababishia kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kubakwa.

Alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa kesi nyingi ambazo wamekuwa wakizipokea ofisini hapo zinahusiana na vitendo vya ubakaji wanavyofanyiwa wanawake wanaolewa pombe.

Kwezi alikuwa kwenye hafla ya utekelezaji wa mradi wa sauti za kaya na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na klabu ya waandishi wa habari mkoani Shinyanga kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Alisema wanawake wa kata hiyo wanalewa pombe kupindukia pamoja na baadhi ya wanaume wasio waadilifu ambao baadaye huwageuka na kuwabaka.

"Wakishalewa usiku wakati wa kurudi nyumbani njiani hubakwa na wengine kufanyiwa vitendo vibaya vya ukiukwaji wa maadili na ukatili wa jinsia na wanakuwa hawana kumbukumbu ya watu waliowatendea," alisema.

Hivyo aliwataka wanawake hao kuacha ulevi na kueleza kuwa hiyo ndiyo itakuwa njia pekee ya wao kujiepusha na kufanyiwa ukatili wa jinsia.

Mtendaji wa Kata ya Didia, Jackson Maganga, alisema kupitia dawati la jinsia na Polisi Kata wamekuwa wakipita mara kwa mara kwenye mitaa ya mji huo kutoa elimu juu ya vitendo viovu wanavyofanyiwa wanawake wakishalewa pombe.

Alisema pia wanatoa elimu ya kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria kwa sababu kuna baadhi ya waathirika hawatoi taarifa sehemu husika pindi wanapofanyiwa vitendo vya ukatili.

Alisema; "Ili kupunguza vitendo hivi tumekuwa tukizuia ufunguaji wa vilabu vya pombe asubuhi na badala yake wanafungua jioni hali ambayo imesaidia vijana wengi kuacha kulewa kuanzia asubuhi."



Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wakiendelea na kazi za uchimbaji katika mgodi wa Nyamahuna wilayani Geita mkoani Geita. **PICHA: ALPHONCE KABILONDO**

## DC aagiza watumishi kulinda tunu za taifa

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

MKUU wa Wilaya ya Geita mkoani Geita, Wilison Shimo, amewaagiza watendaji wa serikali kulinda tunu za taifa pamoja na kuweka mbele suala la umoja, amani, mshikamano na uzalendo.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru liliofanyika Mjini Geita.

Shimo alisema Wilaya ya Geita inahitaji uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo miradi ya kilimo cha umwagiliaji, umeme, maji, upimaji na kwamba mambo hayo yanahitaji kuwapo kwa umoja, amani na mshikamano.

Alisema waasisi wa taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Aman Karume walikemea ubaguzi, uvivu na rushwa na walitanguliza moyo wa uzalendo na kudumisha amani upendo na mshikamano.

Aliongeza kuwa wananchi wa Geita wanatakiwa kijipima katika vitu hivyo pamoja na kulinda tunu za taifa.

Mchumi wa Wilaya ya Geita, Ndaro Samson, alisema kuwa kulikuwa na tawala saba za kimila lakini kwa sasa viongozi wanachaguliwa kwa njia ya kidemokrasia.

Alisema kwa upande wa elimu, wakati nchi inapata uhuru kulikuwa na shule moja ya sekondari, lakini kwa sasa zimeongezeka na kila kata kuna shule.

Kuhusu sekta ya afya alisema mwaka 1957, Wilaya ya Geita ilikuwa na hospitali moja lakini kwa sasa zipo nne na vituo vya afya 14.

# Ukosefu taulo za kike wasababisha wanafunzi kuwashwa wakiwa hedhi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Masegwa wilayani Shinyanga wamesema huwa wanajisikia hali ya kuwashwa sehemu za siri pindi wanapotumia njia za kienyeji kijisitiri wakati wa hedhi.

Walieleza hayo wakati wakizungumza na Nipashe lililofika shuleni hapo.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa wanafunzi hao, Tatu Lukasi, alisema wanapokuwa shuleni hupewa taulo za kike kwa ajili ya kujisitiri, lakini wakati wa likizo wanapokuwa nyumbani hutumia njia za kienyeji ambazo zinawasababishia madhara.

"Tunashukuru hapa shuleni tunapewa taulo za kike kwa ajili ya kujisitiri tunapokuwa hedhi, tunaporudi nyumbani au tukiwa likizo tunatumia njia za kienyeji ikiwamo kuweka vitambaa ambayo hatujui kuna usalama kiasi gani kwa sababu lazima upatwe na muwasho sehemu za siri," alisema Tatu.

Aliongeza: "Lakini tunapotumia hizi taulo za kike ambazo tunapewa hapa shuleni huwezi kupatwa miwasho yoyote ile na tunasoma bila wasiwasi kabisa".

Mwanafunzi mwingine, Kulwa Dotto anayesoma alisema siyo kila mara huwa wanapewa taulo la kike shuleni, kuna siku wanakosa na hivyo kulazimika kutumia njia za kienyeji ikiwamo kuweka vitambaa.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Masengwa, Twaha Swalehe, akizungumza kwa niaba ya Mwalimu Mkuu Msaidizi, alisema wamekuwa wakitenga bajeti ya kununua taulo za kike na kuwapatia wanafunzi ili wasiwe watoro.

Alisema wanafunzi wa maeneo ya vijijini wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa taulo za kike na wengi wao hutumia njia za kienyeji ambazo siyo salama.

Alisema kutokana na tatizo hilo shule iliamua waanzishe utaratibu wa kununua taulo za kike na kuwapatia wanafunzi ili wawe salama na kuhudhuria vipindi vyote darasani.

"Licha ya kutoa taulo za kike kwa wanafunzi, inafikia kipindi bajeti yetu inakuwa ndogo, tunashindwa kutoa huduma stahiki, tunaomba wadau watusaidie kupata taulo za kike, tulikuwa tuna tatizo la chumba maalumu cha kubadilishia nguo tumelitatua, wanafunzi wakifungulia shule Januari mwakani wataanza kukitumia," alisema.

Mmoja wa wazazi wenye watoto katika shule hiyo, Janeth Nkuba, alikiri kuwapo na tatizo kwa watoto wao pindi wanapokuwa nyumbani wanatumia njia za kienyeji kujisitiri wanapokuwa hedhi.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Elifuraha Elieza Mbwambo T/A Mau Petrol and Service Station, S.L.P 12465, Arusha. | Kiwanja Namba 1, Kitalu "J", Eneo la Oloresho, Kata ya Olasiti, Arusha. | Elifuraha Elieza Mbwambo (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 2. | Gapco Tanzania Ltd – Monduli, S.L.P 9103, Monduli – Arusha. | Kiwanja Na. 307,309 na 311, Kitalu "R", Monduli, Arusha | Jean Francoise (Raia wa Ubelgijii) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 3. | Ally Joseph Karanjay, S.L.P 125, Ngorongoro – Arusha. | Kiwanja Na. 23, Kitalu "E", Eneo la wasso, Ngorongoro, Arusha. | Ally Joseph Karanjay (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 4. | Mount Meru Petroleum Ltd – Meru 7, S.L.P 7094, Arusha Mjini – Arusha | Kiwanja namba 43, Kitalu "HH", Eneo la Themi, Arusha. | Attul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Mount Meru Petroleum Ltd – Karatu, S.L.P 7094, Karatu – Arusha. | Kiwanja namba 1322, Kitalu "G", Eneo la Karatu mjini, Arusha | Attul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Ryoba Tindo Wambura T/A Tindo Filling Station, S.L.P. 68, Tarime | Kiwanja Na. 2073, Kitalu "A", Eneo la Kewanja, Tarime, Mara. | Ryoba Tindo Wambura (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 7. | Washington Jared Benasius T/A Mukendo Agrovet & General Supply, S.L.P. 907, Tarime. | Eneo la Komaswa, Tarime, Mara. | Washington Jared Benasius (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | Olympic Petroleum (T) Limited, S.L.P. 6185, Mwanza. | Kiwanja Na. 242, Kitalu "T", Eneo la Kenyatta Road, Mwanza. | Ally Mohamud Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Marwa William Matiku T/A Williamsons Service Station, S.L.P. 872, Musoma | Kijiji cha Simiyu, Kata ya Migato, Itilima, Simiyu. | Marwa William Matiku (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 10. | BM APEX (T) Limited, S.L.P. 59, Kishapu. | Kiwanja Na. 10&11, Kitalu "B", Eneo la Maganzo, Kishapu, Shinyanga. | Balele Makonda Chole (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 11. | JR Service Station Limited, S.L.P. 74, Muleba. | Kiwanja Na. 46, Kitalu "H", Eneo la Kamanengo – Muleba Mjini, Kagera. | Josephati Method Rweyemamu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 12. | Bukula Company (T) Limited, S.L.P. 183, Magu. | Kiwanja Na. 121&128, Kitalu "Z", Eneo la Barabara ya Kashozi, Bukoba, Kagera. | Sylivester John Bukula (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 13. | Tembo Nickel Corporation Limited, S.L.P. 80512, Dar es Salaam. | Kijiji cha Nyakuguma, Kata ya Bugarama, Ngara, Kagera. | Tembo Nickel Corporation Limited | Leseni ya Kituo cha Mafuta Matumizi Binafsi |
| 14. | Ngara Oil Tanzania Limited - Kabanga Petrol Station, S. L. P. 318, Ngara, Kagera. | Kiwanja Na. 95, Kitalu "A", Eneo la Kabanga Mjini, Ngara, Kagera. | Ally Suleiman Hillal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 15. | Ngara Oil Tanzania Limited - Nzaza Petrol Station, S. L. P. 318, Ngara, Kagera. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "G", Eneo la Nzaza, Kabanga, Ngara, Kagera. | Ally Suleiman Hillal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 16. | Tilu Amos Nsimba, S. L. P. 1006, Katoro, Geita. | Kiwanja Na. 180, Kitalu "A", Bugayambelele "A", Katoro, Geita. | Tilu Amos Nsimba (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 17. | Punguja Luhumbika Majani, S.L.P. 170, Chato. | Eneo la Rutunguru, Kata ya Muganza, Chato, Geita | Punguja Luhumbika Majani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Issa Ramadhan Nais, S.L.P 42, Babati – Manyara. | Kijiji cha Endanoga , Kata ya Galapo, Babati, Manyara | Issa Ramadhan Nais (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 19. | Eliyasa Shabani Kisisa S.L.P 98, Kiteto – Manyara, | Kiwanja Na. 77, Kitalu "C", Eneo la Matui, Kiteto, Manyara. | Eliyasa Shabani Kisisa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 20. | Amin Habibu Punja – Kimana Petrol station, S.L.P 80, Kiteto – Manyara. | Kijiji cha Kimana, Kata ya Partimbo, Kiteto, Manyara. | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 21. | Amin Habibu Punja – Njoro Petrol station, S.L.P 80, Kiteto – Manyara. | Kijiji cha Njoro, Kiteto, Manyara | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 22. | Amin Habibu Punja – Engusero Petrol station, S.L.P 80, Kiteto – Manyara. | Kijiji cha Engusero , Kiteto, Manyara | Amin Habib Punja (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 23. | GG – Oil Tanzania, S.L.P 12699, Arusha. | Kijiji cha Dirma, Kata ya Dirma, Hanang, Manyara. | Charles Gidamoni Gapchojiga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 24. | Tanzanite Petrol Station, S.L.P 8570, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 7, Kitalu "A", Eneo la Mjohoroni, Moshi, Kilimanjaro. | Deogratias Isdori Assenga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 25. | Mount Meru Petroleum Ltd – Moshi 2 Himo Njiapanda, S.L.P 7094, Moshi Mjini – Kilimanjaro. | Kiwanja Na.797 & 799, Kitalu "F", Eneo la Himo njiapanda, Moshi vijijini, Kilimanjaro. | Attul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 26. | Mount Meru Petroleum Ltd – Handeni, S.L.P 7094, Handeni – Tanga. | Kiwanja Na. 113, Kitalu "F", Eneo la Chanika, Handeni, Tanga. | Attul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 27. | Khamisi Isuja Gaga, S.L.P 155, Tabora. | Eneo la Kijiji cha Atta, Kondoa, Dodoma. | Khamisi Isuja Gaga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Anuari Almasi Kihodogo, S.L.P 34, Rujewa, Mbeya | Eneo la Kijiji cha Itunundu, Iringa Vijijini, Iringa. | Anuari Almasi Kihodogo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Gapco (T) Ltd – Forest Hill Service Station, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1447, Kitalu "M", Eneo la Forest, Mbeya. | Jean-Francois Schoepp (Raia wa Ubeligiji) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 30. | Emmanuel Joel Mboya – Imarq Filling Station, S.L.P 865, Mbeya. | Kijiji cha Ruanda, Kata ya Santilya, Mbeya. | Emmanuel Joel Mboya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 31. | Mbeya Highway Service Station, S.L.P 229, Mbeya. | Kiwanja Na. 1411, Kitalu "M", Eneo la Forest, Mbeya. | Mehbooba Alnoor Bhanji (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 32. | Summer Estate Limited, S.L.P 702, Mbeya. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "A", Ikamambande, Busokelo, Mbeya. | John J. Summer (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 33. | GMS Oil & Lubricants Co. Ltd – GMS Oil Filling Station | Kiwanja Na. 9, Kitalu "D, Kijiji cha Mageuzi, Namtumbo, Ruvuma. | George Abraham Mwalongo (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 34. | SLEM Oil, S.L.P 761, Songea. | Kiwanja Na. 3, Kitalu "A", Shule ya Tanga, Songea, Ruvuma. | Exavery Lucas Msigwa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 35. | Madema Company Limited, S.L.P 62, Mpanda. | Kiwanja Na. 22, Kitalu "A", Kawajense, Mpanda, Katavi. | Andrea Ernest Madema (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 36. | Werema William Mwita – Muhoji Filling Station, S.L.P 7619, Mwanza | Kijiji cha Litundu, Wang'ing'ombe, Njombe. | Werema William Mwita (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 37. | Gapco (T) Ltd – Sumbawanga Service Station, S.L.P 9103, Mbeya. | Kiwanja Na. 1, 2 & 3, Kitalu "AA", Eneo la Mazwi, Summbawanga, Rukwa. | Jean-Francois Schoepp (Raia wa Ubeligiji) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 38. | Tristar Energy Tanzania Limited S.L.P. 50101, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 22, Eneo la Chang'ombe, Temeke, Dar es Salaam. | Eugene Aloysious Mayne (Raia wa India) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 39. | Sinohydro Corporation Limited, S.L.P. 70589, Dar es Salaam. | Eneo la Yombo Vituka, Ilala, Dar es Salaam | Guo Kun (Raia wa China) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 40. | Novores Construction Close Corporation Company Limited, S.L.P 31901, Dar es Salaam. | Eneo la Msasani, Kinondoni,Dar es Salaam. | Qian Fangfang (Raia wa China) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 41. | Octavian Revelian Stambuli, S.L.P. 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1082, Kitalu "H", Eneo la Flamingo Madale, Kinondoni, Dar es Salaam | Octavian Revelian Stambuli (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 42. | Africa Energy Ltd, S.L.P. 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 493, Kitalu "I", Eneo la Temeke, Dar es Salaam | Edhah Abdallah Munif. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 43. | Gapco Tanzania Limited-Oysterbay Service Station, S.L.P. 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 3 & 4, Kitalu "40", Eneo la Oysterbay, Kinondoni, Dar es Salaam | Jean-Francois Michel M.Shoepp (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 44. | Top Oil Petroleum Limited, S.L.P. 42445, Dar es Salaam. | kiwanja Na. P13610, Eneo la Mbezi, Ubungo, Dar es Salaam. | Mbarak Salim Bawazir. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 45. | Rosemary Ruwaichi Mosha, S.L.P. 40388, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1681&1682, Kitalu "A", Eneo la Bonyokwa, Ilala, Dar es Salaam. | Rosemary Ruwaichi Mosha. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 46. | Lake Oil Limited Msasani Mwisho Dar Es Salaam, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | kiwanja Na.706&707, Kitalu "B", Eneo la Msasani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 47. | Lake Oil Limited Msasani Village Dar Es Salaam, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P21601, Eneo la Msasani Village, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 48. | Lake Oil Limited Buguruni Mataa Dar Es Salaam, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1136/1&1138/1, Kitalu "A", Eneo la Buguruni, Ilala, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 49. | Oilcom (T) Ltd - Mikwambe Petrol Station S.L.P. 20831, Dar es Salaam. | Eneo la Ponde Mtaa, Kigamboni, Dar es Salaam. | Ameir Munif Abdallah Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50. | Gulf Agreegate Limited S.L.P. 5055, pwani. | Eneo la Lugoba, Bagamoyo, Pwani. | Ally Edha Awadh. (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 51. | Christina Fredrick Marandu, S.L.P. 30112, Pwani | Eneo la Kibondeni, Kibaha, Pwani. | Christina Fredrick Marandu (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 52. | Ngamila Tanzania Limited, S.L.P. 80476, Pwani. | Kiwanja Na.10, Eneo la Vigwaza, Chalinze, Pwani. | Godfrey Jafary Chaula (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 53. | Petroafrica (T) Limited-Miomboni Service Station, S.L.P. 4878, Pwani. | Kiwanja Na.4, Eneo la Miomboi/Misugusugu, Kibaha, Pwani. | Yassin Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 54. | Acer Petroleum (T) Ltd-Kisemvule, S.L.P. 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 13, Eneo la Kisemvule, Mkuranga, Pwani. | Atul Mittal. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 55. | ATN Kichangani, S.L.P. 683, Morogoro. | Kiwanja Na.5, Eneo la Kichangani, Morogoro. | Abdulatif Taalib Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 56. | Ismail Abdulaziz - Madina Filling Station, S.L.P. 93, Mtwara. | kiwanja Na.20, Kitalu "D", Eneo la Mji Mpya, Tandaimba, Mtwara. | Ismail Abdulaziz Ismail. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

17192502

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.152/ 2022**
**In the matter of the Estate of the late MATHIAS MARTIN MKONGELWA**
**Of Kikuyu within Dodoma Region**
**And**
**In the matter of the application for letters of administration by JUSTUS MARTIN MKONGELWA.**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **29 Day of 11, 2022**
Dated at Dodoma this 20TH day of October, 2022

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA LESENI YA MAKAZI YA KUMILIKI ARDHI

**Sheria ya Uandikishaji Ardhi**
**(Sura 334)**

Mmiliki: **Anyamle Benard Luoga wa S.L.P LUDEWA**
Namba ya Kiwanja: **65 Kitalu Eneo la Ibani Juu.**
NA
Namba ya Kiwanja:**63 Kitalu Eneo la Ibani Juu.**
Muombaji: Samora Benard Luoga Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Benard Luoga wa **S.L.P 327** Makambako.
Taarifa imetollewa kwamba Leseni ya Makazi ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudi kutoa leseni mpya ya kumiliki ardhi. Iwapo hakuna pingamizi lolote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la serikali.
Leseni ya makazi ya asili ninaomba irejeshwe ka Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Ludewa **S.L.P 19 LUDEWA, NJOMBE.**
**08.12.2022**

## KUPOTEA KWA LESENI YA UDEREVA

Ndugu **SAIDI ABRAHMAN KIROBOTO** anatangaza kupotelewa na leseni ya udereva yenye namba **4000465048.** Amefika Polisi na kupewa Loss Report: **MUH/RB/595/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 2373/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RAJABU MASHAKA PEMBE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABDULKHERI RAJAB PEMBE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 Mwezi wa 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 8 Mwezi wa 12 Mwaka 2022.

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LTD, Sisi RAISSA COMPANY LTD** tunatangaza mnada wa hadhara wa kuuza mali (dhamana) za mdaiwa sugu aliyekopa na kushindwa kulipa deni lake. Mnada utaendeshwa kama

| Mdaiwa/ Mdhamini | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Ally Shomari Mrungula | Photocopy Mashine- Canon # IR2318 –Tawi la Mbagala | 27.12.2022 |
| Ali Shomari Mrungula | Printer Epson # L382 – Tawi la Mbagala | 27.12.2022 |

**Mashati Mengine:-**
Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kubeba mali iliyouzwa ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**RAISSA CO LTD Phone no. 0652113262**
**Tujijenge (TZ)+255 222774742-3/0677045064**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SALUMU SAIDI NGUMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **SAN LG** yenye usajili namba: **T 252 BBC.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB/465789/2022**

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1123 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late HILLARY FIDELIS MAGHALI**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**ROSE PAULO CHUMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 06th day of February, 2023.
**Dated at DAR ES SALAAM this 5th day of December, 2022.**

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MURO INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T369AXL** aina ya **YUTONG.** Chassis No. **2X71024024,** Engine No. **DF50917230.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/474992/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI ARUSHA**
**MAOMBI YA MADAI NA.34 YA MWAKA 2022**
**EVA.....ELILIMA MAWOLE...MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**BOSCO THADEI KOMBA....MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
**BOSCO THADEI KOMBA**
**EVA ELILIMA MAWOLE** amewasilisha shauri la maombi ya madai ya kesi namba 34 ya mwaka 2022 mbele ya mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha. Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 14/12/2022 saa 08:30 asubuhi.Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuhudhuria bila kukosa.Endepo hautatekeleza,maombi hayo yataendelea upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa muhuri na Mahakama ya Hakimu Mkazi leo tarehe 7/12/2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI ARUSHA.

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Huddah aleta taharuki

**Na Mwandishi Wetu**

MREMBO Huddah Monroe, amezua taharuki kwenye mitandao ya kijamii baada ya kujitambulisha upya akijiita mke na mke wa mtu.


Kupitia Instagram yake Huddah aliweka picha yake akiwa na mwonekano mpya ambapo kwa mara ya kwanza alionekana amefunga kitambaa kichwani na kuvalia nguo zilizositiri sehemu kubwa ya mwili wake kinyume na mavazi yake ya kawaida.

Alisema kuwa yeye licha ya kuwa binti na mfanyabiashara mkubwa, pia ni mke wa mtu na mama.

Mitandaoni, watu hawakuwa na tatizo na Huddah kujiita binti na mfanyabiashara kwa sababu hilo linafahamika wazi kuwa ana ufanisi mkubwa sana katika bidhaa zake za kujipodoa.

Lakini pale alipojiita mke wa mtu na mama, wengi walitaka kujua ni lini amepata mtoto kwa sababu kwa muda mrefu amekuwa akionekana kulipuuzia mbali kabisa suala la kupata mtoto.

"Mimi ni mfanyabiashara mkubwa, binti, mama na mke wa mtu," aliandika Huddah.





# MWIJAKU KUMSHTAKI KAJALA

**Na Mwandishi Wetu**

MTANGAZAJI na 'chawa' maarufu, Mwijaku amemgeuka Kajala na sasa anadai kuwa ataelekea mahakamani kumfungulia kesi ya ulaghai na kumharibia msanii Harmonize muda wake kwa zaidi ya miezi mitano.

Mwijaku aliweka video ya Harmonize akimvisha pete Kajala ya Juni mwaka huu ambapo yeye ndiye alikuwa mshereheshaji mkuu na kusema kuwa alimuuliza Kajala kurudia maneno yake.

Kajala anasikika akirudia maneno yake kwa Harmonize akimpa hakikisho kuwa atampenda leo, kesho na hadi milele.

Mwijaku amesema Kajala alikuwa mnafiki kwa maneno yake na ndio maana akamwomba arudie huku akijifanya kuwa hakusikia mara ya kwanza.

"Hapa nilivyo mwambia rudia nilitaka kujihakiki, je, hii inatoka ndani ya moyo wake? Na alivyokuwa...akirudia nikajua ni mnafiki," Mwijaku aliandika kwenye video hiyo.

Alisema kuwa sasa anabakia na hatua ya kuelekea mahakamani kumfungulia Kajala kesi ya kuharibu muda na mali ya msanii Harmonize na mwisho wa siku kukiuka maneno yake kuwa atampenda muda wote.

"Nakwenda kufungua kesi ya madai mahakamani kesho (leo) ya kumpotezea muda msanii," aliandika Mwijaku.

# *Harmonize, Sallam mambo shwari*

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara ya kwanza mwanamuziki na CEO wa Konde Ganda, Harmonize amekutana na kusalimiana na bosi wake wa zamani ambaye ni Meneja wa Lebo ya WCB, Sallam SK, visiwani Zanzibar.

Harmonize ambaye yuko visiwani humo kwa ajili ya shoo yake, amekutana na Sallam ambaye walikuwa na ugomvi mkubwa ambao uliibuka baada ya Harmonize kujitoa WCB na mara kadhaa wawili hao walifanya mahojiano na kila mmoja kuzungumza mabaya ya mwenzake ambayo alimfanyia.

Tukio lililoibua gumzo na kuthibitisha kwamba wawili hao wana vita, ni pale ambapo Sallam SK alipokataa mkono wa salamu wa Harmonize kwenye msiba wa mke wa Babu Tale mkoani Morogoro mnamo Juni mwaka 2020, na baada ya hapo yaliibuka maneno mengi.

Video inayosambaa mitandaoni inaonyesha kwamba wawili hawa wamemaliza tofauti zao na kwa sasa wana maelewano mazuri ndio maana kwenye video Harmonize amemwambia Sallam kwamba anampenda sana.



# TAIFA JANG'OMBE SASA YAGEUKIA USAJILI DIRISHA DOGO KUJINUSURU

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI dirisha dogo la usajili na uhamisho wa wachezaji limefunguliwa leo visiwani Zanzibar, 'Wakombozi Wang'ambo' timu ya Taifa Jang'ombe, wamejipanga kuhakikisha wanasajili wachezaji watakaoibakisha Ligi Kuu Zanzibar.

Taifa Jang'ombe msimu huu imeanza vibaya kwa kuangukia vipigo 10 katika michezo yao 15 waliyocheza ya mzunguko wa kwanza huku wakiwa wanaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 14, ambayo timu nne za mwisho zitashuka daraja mwisho mwa msimu huu wa 2022/2023 kwa mujibu wa kanuni.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Omar Khamis 'Matu', alisema wamejipanga kuhakikisha wanasajili wachezaji vitasa watakaoisaidia timu hiyo kufanya vizuri katika mzunguko huu wa lala salama.

**Alisema miongoni mwa nafasi ambazo wamejipanga kusajili wachezaji hao ni safu ya ushambuliaji pamoja na nafasi ya ulinzi ambazo ndio ilikuwa changamoto kubwa kwa timu hiyo.**

Alisema ni mapema kuweka wazi wachezaji hao watatoka katika timu gani, lakini mipango yao ni kusajili wachezaji kutoka klabu za Ligi Kuu Zanzibar na wengine kutoka nje ya Zanzibar.

"Tunataka kusajili wachezaji ambao wataisaidia timu kuibakiza katika Ligi Kuu, tunajua tunaenda katika mzunguko wa vita kila timu ikihitaji kumaliza vizuri, na sisi katika michezo yetu 15 ya mzunguko huu wa pili tunataka kuitumia vizuri ili tuinusuru kushuka daraja," alisema.

Aidha, akizungumza juu ya wachezaji ambao wamepanga kuwaacha, alisema kuna baadhi tayari wameondoka mara tu walipomaliza mzunguko wa kwanza na wapo wachezaji ambao watakaachana nao.

Hata hivyo, alisema timu hiyo itaanza mazoezi yake mapema ili kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar utakaoanza Januari mwakani.

## Agyei kumrithi Mbrazil Singida Big Stars

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Singida Big Stars, uko katika mchakato wa kuinasa saini ya aliyekuwa nyota wa Azam FC, Enock Atta Agyei, kutoka nchini Ghana kuelekea usajili wa dirisha dogo linalofunguliwa Alhamisi wiki hii, imeelezwa.

Nyota huyo aliyewahi kuitumikia Azam FC mwaka 2016 na baadaye kutemwa na 'Wanalambalamba' hao, 2019 hadi 2020 alijiunga na Klabu ya Horoya AC ya Guinea na sasa ni mchezaji huru.

Agyei anayeweza kucheza winga wa kushoto na kulia, yuko katika mazungumzo ya kutua ndani ya kikosi cha Singida Big Stars kuchukuwa nafasi ya Mbrazil Peterson Silvano Da Cruz aliyevunja mkataba na klabu hiyo kwa sababu ya matatizo ya kifamilia na kurejea kwao Brazil.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jana kutokana ndani ya uongozi wa Singida Big Stars, zimeeleza kuwa mazungumzo kati ya pande hizo mbili yamefikia mahali pazuri na muda wowote anaweza kuja nchini kujiunga na kikosi hicho.

"Ni kweli nyota huyo tunafanya naye mazungumzo na yanaenda vizuri kuja kuitumikia timu yetu kipindi cha usajili wa dirisha dogo ili kuongeza nguvu ndani ya kikosi chetu," kilieleza chanzo chetu.

Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hassan Massanza, alisema kwa sasa suala la usajili limeachiwa benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu Hans Van Pluijm.

Alisema kuhusu nyota wao Da Cruz, amevunja mkataba kwa sababu ya matatizo ya kifamilia na tayari amerejea kwao Brazil.

"Usajili tutafanya kulingana na mapendekezo ya benchi letu la ufundi, nani na nani watasajiliwa hilo suala litakuja baada ya kupokea ripoti ya kocha, kwa sasa tunaendelea kujiandaa kwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Massanza.

HUNIWEZI...




Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akimtoka beki wa Kurugenzi FC kwenye mechi ya raundi ya 64 ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na Yanga kushinda mabao 8-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba iko salama asema Try Again

**Na Saada Akida**

HUKU akiweka mikakati yao hadharani ikiwamo kuimarisha benchi la ufundi liwe bora zaidi na kuleta kocha mkuu mwenye viwango bora, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amesema Simba ni imara na salama na kuwaomba wanachama wa klabu hiyo kupuuzia porojo za wasioitakia klabu yao mema.

Kikosi cha Simba kwa sasa kipo chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda anayeongoza timu hiyo katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Try Again (pichani), alikanusha propaganda zinazoenezwa na wasioitakia mema klabu yao ikiwamo suala la kupokonywa basi lao akieleza kuwa lipo katika matengenezo chini ya wadhamini wao, Africaries.

Alisema mikakati yao kwa sasa ni kuimarisha benchi la ufundi kuwa bora zaidi kwa kuleta kocha mkuu na kutumia vema dirisha la usajili kwa kufanya usajili bora wa wachezaji bora kulingana na mapendekezo ya ripoti ya benchi la ufundi linaloongozwa na Mgunda kwa sasa.

"Kufanya usajili bora na sahihi na wa nguvu ili kuiboresha timu yetu iweze kuwa tayari kupambana kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika pia kuendelea kupambana kwenye Ligi Kuu ili kuchukua ubingwa kwa msimu huu," alisema Tyr Again.



Alisema wanahitaji kufanya maboresho ndani ya kikosi chao kwa kuleta wachezaji watakaofanikisha kufikia malengo yao hayo kwa kuanza vizuri kampeni yao ya michezo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Mwenyekiti huyo alisema mipango mingine ni pamoja na kufanya uchaguzi huru ili kupata viongozi bora wa kuiongoza klabu ya Simba baada ya uongozi ulioko sasa kumaliza muda wake.

"Naomba wapenzi na wanachama tupuuze porojo za wasioitakia mema klabu yetu, niwaondoe hofu Wanasimba kwani Simba iko salama na imara hayo mengine yanaletwa ili kutuondoa katika malengo," alisema mwenyekiti huyo.

## ZISIKUPITE

### PSG YAMTAKA RASHFORD

KLABU ya Paris St-Germain iko tayari kumfanya mshambuliaji wa England, Marcus Rashford, 25, kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi wakiwa wanamtaka, huku mkataba wake na Manchester United ukimalizika msimu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### GUARDIOLA ATAKIWA BRAZIL

SHIRIKISHO la Soka la Brazil linapanga kuwasiliana na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, ili kujua kama angependa kuwa kocha wa timu ya taifa mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

### GVARDIOL AWINDWA CHELSEA

CHELSEA, Manchester City na Manchester United zimewasilisha ofa kwa mchezaji wa kimataifa wa Croatia, Josko Gvardiol, 20, huku Bayern Munich pia wakimtaka beki huyo wa RB Leipzig. ***(Foot Mercato)***

### PULISIC APIGIWA HESABU

KLABU ya Newcastle inatumaini kumsajili mshambuliaji, Christian Pulisic, 24, huku Arsenal na Manchester United pia wakifuatilia hali ya mchezaji huyo. ***(Mirro)***

### FELIX ATAFUTIWA SOKO

WAKALA wa mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, 23, ambaye tayari amefanya mazungumzo ya awali na Chelsea na Manchester United, anatarajia kuzungumza na Aston Villa na Newcastle United kuhusu kiwango chao cha kutaka kumnunua mshambuliaji huyo wa Atletico Madrid. ***(Mirro)***

### JUVE YAMGEUKIA MOUNT

KLABU ya Juventus inaweza kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na England, Mason Mount, 23, na kumwachia mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 28. ***(CalcioMercatoWeb)***

### BENFICA KUMZUIA COSTA

RAIS wa Benfica, Rui Costa, amesema klabu haitamruhusu mchezaji wake yeyote muhimu, akiwamo mshambuliaji wa Ureno mwenye umri wa miaka 21, Goncalo Ramos, kuondoka. ***(Correio da Manha)***

### NEWCASTLE KUACHIA NNE

KLABU ya Newcastle itamruhusu beki wa kati wa England, Jamaal Lascelles, 29, na beki wa kushoto wa Ireland ya Kaskazini, Jamal Lewis, 24, pamoja na winga wa Scotland, Matt Ritchie (33) na Ryan Fraser (28), kuondoka Januari. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YAMTAKA FELIX

KLABU ya Arsenal imeingia kwenye orodha ya klabu zinazomwania Joao Felix. ***(AS - In)***

### DALOT KUONGEZWA MKATABA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema klabu hiyo itatumia chaguo la kuongeza mkataba wa Marcus Rashford na beki wa kulia wa Ureno Diogo Dalot, 23, hadi 2024 huku wakijadili kuongezwa kwa mkataba wa wawili hao. ***(Metro)***

### TRAORE NA UHAMISHO

KIUNGO wa kati wa Mali, Boubacar Traore, 21, anatarajiwa kutimiza masharti katika uhamisho wake wa mkopo kwenda Wolves kutoka Metz. ***(Express & Star)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE ATESEKA KWA FIKRA ZA KUJIUZULU ENGLAND

**LONDON,** England

**Nataka kufanya uamuzi sahihi, hisia zangu zimekuwa ngumu kufikiria vizuri katika...**

KOCHA wa England, Gareth Southgate, "anazozana" anapofikiria mustakabali wake katika nafasi hiyo kutokana na timu hiyo kutolewa katika robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa wiki iliyopita.

**Southgate aliweka wazi baada ya kipigo cha mabao 2-1 Jumamosi dhidi ya Ufaransa kwamba, hataharakisha kufanya maamuzi kuhusu mustakabali wake, huku chama cha soka kikiwa kimeacha wito huo mikononi mwake.**

Kocha huyo wa England, ambaye aliiongoza timu hiyo kufika nusu fainali ya Kombe la Dunia 2018 na fainali ya Euro 2020, amekuwa kocha tangu 2016 na ana mkataba hadi Desemba 2024.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52, alitangaza kuwa anataka kufurahia Kombe la Dunia 2022, akiwa na kipindi "kigumu" baada ya England kufungwa kwa mikwaju ya penalti na Italia katika fainali ya Euro 2020.

"Nimeona sehemu kubwa za miezi 18 iliyopita kuwa ngumu," alisema Southgate.

"Kwa kila kitu ambacho nimependa kuhusu wiki chache zilizopita, bado nina miezi 18.

"Ninachotaka kuhakikisha, ikiwa ni jambo sahihi kubaki, ni kwamba hakika nimepata nguvu ya kufanya hivyo. Sitaki kuwa miezi minne au mitano chini ya mstari nikifikiria."

Southgate ameibadilisha England tangu ilipotoka katika hatua ya 16-bora ya Euro 2016 na kuwa mshindani wa kweli wa mataji makubwa.

Beki huyo wa zamani wa England hakuwa na muda wa kuamua ni lini angefanya uamuzi kuhusu mustakabali wake, akisema alikuwa na hamu ya kushinda hisia za kushindwa.

"Nilipopitia mashindano machache yaliyopita, hisia zangu zimekuwa ngumu kufikiria vizuri katika wiki chache zinazofuata," alisema.

"Nataka kufanya uamuzi sahihi kwa njia yoyote ile kwa sababu ni lazima iwe haki ya kwenda tena, au sahihi kutokwenda tena, na sidhani sasa ni wakati wa kufanya uamuzi kama huo siku chache zijazo."

SportPesa
LIVE IN PLA

MECHI KALI
ARGENTINA
VERSUS
CROATIA
1 | 1.82
X | 3.30
2 | 4.60

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEYMAR ATOA YA MOYONI



**SAO PAULO,** Brazil

NEYMAR anaendelea kutatizika kukubaliana na kutolewa kwa Brazil katika Kombe la Dunia, akisema kwamba "bado naumia kwa kupoteza".

Brazil waliopewa nafasi kubwa ya kutwaa Kombe la Dunia nchini Qatar, walitolewa na Croatia kwa mikwaju ya penalti 4-2 baada ya mchezo kuisha kwa sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 120.

Neymar, ambaye alifunga bao katika muda wa ziada, lakini hakupiga mkwaju wa penalti, aliandika kwenye Instagram Jumamosi kwamba "nimeharibikiwa kisaikolojia".

"Katika ardhi ya Brazil... bado inauma kama kuzimu kutokana na kupoteza, tulikuwa karibu sana, karibu sana," aliandika Neymar. "Kwa bahati mbaya au nzuri bado sijajifunza kushindwa, kushindwa kunanifanya niwe na nguvu zaidi, lakini kunaniumiza sana na bado sijazoea.

"Hata hivyo, lazima tuendelee... maisha yanasonga, hata yakiuma na maumivu yanachukua muda kupona, lazima tuendelee. "Kwa mara nyingine tena nataka kuwashukuru watu wa Brazil kwa msaada wao na upendo wao. Kusikia kutoka kwao kwamba tulipigana, kutolewa hadi mwisho kunafariji kidogo ya maumivu yetu.

"Asante Qatar kwa kila kitu. Kombe lilikuwa zuri na ilibidi atoke Brazil ili kutwaa yote, lakini kwa majaliwa ya Mungu haikuwa hivyo."

Imekuwa ikikisiwa kuwa hii itakuwa michuano ya mwisho kwa Neymar mwenye umri wa miaka 30, na alisita kujitolea kuichezea nchi yake mara tu baada ya mchezo.



## Deschamps kuamua mwenyewe

**DOHA,** Qatar

DIDIER Deschamps ataamua yeye mwenyewe kama atabaki kuwa kocha mkuu wa Ufaransa baada ya Kombe la Dunia Qatar 2022, kwa mujibu wa Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, Noel Le Graet.

Deschamps alichukua nafasi ya kocha wa Ufaransa mwaka 2012 na tangu wakati huo ameiongoza 'Les Bleus' kutwaa taji la Kombe la Dunia pamoja na fainali ya Euro 2016, akiwa ameshinda mechi 103 wakati wa uchezaji wake.

Timu yake ya Ufaransa iliishinda England Jumamosi na kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia nchini Qatar, na kuweka hai matumaini yao ya kuwa timu ya kwanza tangu Brazil mwaka 1962 kutetea kombe hilo.

Mkataba wa Deschamps unatarajiwa kumalizika baada ya michuano hiyo, huku tetesi zikisema kuwa kocha mkuu wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane anaweza kuchukua nafasi hiyo.

Hata hivyo, Le Graet anatumaini Deschamps atachagua mwenyewe.

"Tuna bahati kuwa n kocha mzuri (Deschamps wafanyakazi wazuri wa ki fundi," alisema Le Graet a iliambia gazeti la L'Equip "Wachezaji wanahitaji k hakikishiwa, tuna timu y wasimamizi wa hali ya ju karibu nao.

"Suala la kuongeza muda juu yake kabisa, kutafuta k cha wa ubora huu si rahisi. yeye anayeamua, natumai atasema ndiyo. "Lakini ba inastahili, haswa kwa upan wake, kutafakari."

CHEZA USHINDE KASINO

# MZIZE AAHIDI MAKUBWA YANGA

Na Shufaa Lyimo

BAADA ya kuonyesha kiwango cha hali ya juu wakati akiisaidia timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 8-0 dhidi ya Kurugenzi FC kwenye mechi ya Kombe la FA, mshambuliaji kinda wa Yanga, Clement Mzize (pichani), amesema ataendeleza ushindani kwenye michezo yote atakayopewa nafasi ya kucheza ili kuipa mafanikio klabu yake hiyo.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, Mzize alifunga mabao manne.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mzize alisema malengo yake ni kufanya vizuri kwenye kila mchezo atakaoucheza ili kuweza kufikia malengo yake na ya klabu.

**"Ninaahidi kufanya vizuri kwenye michezo yangu yote nitakayocheza ili nitimize ndoto yangu, lakini kuiwezesha klabu kufikia malengo yake," alisema Mzize.**

Alisema anatamani kuwa mshambuliaji wa kutegemewa ndani ya timu hiyo huku akiweka wazi kufurahishwa na ushirikiano anaopewa na wachezaji wenzake.

Akizungumzia mchezo wao wa juzi wa Kombe la Shirikisho dhidi ya timu ya Kurugenzi FC, alisema alifurahi kufunga mabao manne ikiwa ni pamoja kupata zawadi ya mchezaji bora wa mechi.

"Nimefurahi kuwa mchezaji bora katika mchezo wetu dhidi ya Kurugenzi, ushindi huu unanifanya nizidi kujituma zaidi," alisema kinda huyo ambaye ni zao la klabu hiyo akiwa amepandishwa kutoka kikosi cha U-20.



## Hat-trick sita zapigwa FA

INATOKA UKURASA 32

mabao 7-1 dhidi ya Misitu.

Mbali na 'hat-trick', kulikuwa na vipigo vikali vilivyotolewa, ambapo mbali na matokeo hayo, Azam FC pia iliiadhibu Malmao FC mabao 9-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam katika mechi ambayo pamoja na kwamba ilikuwa na idadi kuwa ya mabao, lakini haikuwa na 'hat-trick'.

Kwenye raundi hii, timu zote za Ligi Kuu zimeonekana kupeta na sasa inasubiriwa droo ya raundi ya tatu, jumla ya timu 32 zikiwa zimesalia kwenye michuano hiyo.

## Simba Raja, Yanga Watunisia

INATOKA UKURASA 32

iliyo kwenye kundi moja na Yanga. Mabingwa walichapwa bao 1-0 ugenini Tunisia, na kulazimishwa suluhu nyumbani.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na CAF jana Simba itaanzia ugenini nchini Guinea dhidi ya Horoya FC kati ya Februari 10-12, kabla ya kurejea nyumbani kuikaribisha Raja Casablanca Februari 17-19 na kisha Februari 24-26, mwakani kuifuata Vipers ya Uganda.

Kwa upande wa Yanga nayo itaanzia ugenini nchini Tunisia dhidi ya US Monastir Februari 12 na kisha kurejea nyumbani kuikaribisha TP Mazembe Februari 19 kabla ya kuhitimisha raundi ya kwanza kwa kuifuata Real Bamako ya Mali Februari, 26, mwakani.

Akizungumzia kuhusu droo hiyo, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wanafahamu timu walizopangiwa nazo nzuri, hivyo kundi litakuwa gumu.

Alisema kuna muda wa kujipanga kwa sababu mashindano hayo yanatarajiwa kuanza Februari mwakani na sasa Kocha wao, Juma Mgunda atapata nafasi ya kuwasoma wapinzani.

"Siwezi kusema lolote juu ya hili kundi, kiufupi tunajua ubora wa hizi timu, ninaamini baada ya kutoka kwa haya makundi kocha (Mgunda) ataanza kufuatilia, nadhani baada ya hii leo (jana) anaweza kusema lolote," alisema Meneja huyo.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wameona makundi hayo na wanatambua litakuwa kundi gumu kwao kwa sababu timu watakazocheza nazo ni nzuri, lakini wanaendelea kufanya maandalizi kupitia michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ili kujiimarisha na hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kwa sasa tunaendelea na ligi, inatusaidia kufanya maandalizi ya michuano hiyo, tunaheshimu kila timu katika hili kundi, tutaanza kufuatilia taarifa zao katika baadhi ya michezo yao, kwa kuona ubora na madhaifu ya wapinzani wetu," alisema kocha huyo.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 13/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 2864 | Persebaya Surabaya vs Persik Kediri | 1.61 | 3.69 | 4.76 |
| 13:00 | 4445 | Keshla FK vs Zira | 6.04 | 3.80 | 1.49 |
| 13:30 | 4650 | St Andrews vs Naxxar Lions | 4.17 | 3.59 | 1.72 |
| 14:00 | 3209 | Persita Tangerang vs Rans Nusantara | 1.96 | 3.07 | 3.80 |
| 15:35 | 2859 | Al Oruba vs Oman Club | 2.55 | 2.85 | 3.05 |
| 15:40 | 1924 | Al Nahda (Oman) vs Sur | 1.45 | 3.74 | 7.00 |
| 15:40 | 5844 | AL Bashair vs AL Musanaa | 3.85 | 3.00 | 2.11 |
| 16:00 | 2899 | Vittoriosa Stars vs Attard FC | 3.84 | 3.60 | 1.78 |
| 16:00 | 3300 | Dire Dawa Kenema FC vs Welayta Dicha FC | 2.75 | 2.85 | 2.80 |
| 16:00 | 4544 | AL Qadsia vs AL Sahel | 1.51 | 4.00 | 5.27 |
| 16:00 | 5163 | Sliema Wand vs Fgura United | 1.65 | 3.78 | 4.36 |
| 16:15 | 4080 | Psis Semarang vs Persija Jakarta | 3.01 | 3.11 | 2.24 |
| 16:30 | 4422 | Mohammedan SC vs Kenkre FC | 1.29 | 4.87 | 8.57 |
| 18:00 | 3003 | Etehad Alreef vs AL Ittihad Bhr | 6.81 | 4.47 | 1.37 |
| 18:00 | 4893 | Legetafo Legedadi vs Arba Minch Kenema | 4.67 | 3.21 | 1.74 |
| 18:00 | 5369 | Karabakh vs Gabala | 1.26 | 5.60 | 10.00 |
| 18:30 | 1582 | San Gwann FC vs Swieqi United FC | 2.60 | 3.40 | 2.55 |
| 18:30 | 4849 | Melita FC vs Lija Athletic | 2.24 | 3.21 | 2.92 |
| 18:40 | 4347 | AL Arabi vs AL Nasr | 1.65 | 3.85 | 4.90 |
| 22:00 | 1559 | Burton vs Accrington | 2.00 | 3.36 | 3.31 |
| 22:00 | 1759 | Plymouth vs AFC Wimbledon | 1.71 | 3.71 | 4.10 |
| 22:00 | 2369 | Lincoln vs Everton U21 | 1.98 | 3.59 | 3.16 |
| 22:00 | 4825 | Argentina vs Croatia | 1.82 | 3.30 | 4.60 |
| 22:00 | 5199 | Portsmouth vs Stevenage | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 22:00 | 5508 | Cheltenham vs Chelsea U21 | 2.00 | 3.60 | 3.11 |
| 22:30 | 2621 | Bristol Rovers vs MK Dons | 2.00 | 3.35 | 3.31 |
| 22:30 | 5856 | Salford City vs Port Vale | 2.78 | 3.17 | 2.36 |
| 22:45 | 1150 | Wrexham vs Chesterfield | 1.63 | 4.04 | 4.43 |
| 22:45 | 1336 | Bolton vs Manchester United U21 | 1.96 | 3.60 | 3.21 |
| 22:45 | 1555 | Notts County vs Gateshead | 1.18 | 6.50 | 11.81 |
| 22:45 | 1667 | Scunthorpe vs Woking | 4.52 | 3.83 | 1.66 |
| 22:45 | 2176 | Dorking Wanderers vs Maidstone | 1.99 | 3.84 | 3.10 |
| 22:45 | 2392 | Aldershot vs Boreham Wood | 3.11 | 3.31 | 2.17 |
| 22:45 | 2419 | Bath City vs Hampton and Richmond | 2.00 | 3.26 | 3.40 |
| 22:45 | 2526 | Barnet vs Yeovil | 1.96 | 3.40 | 3.55 |
| 22:45 | 3007 | Altrincham vs Maidenhead U | 1.93 | 3.45 | 3.60 |
| 22:45 | 3415 | York City vs Solihull Moors | 3.01 | 3.21 | 2.27 |
| 22:45 | 3631 | AFC Fylde vs Farsley Celtic | 1.37 | 4.49 | 6.84 |
| 22:45 | 3981 | Telford vs Kettering Town | 2.01 | 3.37 | 3.27 |
| 22:45 | 4260 | Brackley Town vs Kings Lynn | 2.10 | 3.31 | 3.11 |
| 22:45 | 4318 | Boston Utd vs Banbury United | 2.39 | 3.32 | 2.63 |
| 22:45 | 4898 | Ebbsfleet vs Eastbourne Borough | 1.38 | 4.57 | 6.41 |
| 22:45 | 5038 | Taunton Town vs Farnborough Town | 2.36 | 3.25 | 2.72 |
| 22:45 | 5098 | Dagenham and Redbridge vs Eastleigh | 2.11 | 3.45 | 3.11 |
| 22:45 | 5381 | Cheshunt vs Welling | 2.63 | 3.37 | 2.36 |
| 22:45 | 5509 | Darlington vs Southport | 1.84 | 3.61 | 3.56 |
| 22:45 | 5613 | Hereford United vs Chester | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 22:45 | 5626 | Southend vs Halifax | 1.78 | 3.46 | 4.26 |
| 23:45 | 4346 | Sporting Lisbon vs Maritimo | 1.21 | 6.42 | 11.04 |
| 23:45 | 5946 | Rio Ave vs Sporting Farense | 2.06 | 3.30 | 3.55 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Desemba 13, 2022

Nipashe




Southgate ateseka fikra kujiuzulu UKURASA 29




MGUNDA

NABI

# Simba yapewa Raja, Yanga na Watunisia

Adam Fungamwango na Saada Akida

**Zote kuanzia ugenini, wapinzani wao wanakimbiza msimamo ligi za nyumbani, makocha wasema...**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, Simba wakipangwa kukutana na Waarabu wa Morocco, Raja Casablanca, mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga wenyewe wamerejeshwa tena Tunisia kuwavaa US Monastir huku pia wakiwa na shughuli pevu dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

**Kwa mujibu wa droo ya michuano hiyo inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Februari 12, mwakani, iliyotolewa jana Cairo nchini Misri, Simba imepangwa Kundi C ikiwa na Vipers FC ya Uganda ambayo ilitinga hatua hiyo ya makundi kwa kuiondosha TP Mazembe kwa penalti 4-2 kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa nchini DR Congo, baada ya kutoka suluhu ka-tika mechi zote mbili. Mbali na Vipers na Raja Casablanca, kundi hilo pia imo Horoya FC ya Guinea.**

Horoya inaongoza ligi nchini Guinea ikiwa haijapoteza mechi yoyote, ikicheza michezo minane ikishinda saba na sare moja, ikijikusanyia jumla ya pointi 22, Vipers ikiwa ya pili kwenye msimamo wa ligi nchini Uganda kwa pointi 23, ikicheza mechi 11, ikishinda saba, sare mbili na kupoteza mbili, huku Raja Casablanca ikiwa kwenye nafasi ya tano ya msimamo wa nchi yao, ikiwa na pointi 12 kwa mechi nane ilizocheza, ikishinda mechi tatu, sare tatu na kupoteza mbili.

Mabingwa wa Afrika, Wydad Casablanca wameangukia kwenye Kundi A, wakiwa na Atlético Petroleos de Luanda ya Angola, JS Kabylie ya Algeria, na AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo.

Kundi B wapo mabingwa wa kihistoria Al Ahly ya Misri ikipangwa kukutana na mahasimu wao wakubwa Mamelodi Sundowns, Al Hilal ya Sudan ambayo iliwaondosha Yanga kwenye Ligi ya Mabingwa, na Coton Sport ya Cameroon, huku Kundi D likiwa na 'Waarabu' watupu Esperance ya Tunisia, Zamalek ya Misri, CR Belouizdad ya Algeria na Al Merrikh ya Sudan.

Kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Yanga itakutana na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ikipangwa kwenye Kundi D, pamoja na timu za Real Bamako ya Mali na US Monastir ya Tunisia.

Yanga inaonekana kuwa na faida ya kupangwa na TP Mazembe ya DR Congo, nchi ambayo ina wachezaji wengi ambao wanaichezea timu hiyo, lakini Real Bamako ipo kwenye nchi ambayo kipa Djigui Diarra anakotokea.

Faida nyingine ni kwamba, Yanga itakwenda tena nchini Tunisia, sehemu ambayo ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi ya kombe hilo ilipoichapa Club Africain bao 1-0, lakini Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi anatokea huko.

US Monastir inashika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu ya Tunisia ambayo inachezwa kwa makundi, ikiwa Kundi B, ikicheza mechi tano, kushinda tatu, sare moja na kufungwa moja ikimiliki pointi 10, TP Mazembe ikiwa kwenye nafasi ya nne kwenye Ligi ya Jamhuri ya Congo kwa pointi 15, ikicheza mechi saba, kushinda nne na kutoa sare tatu, huku Real Bamako ikishika nafasi ya pili kwa alfabeti ikifanana kila kitu na Djoliba, zote zikiwa na pointi 14, zikicheza mechi sita, kushinda nne na sare mbili.

Kwenye Kundi A, kuna timu za USMA ya Algeria, Marumo Gallants ya Afrika Kusini, Al Akhder ya Libya ambayo iliiondosha Azam FC na St Eloi Lupopo ya Afrika Kusini, huku Kundi B likiundwa na timu ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, Diables Noirs ya Congo Brazzaville, Rivers United ya Nigeria na DC Motema Pembe ya DRC.

Kundi C la michuano hiyo zipo timu za Pyramids ya Misri, Asco de Kara ya Togo, Future ya Misri na Asfar ya Morocco.

Michuano hiyo inachezwa huku ikiwa haina bingwa mtetezi kutokana na mabingwa, RS Berkane ya Morocco kutolewa katika mechi za mchujo na US Monastir

INAENDELEA UK. 31

## Hat-trick sita zapigwa FA

Na Adam Fungamwango

RAUNDI ya pili ya Kombe la Shirikisho la Soka maarufu FA Cup, imekamilika ikishuhudiwa baadhi ya timu zikipata vipigo vikubwa, huku 'hat-trick' sita zikipatikana.

Wachezaji walioweka rekodi ya kupiga 'hat-trick' ni Mosses Phiri wa Simba, Andrew Sinchimba wa Ihefu, Clement Mzize wa Yanga, Sadala Lipangile wa KMC, Ismail Mgunda wa Tanzania Prisons na Richardson Ng'onya wa Mbeya City.

Ng'ondya ndiye mchezaji wa kwanza kutupia 'hat-trick' kwenye raundi hii, akifunga mabao manne yaliyoiwezesha timu yake kuishindilia Stand FC 5-1, mechi ikichezwa Desemba 9, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Desemba 10, Phiri naye aliweka mabao manne kwenye mechi nyingine ya raundi ya pili ya Kombe la FA, Simba ikishinda mabao 8-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Eagle FC ya Dar es Salaam, huku Sinchimba akiwa na timu yake ya Ihefu akitia fora alipopachika jumla ya mabao matano kwenye Uwanja wa Highland Estates, akiiongoza timu yake kutoa kipigo kinono cha mabao 9-0 dhidi ya Mtama Boys.

Straika wa KMC, Lipangile alifunga mabao manne juzi, timu yake ilipoisulubu Tunduro Korosho mabao 6-1, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, na kinda wa Yanga Mzize pia alipachika manne, timu yake ikiondoka na ushindi wa mabao 8-0 dhidi ya Kurugenzi FC, mechi iliyochezwa juzi Jumapili kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mgunda wa Prisons naye juzi alifunga 'hat-trick', wakati timu yake ikishinda

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >